Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 11 Julai, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti, (Mhe. Silvester M. Mabumba) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 173

Kuwapatia Maji Wananchi wa Tarafa ya Mzenga

MHE. SELEMANI S. JAFO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakazi wa Tarafa ya Mzenga kutoka chanzo cha Mto Ruvu kutokana na janga kubwa la ukosefu wa maji linalovikabili Vijiji vingi vya Tarafa hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Tarafa ya Mzenga yenye Kata nne za Mzenga, Vihingo, Kurui na Mafizi zenye jumla ya Vijiji 19 ina tatizo kubwa la upatikanaji wa huduma ya maji. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 15.7 tu ya wakazi wote ndiyo wanaopata maji safi na salama ambao hupata maji toka kwenye visima vifupi, visima virefu na Mto Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti umebaini kwa Vijiji vya Kimalamisale, Gwata, Nyani, Mafizi na Ving'andi ndivyo ambavyo vinaweza kutumia chanzo cha maji cha Mto Ruvu kutokana na kuwa karibu na Mto Ruvu. Aidha Vijiji vya Mzenga A, Vilabwa, Mitengwe, Kibwemwenda, Mzenga B, Sangwe, Chamalale, Mihungwe, Zegero, Kidugalo, Vihingo, Gurui na Mtakayo vitatumia maji ya aridhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua tatizo la maji safi na salama katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Serikali imeanza kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kupitia Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji, Serikali inakusudia kutekeleza mradi wa maji katika Kijiji cha Mafizi kwa kutumia chanzo cha Mto Ruvu.

Halmashauri imepanga kutumia shilingi milioni 146.8 zilizoidhinishwa kwa mwaka 2011/2012 kwa ajili ya mradi wa maji wa Chakenge kwa kutumia maji ya ardhini. Aidha, Halmashauri imeomba shilingi milioni 379.5 katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa ajili ya

mradi wa maji wa Mafizi kwa kutumia chanzo cha Mto Ruvu.

(ii) Katika mwaka wa fedha wa 2012/13, Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Shirika la *Plan International* imepanga kutumia jumla ya shilingi milioni 308 kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji ya bomba wa Mtakayo ambao utahudumia Vijiji vya Kurui na Mtakayo. Vijiji vilivyobaki vitaendelea kujengwa miundombinu kwa kadri rasilimali ya fedha itakavyopatikana.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza, ningelipenda kuwajulisha wafanyakazi wangu wa Wilaya ya Kisarawe pale Kisarawe Mjini sasa hivi maji miezi miwili iliyopita tumemaliza tatizo la umeme lakini nimesikia mgao wa maji bado unaendelea.

Sitakubali katika hili na wakifanya masihara, nitamwambia Waziri Mkuu wazembe wote wanaosababisha wananchi wa Kisarawe waichukie Serikali yao na Viongozi wao, tutawakabidhi kwa Waziri Mkuu. Sasa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kisarawe, mwaka huu tulileta mchakato wa kuleta Bajeti wa kwa maombi maalum kwa ajili ya shida ya maji kama tulivyozungumza hapo awali. Je, Waziri yuko radhi kuridhia ombi letu ambalo tumeleta ombi

maalum kwa ajili ya kufanya *feasibility study* na *detailed design* mradi wa kutatua tatizo la maji?

(b) Kwa kuwa sasa Kisarawe tatizo la maji limekuwa kama ni janga kabisa na ninajua Ofisi ya Waziri Mkuu ina kitengo maalum cha maafa na kule Tarafa ya Chole hivi sasa, hali ni mbaya na tete.

Je, Waziri anatueleza nini Wanakisarawe katika mpango ule wa kuhudumia majanga maalum?

Je, itakuwa tayari kuja kuhudumia katika Tarafa ya Chondesambura ili mradi kuweza kuwaokoa wananchi wale ambao wako katika hali kubwa ya shida ya maji hivi sasa?(*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge huyu anaezungumza sasa hivi, mimi jana nilimsikiliza kwa karibu sana alipotoa hotuba, alipozungumza juzi na jana na utamwona jinsi ambavyo kwa kweli anawapigania wananchi wake kwa maana ya kuweza kupata maji safi na salama.

Hii Tarafa Mheshimiwa anayozungumza ni kweli kwamba wana matatizo makubwa sana. Asilimia 15.7

tu ndiyo ambao wanasaidiwa katika jambo hili. Sasa anazungumza habari ya ombi maalum, hili ombi maalum analolisema, linakwenda kwenda kwenye shilingi milioni mia moja na kitu, Halmashauri hii ya Wilaya ya Kisarawe, yote kwa ujumla kabisa imetengewa karibu shilingi milioni 835 na kama tumemsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Waziri wa Maji alipozungumza hapa, naye aliona kwamba anaridhika kwamba pale pana tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba tulipokee hili tatizo na hili ombi maalum ambalo amelisema hapa ili tukalishughulikie kwa pamoja, pamoja na Mbunge ili tuweze kumwondoa katika hali hiyo.

(b) Lakini la pili amezungumzia Kitengo cha Maafa, sasa Kitengo cha Maafa, Mheshimiwa Lukuvi yuko hapa anasikia na ameeleza kuhusu eneo hili la Chwele, tunafanya wote ofisi moja ni maeneo tu kidogo tumetofautiana, tuko TAMISEMI yeye yuko katika eneo lingine. *I hope* amelisikia, lakini mimi *officially* nitalipeleka kwa Mheshimiwa Lukuvi ili tuweze kusaidiana kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuweze kuona jinsi ya kuisaidia hii Tarafa aliyoisema. (*Makofi*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa *concern* kubwa ya Wabunge humu ndani ni tatizo la maji katika maeneo wanayotoka na kwa uzoefu tumeona baadhi ya miradi ikishindwa kutimiza malengo ya kuwaletea

wananchi wa Tanzania ya maji safi na salama ikiwa mradi wa visima 10 na miradi mbalimbali.

Hii yote inatokana kutegemea fedha nyingi kutoka kwa wafadhili. Sasa je, Serikali kwa mwaka ujao wa fedha, wana mikakati gani ya kuhakikisha wanatenga fedha zetu za ndani ili wananchi wa Tanzania wakiwepo wa Mkoa wa Mara hususani Wilaya ya Bunda, kupata maji safi na salama?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi nadhani jana Mheshimiwa Waziri wa Maji alijieleza vizuri sana hapa kuhusu mkakati ambao wanaendelea nao katika kuhakikisha kwamba maeneo mengi na ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Bulaya kwamba tuna tatizo kubwa sana la maji. Kuhusu Vijiji 10, mlimsikia Waziri alivyosema hapa, akasema ebu twende kwanza na vile Vijiji vitano (5) kwa mwaka huu, halafu tuendelee tuangalie tena mwaka mwingine utakaokuja tuangalie vile Vijiji vingine vilivyobakia pale. Kwa maana hiyo nisingetaka nirudi tena nianze kueleza kile kwa sababu alieleza vizuri sana na kwa ufundi wa hali ya juu sana.

Lakini sasa anazungumzia hili la Bunda, hili la Bunda Mheshimiwa Wasira yuko hapa, amefanya kazi kubwa sana kule, ameweka kisima, umeme, wananchi

wa Bunda sasa hivi wanapata maji, kwa hiyo, tunapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Wasira kwa kazi nzuri anayoifanya pale.(*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, mambo yaliyoko pale Bunda kwa kweli ni mambo mazuri yanayoendelea pale. Kwa hiyo, hatuna wasiwasi. Lakini la mwisho ambalo Mheshimiwa Bulaya analizungumzia hapa, Mheshimiwa Mbunge huyu anasema jambo la msingi sana, kama naelewa vizuri, 60% inatoka ndani katika maana ya Bajeti yetu na 40% inatoka nje. Hii habari ya kuendelea kutegemea Mataifa na ya nje ndiyo yatusaidie katika mambo haya, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge tunakubaliana na wewe kwamba kuna haja ya sisi wenyewe kuanza kuangalia kidogo kidogo kwamba tunafanyaje tujitegemee ili tuweze kuondokana na matatizo ya maji tuliyonayo katika nchi yetu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI kwa majibu mazuri na kwa niaba ya Waziri wa TAMISEMI, naomba nitoe majibu ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Tayari Serikali imeanza kuweka mkakati wa kutumia fedha zake za ndani mwaka 2011/2012, tulitenga bilioni 41 na mwaka huu zimeongezeaka, tumetenga bilioni 140 fedha za ndani ambazo zimeelekezwa kutatua tatizo la maji Dar es Salaam. Kwa hiyo, mwaka ujao tutatenga fedha zaidi ya hapo ili ziende kwenye Vijiji. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 174

Walimu Kupandishwa Vyeo na Kulipwa Stahili Zao

MHE. SALOME D. MWAMBU aliuliza:-

Walimu hucheleweshwa sana kupandishwa madaraja na pia pale wanapohamishwa hawalipwi posho za uhamisho ambazo wanatakiwa walipwe na hivyo kuwavunja moyo na kusababisha matizo ya migomo na kadhalika:-

(a) Je, Serikali itamaliza lini matatizo ya walimu ili nao waishi kama wafanyakazi wengine wa Serikali?

(b) Je, Serikali itachukua hatua gani kwa Wakurugenzi Watendaji wanaochelewa kuwasilisha *"Seniority list"* ambayo hutumika kupandishia vyeo watumishi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa walimu na kuthamini mchango wao mkubwa katika kutoa elimu nchini. Kwa kutambua hilo, Serikali imekuwa ikiboresha huduma kwa watumishi wote nchini wakiwemo walimu na kuchukua

hatua mbalimbali kumaliza matatizo ya walimu ikiwemo; kuboresha viwango vya mishahara, posho nyingine ambazo watumishi au mtumishi anastahili kwa mujibu wa Kanuni.

Sheria na Taratibu zilizopo, kutenga fedha za malipo ya stahili mbalimbali ikiwemo uhamisho katika Bajeti za kila mwaka na kutoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri kuhakikisha kwamba uhamisho unafanyika pale tu ambapo fedha zimetengwa kwa ajili hiyo.

Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 15.8 kwa ajili ya uhamisho kwa walimu wa Shule za Msingi na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ilipata jumla ya shilingi milioni 131.5.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakurugenzi Watendaji kwa mujibu wa ratiba kila robo mwaka wanatakiwa kuwasilisha orodha ya ukubwa kazini (*Seniority list*) kwenye Mamlaka za Wizara na Tume ya Utumishi. Halmashauri zimeendelea kuandaa na kuhuisha kwa wakati orodha ya ukubwa kazini ili kuwa na taarifa sahihi za watumishi. Aidha, Serikali inaendelea kuwasisitiza Wakurugenzi kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kuhakikisha kwamba taarifa zinazohitajika zinaendelea kuwasilishwa katika Mamlaka husika kwa wakati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (ORMUU), imeanzisha matumizi ya mfumo shirikishi wa taarifa za kiutumishi na mishahara (*Human Capital Management System*) ambao utapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la ucheleweshaji wa taarifa za watumishi kuhusiana na upandishwaji wa madaraja.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Mwenyekit, ahsante. Mimi napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri:-

(a) Je wale waliocheleweshwa na ikatokea mpaka wakastaafu yale Madaraja yao watafidiwa ili walipwe stahili yao? Maana yake hata kwenye *pension* wanapunjika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, je wale watumishi Serikalini waliocheleweshwa kwa makusudi madaraja ya hao watu, Serikali itawachukulia hatua gani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salome Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

(a) Swali la kwanza kwa watumishi wale wote ambao wamecheleweshwa kupandishwa madaraja yao na sasa wamefariki, lakini inaonekana kuwa wamepunjwa stahili zao, bado suala la uhakiki wa

utumishi wao na madaraja yao ili kuweza kuyatambua unaendelea na kwa kuwa nyaraka zao zote ziko katika kila Halmashauri walimokuwa wanafanyia kazi.

Jambo hili litakuwa linaendelea kadiri ambavyo anatakiwa mtumishi na stahili zake ili aweze kulipwa haki zake na zitaingizwa kwenye madai yake ya mirathi pale ambako yule aliyeteuliwa kuwa mrithi ambaye atakakuwa anafuatilia madai hayo atakapokuwa anawasilisha pia na hili na Idara ya Utumishi inatambua hilo.

(b) Suala la watumishi ambao walisababisha ucheleweshwaji wa madaraja haya, watachukuliwa hatua gani? Kwa utaratibu tuliouweka na kwa kuwa sasa tunaendelea kuhuisha watumishi hawa waliosababisha bado wanaingia katika utaratibu wa kiutumishi wa kuona kwamba wanawajibika kufanya kazi yao vizuri na pindi itakapothibitika kwamba jambo hili walilitenda kwa makusudi, hatua za kinidhamu na za Kisheria zitachukuliwa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika swali la msingi, Serikali iliulizwa Serikali itamaliza lini matatizo ya walimu na matatizo ya walimu yako maeneo mengi nchini ikiwemo katika Jimbo la Ubungo.

Katika majibu Mheshimiwa amezungumza kwamba matatizo hayo ni pamoja na masuala ya mishahara, madai ya posho na mengineyo. Kwa kuwa hivi karibuni walimu wametangaza mgogoro na Serikali, ningeomba kupata jibu kutoka kwa Serikali, ni

lini haswa haya matatizo yatakamilika ili kuepusha mgogoro kati ya walimu na Serikali unaojirudia mara kwa mara?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikanushe kwamba, Walimu wametangaza mgogoro kwa sababu, ziko taratibu za utangazaji wa mgogoro.

Swali la Serikali, litamaliza lini matatizo ya walimu, ni swali la msingi ambalo kila mtumishi anahitaji kujua na hasa walimu, ili pia wasiingie kwenye migogoro ambayo sio muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu – *TAMISEMI,* imeandaa utaratibu kabambe wa kuhakikisha kwamba, tunamaliza matatizo ya walimu kwenye sekta zote.

Kwanza tumeimarisha Sekretarieti za Mikoa, ambazo zitakuwa zinasimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa maana ya Halmashauri, kwa ukaribu ili kuhakikisha kwamba, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa maana ya Halmashauri, zinaratibu kikamilifu taratibu zote za walimu na watumishi wengine, ili kila mtumishi aliyeko katika Halmashauri, anapata haki yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu wa uimarishaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuziimarisha pia Sekretarieti za Mikoa, maeneo yote mawili, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zitakuwa zinafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kwamba, watumshi katika Mikoa yao, watumishi katika Halmashauri, wanaratibiwa taratibu zao za kiutumishi pamoja na stahili zao, wakiwemo walimu, bila kusababisha migogoro katika maeneo ya kazi.

Huo ndio mkakati ambao kwa kweli, Serikali, imejipanga kuhakikisha kwamba, tunakomesha matatizo yote, yakiwemo na ya walimu. *(Makofi)*

Na. 175

Fedha Kwa Ajili ya Ujenzi wa Barabara ya Njombe Lupembe kwa Lami

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (K.n.y. MHE. DEO K. SANGA) aliuliza:-

Barabara ya Njombe – Lupembe, ilijadiliwa katika Kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Iringa na kupitisha uamuzi wa kuijenga kwa kiwango cha lami. Lakini katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 haikutengewa fedha:-

Je, katika Mwaka wa Fedha 2012/2013 barabara hiyo itatengewa fedha, ili iweze kujengwa kwa kiwango hicho cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kaseyenda Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Njombe – Lupembe, yenye urefu wa kilometa 66 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS).* Ni kweli, mwaka 2011/2012 barabara hiyo, haikutengewa fedha za kujenga kwa kiwango cha lami, kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Mwaka 2012/2013, barabara hiyo ya Njombe hadi Lupembe, itafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ili baadaye fedha zikipatikana iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa sasa, barabara hiyo, itaendelea kufanyiwa matengenezo, ili iwe inapitika wakati wote wa mwaka.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, tunataka kufahamu ni lini? Tunataka *commitment* ya Serikali, lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Menyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, barabara hii inafanana kabisa na barabara iliyoko katika Jimbo la Mufindi Kaskazini ya Kinyalambosi kwenda Madibira. Je, ni lini Serikali, itaanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgimwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya kwanza anauliza lini? Kwenye jibu la msingi nimesema katika mwaka huu wa fedha ambao umeanza hii Julai mpaka Juni mwakani, tutaanza kufanya upembuzi yakinifu. Sasa katika huo muda hiyo kazi, maana kuna taratibu zake, kwanza ni lazima uanze kumtafuta huyo msanifu, kuna *procedure.* Kwa hiyo, awe na uhakika mwaka huu kazi hiyo inaanza ya usanifu. Ujenzi utaanza baada ya usanifu kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika swali la pili, namwomba sana Mheshimiwa Mgimwa, kwa sababu, barabara hii haikuwa kwenye Swali la Msingi, atuletee ili tumpe majibu ili wananchi wa Mufindi, waweze kupata majibu sahihi.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na ujenzi wa barabara za lami unaoendelea kote nchini, lakini kumekuwa na uwekaji wa *strips* na *humps* katika hizo barabara, usiozingatia viwango. Mfano mzuri ni barabara ya Katesh kwenda Singida, ambako kumewekwa *humps* na *strips* kila baada ya dakika 5, hivyo kusababisha usumbufu mkubwa sana kwa madereva na magari kuharibika. Napenda kufahamu kutoka kwa Waziri, ni lini Serikali,

itaondoa zile *humps* au kupunguza kabisa kwa sababu, zimekuwa zikisababisha usumbufu mkubwa sana?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli baadhi ya *strips* na *humps* ambazo zimejengwa kwenye barabara nyingi hapa nchini, haziko kwenye kiwango ambacho Wizara imeshatoa. Tumeshawaagiza Mameneja wa *TANROADS* Mikoa yote, zile *humps* na *strips* ambazo haziko kwenye *standards* ambayo Wizara imetoa, ziondolewe mara moja. *(Makofi)*

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza. Mwaka jana, wakati Waziri Mkuu, akifanya ziara Wilayani Tarime, aliwaahidi wananchi wa Tarime kuwa, kuna barabara inayotoka Mangucha kupitia Masanga – Kitawasi – Gibaso hadi Mulito, ataipandisha hadhi kutoka barabara ya Halmashauri kuwa, barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Vikao halali vimeshakaa na kuipitisha hiyo barabara kuwa barabara ya Mkoa. Naomba *committment* ya Serikali, ni lini itatenga hela kwa ajili ya hiyo barabara?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba

kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyangwine, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, kupandisha hadhi barabara ni lazima ifuate Sheria ambayo Bunge hili liliipitisha, kuna Taratibu zake. Bodi, inaweza kutoa mapendekezo, lakini kuna taratibu hadi ile barabara iweze kupandishwa. Baada ya kupandishwa hadhi, sasa tunaingia kwenye mchakato wa kuzifanyia mipango endelevu ya kuzitengeneza barabara, zile nyingine zitengenezwe kwa kiwango cha lami, nyingine zinatengenezwa kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa itabidi tuangalie maombi haya yamefikia *stage* gani. Kwa sababu, ni barabara nyingi ambazo zimependekezwa kutoka Mikoa mbalimbali. Kwa hiyo, baada ya kujua imefikia hatua ipi, Mheshimiwa Mbunge, tutamjulisha.

Na. 176

Ukosefu wa Chuo Kikuu Katika Jiji la Tanga

MHE. AMINA M. MWIDAU aliuliza:-

Jiji la Tanga linakabiliwa na ukosefu wa Shule za Kutwa kwa kidato cha V na VI, pamoja na Chuo Kikuu.

(a) Je, Serikali, ina mikakati gani kuanzisha Shule za Kutwa, kwa Kidato cha V na VI katika Jiji la Tanga?

(b) Je, Serikali, haioni kuwa, sasa ni wakati muafaka wa kujenga Chuo Kikuu katika Jiji la Tanga, ili kuwezesha wanafunzi wa Tanga, kupata Elimu ya Juu na pia kuinua uchumi wa Jiji la Tanga?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa, Jiji la Tanga lina shule 3 za Kidato cha V na VI na shule 21 za Kidato cha I – IV *("O – Level")* za Serikali. Utaratibu wa kuanzisha Kidato cha V katika Shule ya Kutwa popote nchini, huanzia kwa Mkuu wa Shule kuomba kibali kwa Kamishna wa Elimu baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Kwa sasa, Jiji la Tanga tayari limeteua shule 2 za Macechu na *Old Tanga,* ili zipandishwe hadhi na kuwa za *"A – Level".* Hata hivyo, ukaguzi wa awali umeonesha kuwa shule hizi bado hazijatimiza vigezo vyote. Mchakato wa kukamilisha vigezo vilivyosalia unategemea kukamilika mwaka wa fedha 2012/2013, ili ziweze kuanza kupokea wanafunzi mwakani mwezi Aprili, 2013. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali, ni kuwa na Vyuo Vikuu vya kutosha, ili kuwawezesha

vijana wetu wenye sifa za kitaaluma kujiunga na Taasisi za Elimu ya Juu. Katika jukumu la utoaji wa elimu, Serikali, inashirikiana na Sekta binafsi ambapo hadi sasa kuna Vyuo Vikuu vya Umma 11 na Vyuo Vikuu visivyo vya Serikali 34. Kutokana na ufinyu wa Bajeti, si rahisi sana kwa Serikali, kuwa na Chuo Kikuu kila Kanda au kila Mkoa.

Hata hivyo, katika Jiji la Tanga, kuna tawi la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, pamoja na Chuo Kikuu cha Eckenford, ambacho kimeanza kutoa programu za Shahada ya Kwanza.

Serikali, itaendelea kushirikiana na kuwahimiza Wadau kuanzisha Vyuo Vikuu sehemu mbalimbali za nchi, ili kufanikisha azma ya Taifa ya kuwa na Wataalamu wa kutosha.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Chuo cha Eckenford ni Chuo cha Mtu Binafsi na kina changamoto nyingi sana. Majengo hayatoshi, hakuna *lecture rooms,* hakuna Maktaba na huu ni mwaka wake wa pili tu, lakini kumeshakuwa na migomo karibu mitatu ambayo wameisuluhisha, lakini huu wa nne (4) umeshindikana kiasi cha kwamba, Chuo kimefungwa kwa mwezi mmoja.

Je, Serikali, haioni sasa ni wakati muafaka kuingiza mkono wake katika Chuo hicho, ili kuweza kwanza kukipa nguvu na kiweze kuendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni pongezi. Niipongeze Serikali, kwa kuona na kuteuwa Shule ya *Old Tanga* na Macechu, ili kuweza kuzipandisha hadhi na kuwa *"A – Level."* Lakini niombe mchakato huo ufanyike haraka, ili kuweza kuchukua watoto kwa ajili, ya Kidato cha V na VI. Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro iliyopo Eckenford, Chuo hiki kama alivyosema ni chuo binafsi. Mimi nikiri tu kwamba, Mheshimiwa Waziri wangu yupo hapa, lakini mimi binafsi bado sijapata tatizo kwamba, Eckenford kuna tatizo na sina taarifa kamili juu ya migogoro inayoendelea pale. Lakini Mheshimiwa Mbunge, kama anazo taarifa vizuri, basi tuwasiliane tuweze kufuatilia namna ya kutatua migogoro katika chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la nyongeza ni kupongeza Serikali, kwa namna tulivyoweza kuanzisha *"A – Level"* katika Jiji la Tanga. Na mimi nimuahidi kwamba, zile shule 2 tutazifanyia

kazi na zikikamilisha vigezo, tutazisajili ili kuwa na *"A – Level"* katika Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa kuipongeza Serikali. Ni Wabunge wachache sana wanaosimama hapa kupongeza juhudi za Serikali, hasa kutoka upande wa Upinzani. Ninakupongeza sana na ahsante sana.

MHE. DUSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa, Chuo cha Elimu ya Biashara, kimeonesha nia ya kufungua Tawi katika Jiji la Tanga, lakini tatizo ni upatikanaji wa majengo. Waziri, atakubaliana nasi kuona uwezekano wa kuzungumza na Waziri wa Ardhi, ili wenzetu wa *National Housing,* waweze kukipa kipaumbele kutupatia majengo?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kitandula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za vyuo mbalimbali kufungua matawi katika nchi yetu, tunazipa baraka na kuzihamasisha sana. Chuo Kikuu Huria Tanzania *(OUT),* kimefanya hivyo katika maeneo mbalimbali karibu Mikoa yote Tanzania na wakati wote tume-*support* kama Serikali. Tutaki-*support* pia, Chuo cha Biashara, pale ambapo kitahitaji kufungua matawi sehemu nyingine.

Lakini ni muhimu sasa wao wenyewe waanze taratibu za awali za kuwasiliana na wale wenye

majengo na hasa katika Halmashauri husika, ili waweze kukubaliwa kutumia majengo hayo. Patakapokuwa na tatizo lolote Wizara ya Elimu, itakuwa tayari kuweza kuwasaidia kuweza kufanikisha hilo. *(Makofi)*

Na. 177

Kiwango cha Umeme na Dira ya Taifa ya Kujenga Uchumi

MHE. DAVID Z. KAFULILA aliuliza:-

Msingi mkubwa wa Dira ya Taifa ya kujenga uchumi wa kati ni umeme:-

(a) Je, kiwango gani cha umeme kinatakiwa kufikia dira hiyo?

(b) Je, tangu tuweke dira hiyo, tumeongeza kiasi gani cha nishati ya umeme, ikilinganishwa na tulichopaswa kuzalisha?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha Watanzania kuwa na maisha bora siku zijazo, Serikali ilianza

kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo *(Vision – 2025)* mwaka 2000.

Pamoja na mambo mengine, Dira hiyo inalenga kuamsha na kuelekeza juhudi za Watanzania katika kutumia rasilimali zao, kujenga uchumi imara unaohimili ushindani na kuboresha maisha yao, ifikapo mwaka 2025. Aidha, ili kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 Serikali, inatekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016). Moja ya vipaumbele katika Mpango huo ni kuhamasisha uwekezaji katika miundombinu ya nishati, ili kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, kiasi cha *MW 4,117* kitahitajika. Aidha, mpango wa muda mfupi ni kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka *MW 1,375.74* za sasa mpaka *MW 2,500* ifikapo mwaka 2015. Ongezeko hilo litahusisha mchango wa nishati jadidifu kama vile jua, upepo na jotoardhi *(Geothermal)* kwenye uwiano wa uzalishaji *(Generation mix).*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo inafikiwa, mwaka 2009, Serikali, kupitia *TANESCO,* iliandaa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme *(Power System Master Plan, 2009 – 2035).* Tangu kuanza kwa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo Mwaka 2000, uwezo wa uzalishaji umeme uliongezeka kwa kiasi

cha *MW 575.74* ukilinganisha na *MW 800* zilizokuwepo mwaka 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika, Serikali, inalenga kuimarisha vyanzo vingine vya kufua umeme kama vile, makaa ya mawe, gesi asilia, jotoardhi, upepo, jua, badala ya kutegemea umeme unaozalishwa kwa nguvu ya maji tu.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni Malagarasi, ndani ya Jimbo la Kigoma Kusini, Mkoa wa Kigoma. Tayari mchakato wa kukamilisha taratibu za awali za *Igamba III* zimekwishakamilika na eneo lile lina uwezo wa kuzalisha *Mw* takribani 43.

Je, Serikali, katika mipango yake hiyo ndani ya mwaka huu, imefikia wapi katika jambo hili, hasa ukizingatia kwamba, hata Mifuko ya Hifadhi, ipo tayari kuwekeza pale kwa ajili, ya kuhakikisha kwamba, Mradi ule unakamilika? Hiyo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili. Moja ya tatizo kubwa sana la ukosefu wa umeme Tanzania, ni kiasi kikubwa cha rushwa na ufisadi katika sekta ya umeme, ambayo imesababisha, tangu mwaka 1994 mpaka sasa, tunaendesha miradi ya dharura kwa gharama kubwa sana, ambazo kimsingi zinanyonya uchumi.

Ningependa Serikali, itoe taarifa ni kiasi gani cha fedha ambazo tumezitumia kwa miradi ya dharura, tangu mwaka 1994 mpaka sasa. Lakini wakati huohuo kama Kiti chako kitaniruhusu, nitoe ushahidi wa kwa kiasi gani Serikali imehusika, kushindwa kesi ya *DOWANS* kwa makusudi ya kuhujumu nchi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Kafulila, mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Mradi wa Malagarasi. Mazungumzo mbalimbali yanaendelea, Mradi huu sio kwamba, umeachwa. Ili uipate vizuri na itakuja kwa maelezo mazuri, wakati tutakapokuwa tunawasilisha Bajeti yetu tarehe 24 na 25 Julai, 2012 unaweza ukaisikia tutakavyokuwa tumeielezea. *(Makofi)*

Lakini, kwa leo tu niseme kwamba, sisi kama Serikali, Mradi huu tunautambua na ziko hatua mbalimbali za mazungumzo zinaendelea, hata *TANESCO* walikuwa wanazungumza na *NSSF;* tunaendelea kuona namna gani tunaweza tukafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili la kwamba, Sekta ya Umeme imekumbwa na mazingira ya rushwa kupitia miradi ya dharura na nini. Mimi ninadhani

Mheshimiwa Mbunge hapa, kama ana jambo lingine, anapaswa kufuata utaratibu wa kibunge ili kuweza kuleta hoja yake hiyo. *(Makofi)*

Lakini kwa madhumuni ya sasa niweze kusema katika hatua hizi ambazo zimetupelekea kuzalisha umeme wa dharura tumeweza kuongeza zaidi ya megawatt 575 kiwango hiki si kidogo hata kidogo ni kwango kikubwa sana sasa kama kuna hayo unayoyajua mimi nadhani siyo sehemu ya swali langu la Wizara ya Nishati na Madini.

Na. 178

Kuvipatia Umeme Vijiji vya Jimbo la Kilwa Kusini

MHE. CLARA D. MWATUKA (K.n.y. MHE. SELEMANI S. BUNGARA) aliuliza:-

Serikali imekuwa ikifanya juhudi kubwa ili umeme uwafikie wananchi hadi vijijini na kurahisisha maendeleo ya wananchi.

(a) Je, ni lini wananchi wa Somanga, Njianne na Nanguruku ambao tayari wamekamilisha taratibu zote za kupatiwa umeme, watapatiwa kama walivyoahidiwa?

(b) Je, Shirika la umeme lina mpango gani wa kuwapatia umeme wananchi wa vijiji vya Tingi, Mtandago, Miteja, Matandu, Mpara na Mkwanyule ambavyo vimepitiwa na nyaya za umeme ili kuongeza idadi ya wateja?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sulemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, tathimini iliyofanywa na Shirika la Umeme *TANESCO* inaonesha kuwa gharama za upelekaji wa umeme katika vijiji vya Somanga, Njia nne, Nangurukuru hadi vijiji vya Tingi, Mtandago, Mitaja, Matandu, Mpara na Mkwanyule ni takribani shilingi milioni 794.5. Mradi huu utatekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 kupitia wakala wa Nishati Vijijini *(REA).*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa Fedha 2012/2013 Serikali, kupitia wakala wa Nishati Vijijini imepanga kupeleka ueme katika vijiji vya Tingi, Mtandago, Miteja, Matandu, Mpara na Mkwanyule.

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa vijiji hivyo vilivyotajwa hapa kwa suala hili la umeme linafanana na vijiji vya Mumbulu Nakanga na Namkwela vilivyopo wilayani Masasi vipo katikati ambapo kuna eneo fupi tu kama kilomita 20 nyaya za umeme zilishawekwa tangu 2010 zikakamilika 2011 mwanzoni lakini hata leo umeme huo bado

haujapatikana, nini kinachelewesha kupatikana kwa umeme huu.

Swali la pili kwa kuwa kila mwaka unapokaribia Uchaguzi Mkuu Serikali huwa inatoa miradi mizuri mingi vijijini. Sasa ukipita Uchaguzi tu miradi inasimama haiendelei, sasa je, je, ile inakuwa ni kwa ajili ya kampeni tu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijiji vya Nanganga Nakwera ambavyo tayari vilikuwa na nyaya na kwamba umeme hadi leo bado katika Bajeti yetu tunataka kuhakikisha Kusini hakuna tatizo la umeme kwa maana ya ile *line* hata iliyokuwa imechakaa tumetoa fedha zaidi ya bilioni tano na sasa hivi *TANESCO* wanaendelea na hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Lakini ninaamini kabisa kwamba kwa sehemu ambazo zina nyaya sisi kwetu si tatizo, tatizo ilikuwa ni kurekebisha kile chanzo cha umeme wa kupeleka kule ambapo hatua hii iko pamoja kwenye *package* hii ya fedha tulizotoa karibu bilioni tano kwa ajili ya kurekebisha *line* ya kule Kusini.

Sasa hili lingine la ukikaribia Uchaguzi Mkuu kunakuwepo na miradi ambayo hujaitaja ni miradi gani napata shida kusema ni yepi. Maana ungekuwa umeitaja ningeweza kusema hii ilitokana na sababu zipi na hatua za utekelezaji zikoje. Lakini tutambue kwamba Serikali ikiahidi wakati wa uchaguzi utekelezaji wake utaujua baada ya miaka mitano. Kwa sababu

utekelezaji wa Ilani inachukua miaka mitano toka Serikali ilipochaguliwa mpaka inapomaliza muda wake. Kwa hiyo, kwa miradi ambayo iliahidiwa na Serikali wakati wa uchaguzi ikiwemo ya kwenye Ilani ikiwepo ni ahadi za wagombea mbalimbali na hasa wa CCM na hata Wabunge wote itatekelezwa tu vizuri kwa sababu ipo kwenye Ilani na Mbunge yeyote wa CCM hawezi kuahidi mradi ambao hauko kwenye Ilani ya Uchaguzi.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi nilikuwa naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kupitia gesi asilia, mafuta mazito pamoja na maji kwenye *grid* ya Taifa sasa tuna megawatt ngapi ahsante.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa gesi peke yake unatupa gesi hii tunayotoa ya Songosongo unatupatia zaidi ya karibu megawatt 428 hivi gesi peke yake. Kwa hiyo ukija mafuta mazito tunapata karibu megawatt kama 680 tunapata kutoka kwenye vyanzo hivi vingine, ukiondoa vyanzo vya maji peke yake.

Na. 179

Kuhusu Kuiwezesha Benki ya Wanawake Hisa za Kutosha na Kufungua Matawi Zanzibar

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA aliuliza:-

Serikali ilifungua Benki ya wanawake ambayo mikopo yake inatolewa kwa masharti nafuu ili kuwawezesha wajasiriamali wadogo wadogo wanawake nchini.

(a) Je, ni lini Serikali itaiwezesha Benki ya Wanawake hisa za kutosha na kufungua Matawi Tanzania, Zanzibar na vijiji ambako Benki hiyo haina Matawi?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa semina endelevu kwa wanawake vijijini na Mikoa juu ya fedha zinazotolewa na Taasisi mbalimbali kwenye Benki hiyo na kuwahamasisha kufungua akaunti na kuendeleza biashara ndogondogo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake ilianzishwa mwaka 2009 kutokana na ombi maalum lililotolewa na Wizara ya Wanawake Jinsi na Watoto pamoja na wanawake wajasiliamali ambayo ililiridhiwa na Rais Mstaafu Benjamini Mkapa na kuanzisha na kwa Mtaji wa Bilioni mbili ulitolewa na Serikali. Aidha, Serikali iliahidi kuendelea kutoa kiasi cha Shilingi bilioni mbili kila

mwaka kwa kipindi cha miaka mitano hadi mtaji wa benki hiyo utakapofikia shilingi bilioni 10.

Serikali imetekeleza ahadi yake ya kuongeza mtaji wa shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa kipindi cha 2010/2011 na 2011/2012 na hata kipindi hiki cha 2012/2013 imeongeza bilioni moja point moja lakini lengo ni kuhakikisha kuwa inaendelea kuongeza mtaji huo mpaka ufikie bilioni kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuiongezea mtaji Benki hii hadi hapo mtaji wake utakapoimarika na kuiwezesha kufungua matawi zaidi Tanzania , Zanzibar na Vijijini ambako Benki hiyo haina Matawi. Aidha, kwa sasa Benki ya Wanawake ipo katika maandalizi ya mwisho ya kufungua vituo vya kutolea mikopo *(lending Centres)* katika Mikoa ya Dodoma, Mwanza, Singida, Morogoro na Zanzibar. Vituo hivi vitawawezesha Wanawake wengi zaidi katika maeneo hayo kupata mikopo ya masharti nafuu iliyotolewa na Benki ya Wanawake.

Vituo hivi vinatarajiwa kufunguliwa katika robo ya mwaka wa fedha 2012/2013 baada ya kupata kibali kutoka Benki Kuu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na taasisi binafsi na za kijamii imekua ikiendesha semina na makongamano mbalimbali kupitia ngazi mbalimbali za uongozi Mikoani, Wilayani na vijiji kwa lengo la kuwaelimisha wananchi hasa wanawake kupitia vikundi vyao juu ya umuhimu wa kutumia fedha za mikopo zinazotolewa na taasisi

mbalimbali za fedha hapa nchini ili kuharakisha maendeleo yao. Aidha, Serikali kupitia Benki ya Wanawake tayari imetoa mafunzo na mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali wadogo wadogo vipatavyo 15 vyenye wanachama wapatao 6,020 katika Mkoa wa Dar es Salaam. Zoezi hili litaendelea kufuatia kufunguliwa kwa vituo zaidi vya kutoa mikopo *(lending centres)* na matawi mengine katika maeneo husika, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kulitolewa mabilioni ya Rais Kikwete na Rais Mstaafu wa Zanzibar Amani Abeid Karume, Mabilioni hayakuwafikia walengwa wakiwemo hawa wanawake wajasiliamali wadogo wadogo na yakaishia mikononi mwa watu wajanja.

Je, Waziri utanihakikishia mabilioni haya yalikwenda wapi yasiingizwe kwenye benki ya wanawake ili wengi wakanufaika na benki hii?

Kwa kuwa wanawake wa vijiji ambao wako pembezoni, wamekuwa wakichukua mikopo ya riba kubwa na kudhalilishwa na kuchukuliwa vitu vyao vya ndani, mtahakikishaje wanawake hawa wanapata mafunzo ya ujasiriamali kwa sababu kila siku tunasikia mtakwenda vijijini lakini hamwendi? Naomba mnipe majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu na mabilioni ya Rais

wa Zanzibar, mabilioni yale yaliingizwa katika mabenki mbalimbali hapa nchini ambapo taratibu za kutoa mkopo zilikuwa zikiendelea.

Wazo la kuwa fedha hii iingizwe kwenye benki ya wanawake ni wazo zuri linaweza likajadilika, tutaangalia uwezekano wa mifuko mingine itakayojitokeza kwa sababu sasa tuna chombo tayari kwa ajili ya benki ya wanawake kitakachoweza kutumika kwa ajili hiyo.

Kuhusiana na mafunzo kama nilivyojibu jibu langu la msingi mafunzo yanaendelea kutolewa siyo tu benki ya wanawake lakini taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya mikopo midogo midogo, na hili ni suala endelevu na sasa ningependa kutoa rai kwa Mheshimiwa Mbunge Maryam pamoja na Wabunge wengine kuwa tutumie fursa hizo zilizopo katika soko la mafunzo yanayotokea kuwahamasisha akinamama na vijana kuhudhuria mafunzo hayo ili waweze kujifunza vizuri jinsi gani ya kutumia mikopo na kujiendeleza katika miradi yao.

Kuhusiana na unyanyasaji unatolewa kwa wale ambao wanashindwa kulipa mikopo yao nilishalitolea hili jibu mapema lakini ningependa kurudia kuwa ni jambo ambalo linasikitisha kuwa mtu anakopa halafu anaposhindwa kulipa ananyanyaswa, lakini hili ni jambo ambalo tulikuwa tunataka kumhakikishia Mheshimiwa Msabaha kuwa tunajaribu kuongea na vyombo husika kuwa watumie njia ya kibinadamu katika kudai. Vilevile wazingatie mazingira hasa yaliyomsababishia mwanamke huyo au mkopaji huyo

kushindwa kulipa mkopo wake ili tuangalie kama kuna njia wanazoweza kumsaidia. Aidha kusogeza mbele au kumpa mafunzo zaidi jinsi gani ya kuboresha mkopo wake.

Lakini vilevile ikumbukwe kuwa kuna wengine ambao hawatumii ile mikopo kwa sababu walizokopea na ndiyo maana wanashindwa kulipa. Sasa pengine ndiyo inaletea kuwa wanadaiwa kwa nguvu zaidi lakini yote haya tutayazingatia na kuyafanyia kazi.

MWENYEKITI: Ahsante, haya Mheshimiwa Dkt. Mary Nangu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nilitaka tu kuongezea majibu ya ziada kuhusu mabilioni ya J. K. Hayajapotea bure kwenye mikono ya watu. Kwanza madhumuni ya fedha zile ni kuimarisha ujasiliamali na kuongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utafiti wa awali fedha zile zimerudishwa kwa aslimia tatu, kwa hiyo si kweli kwamba mabilioni yale yamepotelea mikononi mwa watu na bado yanaendelea kuongeza ajira na kuimarisha ujasiliamali na utafiti utaendelea. Ningeomba Watanzania wanapopewa nguvu wazitumie wanapopewa fursa wazitumie wakumbuke kurudisha fedha hizo ili ziweze kuwasaidia wengine. *(Makofi)*

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, moja ya matatizo ya mabenki yaliyopo Tanzania sasa hivi ni ukwasi mkubwa walionao kutokana na *treasury bill* kuongezwa thamani na mabenki mengi na hasa mifuko ya hifadhi za jamii ambao ndiyo wanaokopesha mabenki wananunua hizo *TB* na maana yake kwamba benki zote zimekosa fedha za kukopesha watu.

Je, haioni Serikali kwa utaratibu wa kuongeza riba kwenye *treasury bill* zinafanya mifuko ya hifadhi ya jamii kutokuzikopesha benki na matokeo yake sasa hivi ukienda kwenye mabenki ukitaka mikopo huwezi kupata fedha kwa sababu hawana fedha kutokana na mabenki mengi yanawekeza zaidi kwenye zile *TB.* Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuanzisha ujasiriamali na watu wengine waweze kupata mikopo kwa urahisi?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge kwanza kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa swali lake nzuri. Serikali kweli inanunua *treasury bill* kwa sababu mbalimbali, kuna sababu tatu ambazo kama Serikali kwa kutumia benki yetu ya *Central Bank* tunaweza tukanunua aidha kwa ajili ya *liquidity management* au kwa ajili ya *financing gap* au kwa ajili ya ku-*roll over liability* za Serikali.

Lakini tunapofanya sasa hivi kununua fedha kwa kutumia *treasury bill* katika soko la fedha la sasa hivi ushahidi uliopo soko la Tanzania sasa hivi lina *access liquidity.* Kwa mfano mpaka jana kulikuwa na *excess*

subscription that is over subscription by 81 billion kwa maana *liguidity* ya soko la fedha katika Tanzania ni kubwa kwa hivyo umma una fedha nyingi ambazo ziko mkononi. Ndiyo maana *treasury bill rate yield* ilipungua kwa *almost* asilimia 0.5 ukilinganisha na safari iliyopita.

Kwa hiyo, inapopungua *interest rate* maana yake kuna *access liquidity* ya *over subscription* lililojitokeza kwenye kopo. Kwa hiyo hoja ya kisayansi inaweza kuwa kisahihi lakini mpaka sasa hivi soko liko sawasawa.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa majibu ya kitaalam Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tunahamia swali Namba 180 Mheshimiwa Mahamoud Hassan Mgimwa.

Na. 180

Kufungua Huduma za Benki Mbalimbali Mafinga

MHE. MAHMOUD HASSAN MGIMWA aliuliza:-

Wakati wa kampeni za Uchaguzi wa mwaka 2010 Serikali iliahidi kutatua kero ya huduma za kibenki kwa kuongeza tawi jingine la Benki zaidi ya *NMB.*

Je, ni sababu zipi zinazosababisha benki nyingine kama *CRDB, NBC, Barclays* zisifungue matawi yake Mjini Mafinga na kusababisha wananchi kufuata huduma hiyo Iringa Mjini na Njombe?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa wananchi wote wa Tanzania kupata huduma za kibenki karibu na maeneo yao wanayoishi.

Napenda ifahamike kuwa kufuatia mabadiliko ya mfumo wa kifedha nchini uliotekelezwa kuanzia mwaka 1991, Serikali iliazimia kutokujihusisha moja kwa moja na masuala ya biashara za mabenki.

Serikali inajitahidi kuweka mikakati ya kuboresha mazingira ili kuiwezesha sekta binafsi kuanzisha mabenki na kutoa huduma bora za kibenki kwa wananchi na katika hali iliyo huru bila kuingiliwa katika utendaji na kufanya maamuzi ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inatambua kuwa mabenki hupeleka huduma hizo za kibenki kwa wananchi wa maeneo husika baada ya kufanya upembuzi yakinifu.

Katika upembuzi huo, lazima pande zote mbili yaani upande wa mabenki na wateja (wananchi), ziweze kufaidika na huduma ya kibenki. Hivyo Serikali haiingilii maamuzi ya wapi benki zitafungua matawi yake na wakati gani.

Lakini baada ya kusema hivyo nafahamu kuwa Mufindi kuna *Community Bank* ambayo tayari imekuwa ikifanya kazi kwa muda mrefu na kwa sasa hivi ninavyozungumza benki ya *CRDB* imefungua tawi ambalo bado halijalizinduliwa rasmi lakini inaendesha shughuli za *mobile* katika eneo hilo.

Kwa hiyo sasa hivi kazi ambayo nataka kumuahidi Mheshimiwa Mbunge Mgimwa ni kuwa nafuatilia kwa karibu *CRDB* watufahamishe ni lini haswa watafungua rasmi tawi lao ambalo naamini lilipaswa kuwa limefunguliwa tantu mwaka jana ili niweze kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge ili shughuli ziende. Naamini itawezesha kuongeza nguvu ya huduma za kibenki katika eneo la Mufindi.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri tawi la *CRDB* ambalo limejengwa sasa hivi pale Mufindi waliahidi kufungua mwezi wa nane mwaka jana. Ujenzi umekamilika lakini mpaka leo hii takribani mwaka mzime umeshapita.

Sasa nataka nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri atuhakikishie lini kwa sababu watu bado wanapata shida pale, ile *mobile* inafanya kazi mara tatu kwa wiki. Kwa hiyo, biashara imekuwa ya mashaka. Ni lini watatufungulia? Na sababu zipi zinasababisha lile tawi lizifunguliwe mpaka sasa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa

Fedha, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimwia Mahmoud H. Mgimwa, kama ifuatavyo:

Kama nilivyoahidi mara ya kwanza ni kwamba najitahidi sasa hivi kuwasiliana na *CRDB* watufahamishe kwa uhakika ni lini watafungua tawi lao ambalo wamelijenga Mufindi na nitapata vilevile sababu kwa nini wamechelewa na ninataka kumhakikishia Mheshimiwa *personally* kuwa nitampatia taarifa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapenda kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Wakati Benki ya *NBC* inagawanywa na kupata *NMB* kusudi kubwa la *NMB* ilikuwa ni kupeleka huduma za kibenki vijijini kwa kufanya *micro finance,* lakini mpaka sasa tabia inayojinyesha ni kwamba badala ya kuapeleka huduma hizo *NMB* sasa inafanya biashara katika miji na wala siyo kufanya *micro finance.*

Ninapenda kujua ni kwa nini Serikali inashindwa kuwasukuma *NMB* wafanye hizo *micro finance* na badala yake wanawa-*encourage* wafanye *commercial bank* na kusababisha matatizo makubwa vijijini maana hakuna huduma za kibenki na ukiona sasa shughuli za *micro finance* zinafanywa na mashirika

mengine kama M-pesa na kadhalika badala ya *NMB.* Nataka kujua ni kwa nini tofauti imetokea?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mkono kwa swali hilo.

Labda niseme tu kiukweli si kweli kwamba Serikali inasukuma *NMB* ifanye shughuli nyingine, lakini *NMB* pamoja na kwamba inaitwa *National Microfinance Bank* lakini ina mamlaka ya kufanya shughuli zote katika shughuli za Benki. Benki inapokuwa imepata licence ina mamlaka ya kufanya shughuli zote ingawaje *NMB* ina shughuli kubwa ya kusaidia *micro activities.*

Lakini niseme kwamba tunaporuhusu *institutions* nyingi kufanya shughuli za fedha ndiyo tunapoelekea kurahisisha utoaji wa huduma na tunaweka ushindani ambao utafanya gharama ya kutumia pesa na kukopa iwe chini kwa sababu ya ushindani wa vyombo vya fedha vinavyofanya.

Kwa hiyo, *NMB* tutaendelea kuiunga mkono kama tunavyozisaidia Benki nyingine na wote pamoja na Mbunge tunaomba tusikate tamaa ili tuone kwamba *NMB* inavyofanya inafanya vizuri na tu-*encourage* na vyombo vingine vya fedha kama M-pesa na vingine viendelee kuleta ushindani wa kifedha ili huduma za fedha ziweze kuboreka nchini na hivyo wananchi wanufaike.

MHE. SABREEN HAMZA SUNGURA – KAIMU KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Ninapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, si mikoa yote mitano ya Zanzibar yenye huduma na matawi ya benki ambazo zimeainishwa katika swali. Ninapenda kujua ni hatua gani na ni lini kwa Zanzibar katika mikoa yote kutakuwa na huduma za kibenki na matawi ya benki ili kupunguza safari ama umbali wa watu wanaofuata huduma hizi katika mikoa mingine kutoka katika mikoa yao?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana muuliza swali.

Kazi kubwa ya Serikali ni kuweka mazingira ambayo biashara na vyombo vya fedha vitafanya kazi ile vizuri. Kazi yetu kubwa ni kuweka mazingira ambayo tumeshaweka mazingira mazuri na tunahamasisha vyombo vya fedha vifungue matawi yao au benki zao kila mahali kulingana na mujibu wa taratibu za biashara.

Kwa hiyo, vyombo vya fedha huwa vinafanya tathmini yaani *technical feasibility study* kuonyesha kwamba namna gani wakifungua biashara eneo fulani wao wenyewe biashara ile itajilipa, na kwa hali hiyo ni vizuri basi sisi Wabunge pamoja na wananchi wengine tuwahamasishe wananchi wetu ili biashara zile wanazozifanya na maeneo yetu wanapokuja

kufanya tathmini waone tunakidhi kwamba benki hizi zinaweza zikafungua matawi na sisi tukanufaika.

Lakini kazi yetu kubwa ya Serikali ni kuweka mazingira ambayo vyombo vya fedha vitaruhusiwa na vitaona kuna usalama wa kufanya kazi. Mazingira hayo Tanzania nzima yapo na yanapendeza. Kazi yetu kubwa Wabunge ni ku-*encourage* na kuwasaidia watu wote waelewe na vyombo vile vione kwamba vinaweza vikafungua matawi hayo hapa tulipo na kule tunakofikiri sisi kunawezekanika.

MWENYEKITI: Ahsante, naomba tutoe majibu mafupi na sasa ni Wizara ya Kilimo swali namba 181.

Na. 181

Mafanikio na Changamoto za Kilimo Kwanza

MHE. SUSAN A. J. LYIMO aliuliza:-

Tanzania ina maeneo makubwa kwa ajiil ya kilimo na wataalamu husisitiza kuwa kilimo ndicho kitakachokuza uchumi wetu kwa haraka:-

Je, kwa kiwango gani Serikali inatekeleza Kilimo Kwanza na nini mafanikio na changamoto zake?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa uwekezaji katika kilimo ni njia ya kupunguza umaskini, kuwa na usalama wa chakula na kuharakisha maendeleo ya uchumi wetu. Kilimo Kwanza ni azma maalum ya kitaifa inayowahusisha wadau mbalimbali wa kilimo nchini katika kuongeza kasi ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini kwa maana ya kilimo cha kijani. Utekelezaji wa Kilimo Kwanza unazingatia nguzo kumi ambapo kila nguzo imeainisha mhusika mkuu na wahusika wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wizara za Sekta ya Kilimo azma ya Kilimo Kwanza inatekelezwa kupitia programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme (ASDP).* Aidha, mpango wa uwekezaji wa kilimo na Kusini mwa Tanzania *(Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)* unaohusisha ushiriki wa sekta binafsi na wakulima wadogo ni njia mojawapo ya kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya Kilimo Kwanza ni pamoja na kuongezeka kwa eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 264,388 mwaka 2006/2007 hadi kufikia hekta 345,690 mwaka 2010/2011. Kuongezeka kwa matumizi ya pembejeo za kilimo kutokana na mpango wa ruzuku, mbolea na kutoka tani 73,000 mwaka 2007/2008 hadi tani 200,000 mwaka 2011/2012, mbegu bora kutoka tani 11,056 mwaka 2007/2008 hadi tani 200,000 mwaka 2011/2012, kuongezeka kwa maafisa ugani kutoka 3,000 mwaka

2006/2007 hadi kufikia 7,974 mwaka 2012, ujenzi wa vituo 131 vya raslimali vya kata *(Ward Resources Centres)* na kuongezeka kwa matumizi ya zana bora za kilimo hadi kufikia matrekta makubwa 8,000 na madogo 4,500 mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, zipo changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na tija ndogo, ukosefu wa masoko ya uhakika, ukame/mabadiliko ya tabianchi, miundombinu duni ya barabara, reli, masoko na upatikanaji wa nishati na umeme wa uhakika vijijini, upatikanaji wa ardhi iliyopimwa na kuwekewa miundombinu muhimu kama vile maji, umeme na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lengo la Serikali kushughulikia changamoto hizo hatua kwa hatua kwa kupitia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano na Mpango wa Uwekezaji katika Usalama wa Chakula Tanzania *(Tanzania Agricultural Food Security Investment Plan (TAFSIP*) pamoja na kuimarisha usimamizi na uwajibikaji kwa maafisa ugani na wadau wengine sisi wote wa Sekta ya Kilimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo kwangu hayajaniridhisha naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, katika kipindi cha miaka mitano Serikali imeweza kuongeza hekta 81,000 tu kati ya hekta milioni 29 za umwagiliaji, hii ikiwa na maana kwamba kwa mwaka tumeweza kuongeza

ekari 16,200 ikiwa na maana kwamba kwa ekari zilizobaki tutaweza kuzimaliza kwa miaka 1,771.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Waziri atuambie kwa kasi hii anadhani tutaweza kweli kuleta mabadiliko ya kilimo?

Lakini la pili, kwa kuwa tumekuwa na tatizo kubwa sana la vijana wetu kukimbilia mijini na vijana wetu kutokuwa na kazi na kwa kuwa, imeonekana wazi kwamba kilimo peke yake ndiyo kitaweza kuimarisha uchumi wa nchi hii. Je, Serikali ina mikakati gani wa kuhakikisha kwamba inawasaidia vijana wetu ili waweze kwenda kufanya kazi katika kilimo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Susan A.J. Lyimo maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba nimtake radhi tu Dada yangu kwa sababu hizo hesabu alizopiga basi siyo sawa kwa sababu ni hesabu na mimi mwenyewe pia fani yangu ni mambo hayo hayo ya hesabu. Kwa hiyo, hesabu ni *subjective* wewe umechukua hesabu za mwaka 1,771 bila kuzingatia vigezo vingine vyote na changamoto nyingine zote pamoja na changamoto za uwekezaji katika sekta ndogo ya umwagiliaji ndani ya Sekta kuu ya Kilimo.

Lakini tunachosema ni kwamba yapo mafanikio makubwa sana ambayo yamepatikana kwenye Sekta ya Kilimo kutokana na usimamizi wa Serikali hii na

tunasema sasa hivi kwa huu mpango wa Kilimo Kwanza, *focus* ya Kilimo Kwanza ni ushiriki wa sisi wote kwa maana ya Serikali na Taasisi zake na wananchi na Halmashauri na kadhalika. Ili uwajibikaji katika kuongeza ufanisi ndani ya Sekta ya Kilimo iwe ni changamoto na wajibu wa sisi wote. Sasa umebana kwenye umwagiliaji lakini kuna eneo lingine ambalo linahusika na Sekta ya Kilimo ambayo ni *mechanisation* kuongeza ma-*power tiller* na pembejeo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo tu katika miaka mitano zimetoka kwenye tani 70,000 mpaka sasa hivi tunazungumzia tani 200,000 na matokeo yake ni kwamba tuna *food security* kwa upande wa mahindi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kwa ujumla kwamba tunaitazama sekta ya Kilimo katika upana wake na kwa sasa hivi tuna *focus* kwenye mikakati ya muda mfupi ambayo ni kuboresha upatikanaji wa pembejeo na pia kuboresha matumizi ya umwagiliaji maji ili kwa ujumla wake kuongeza uzalishaji wenye tija ndani ya Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la kwamba vijana wetu wanakimbilia mijini ni tatizo ambalo linaeleweka na ndiyo maana nikasema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba yapo mambo ya msingi kabisa ambayo yanaelekezwa kwenye Sekta ya Kilimo *especially* kwa maana ya *rural economy* kama *rural electrification,* nishati vijijini, barabara vijijini na kadhalika ambazo kwa pamoja zitaongeza tija kwa

uzalishaji wa kilimo vijijini. Lakini kubwa ni kwamba tunahamasisha vijana kuingia kwenye vikundi vya uzalishaji na vikundi hivyo vya uzalishaji Halmashauri na Serikali Kuu imetengeneza mikakati ili viweze kukopesheka ikiwa ni pamoja na kupunguza masharti ya ukopeshaji wa matrekta kwa vikundi ili waweze kupata motisha ya kuzalisha kwa kutumia zana bora za kilimo na pembejeo hii inayotolewa kwa ruzuku kwa 50%

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Kwa kuwa muda hauturuhusu basi tunahamia swali namba 182, linaulizwa na Mheshimiwa Vita Kawawa lakini kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Alhaji Mtutura.

Na. 182

Hitaji la Matrekta kwa ajili ya Kilimo Kwanza – Ruvuma

MHE. MTUTURA A. MTUTURA (K.ny. MHE. VITA RASHID KAWAWA) aliuliza:-

Mkoa wa Ruvuma ni moja ya mikoa inayozalisha chakula kwa wingi na hakuna hata wakulima au vijiji vinavyomiliki matrekta.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha matrekta yanasambazwa katika vijiji vya mkoa huo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa kuwa Mkoa wa Ruvuma ni moja ya mikoa mitano inayozalisha chakula kwa wingi hasa zao la Mahindi. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa Mkoa wa Ruvuma una jumla ya matrekta makubwa 77 yaliyo katika Wilaya ya Songea/Manispaa, Tunduru 20, Namtumbo 11 na Mbinga 13. Matrekta hayo yanamilikiwa na watu binafsi, vikundi na mashirika binafsi na katika msimu wa mwaka 2010/2011 yaliweza kulima hekta 16,600 kati ya jumla ya hekta 420,000 zilizolimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha matrekta yanasambazwa katika vijiji mbalimbali, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge na viongozi wa Mkoa wa Ruvuma kushirikiana na Wizara yangu kuwahamasisha wakulima wetu vijijini kuibua miradi ya kununua matrekta kupitia mipango ya kuendeleza kilimo Wilaya (*DADPs*). Serikali imesaidia kuwepo na punguzo la bei kwa matrekta yanayouzwa na *SUMA JKT* la kati ya 15% hadi 36% ili kuwawezesha wakulima wengi kumudu kuyanunua na hivyo matrekta yawepo vijijini kwa ajili ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati mingine iliyopo ni pamoja na kuendelea kuwahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na vyama vya ushirika ili

kuunganisha uwezo wa kifedha kwa ajili ya kununulia matrekta haya kwa fedha taslim kufuatia punguzo kubwa la bei.

Vilevile watumishi wa Umma wanaweza kukopa kupitia dhamana ya waajiri wao. Mkakati huu utasaidia kupeleka matrekta vijijini na pale watumishi hawa wanapostaafu kuendeleza shughuli zao za kilimo kwa ufanisi zaidi.

Pia upo utaratibu wa wakopaji wa matrekta kulipia kidogo kidogo na inapofikia zaidi ya 50% mteja anaweza kuchukua trekta lake na kiasi kilichobaki kulipwa kwa makubaliano kulingana na mkataba watakaokubaliana. *(Makofi)*

Hata hivyo, mazungumzo yanaendelea kuangalia uwezekano wa watakaokubaliana. Hata hivyo, mazungumzo yanaendelea kuangalia uwezekano wa kupunguza malipo hayo ya awali na kuongeza muda wa kurejesha.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa, Mkoa wa Ruvuma kupitia ufadhili wa *SUMA JKT* tumefanikiwa hivi majuzi kuzindua mpango wa kukopesha matrekta zaidi ya 53.

Je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kuelekeza fikra katika kuleta vifaa vya kuvunia kwa kuwa

imekuwa ni changamoto kubwa sana na gharama kubwa sana kwa wakulima katika kuvuna? Kwa mfano, uwezekano wa kuleta *min-combine harvester?*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nitambue hilo alilosema kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu Jumamosi wiki iliyopita amefungua huu mkakati wa kukopesha matrekta na kwa uhamasishaji tu naomba nitambue na kuwapongeza wakulima wa Mkoa wa Ruvuma, kwa sababu katika hizi siku chache tu imebainika kwamba wakulima 80 wana vikundi vyao wameomba kuchukua matrekta hayo.

Hili linatarajia kuongeza sana uzalishaji kwa Mkoa wa Ruvuma kwa sababu mtu anayelima kwa trekta ekari moja anatumia dakika 45 wakati akitumia jembe la mkono anatumia siku saba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kusema kweli ni uhamasishaji ambao mikoa hii mikuu ya kilimo tunawahamasisha sana walime kwa trekta.

Kwa maana hiyo kama anavyosema Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, utakapoongezeka uzalishaji pia lazima Serikali itambue kwamba lazima tuingie katika mikakati ya kuvuna. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba nitambue kwamba ni wazo zuri na ni pendekezo zuri kwamba katika mfumo huo wa inputs kwa maana ya pembejeo pia tuzungumzia kuangalia namna ambayo harvesters ama combined harvesters ama min harvester yote yatakuwa sehemu ya utaratibu wa pembejeo kwa maana ya kuboresha uzalishaji na uvunaji wa mazao.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona, nina swali dogo moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kilimo ni uti wa mgongo na kwa kuwa kilimo pia ni sehemu ya ajira. Je, serikali ina mkakatigani wa kutoa matrekta kwa vikundi vya akina mama na vijana ili walime waweze kujipatia ajira na baadaye waweze kulipa hayo matrekta?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majibu yangu yote mawili ya awali kwamba tumeweka utaratibu ili vikundi vya uzalishaji vitakapobainika viweze kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna ule utaratibu ambapo vikundi vya uzalishaji kwanza, vinaanzia kwenye Kata zao, vinakwenda kwenye Halmashauri vinatambulika, wanaandaa *minutes* na kadhalika ili

kuviwezesha vijulikane, hasa kwa sababu mfumo wa kukopesha ni kwamba, kikiwa kikundi cha akinamama na wazee na kadhalika, utaratibu ni kwamba, ukikopeshwa urudishe ule mkopo. Sasa tulichofanya ni kwamba, kwa vikundi kama hivi vya akinamama tumetengeneza kwa makusudi kabisa kulingana na zile *feasibility studies* watakazoleta, lakini tunatengeneza utaratibu ili masharti kwa ajili ya mikopo yao yawe nafuu zaidi kuliko utaratibu wa wakopeshaji kwa mfumo binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhamasishe Mheshimiwa dada yangu Zainabu Matitu pamoja na viongozi wengine wote wa vikundi vya akinamama kwamba, watumie fursa hii ili Serikali iweze kuwahamasisha akinamama kulima kwa kutumia zana bora za kilimo.

MWENYEKITI: Muda wa maswali umekwisha na nina matangazo yafuatayo:-

Kwanza ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Tuna Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wakiongozwa na Ndugu Patrick Rutabanzibwa, Katibu Mkuu. Tunaomba walipo tuwaone. Karibuni. (*Makofi*)

Pia tuna Bi Maria Bilia, Naibu Katibu Mkuu. Pia tuna *Engineer* Kesogukewele Msita, Mwenyekiti wa Bodi ya *National Housing Corporation,* alipo tumwone. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tuna Mbunge Mstaafu, Mheshimiwa Steven Kahumbi, ambaye ni mgeni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, alipo tumwone. Karibu sana. (*Makofi*)

Tuna wageni 11 wa Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambao ni watoto wake; Kemi Tibaijuka na Kankiza Tibaijuka. Walipo wasimame tuwaone. Karibuni. (*Makofi*)

Tuna Madiwani wanne pamoja na wananchi watatu kutoka Kigamboni wakiongozwa na Mheshimiwa Suleiman Mathew, Diwani wa Kata ya Vijibweni. Walipo tuwaone, karibuni. (*Makofi*)

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Goodluck Ole- Medeye, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambao ni familia yake wakiongozwa na mkewe Bi. Anthonia Lekule. Pale walipo tuwaone. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ambao ni Ndugu Isamil Shah, mtoto wake na Jilesh Babla ambaye anatoka India na anatangaza utalii wa Tanzania nchini India. Karibuni sana, mlipo tuwaone. (*Makofi*)

Tuna wageni 45 kutoka Jimbo la Uzini, Zanzibar wakiongozwa na Mwalimu Mkuu Ndugu Hamad Ali Haji, kutoka Skuli ya Pagani, Zanzibar. Walipo tuwaone. Karibuni. (*Makofi*)

Tuna Wanafunzi 60 na Walimu wao kutoka Shule ya Msingi Buigiri, Dodoma, walipo tuwaone. Karibuni na mjifunze kwa juhudi na maarifa. Pia tuna Wanafunzi 99 kutoka Shule ya Msingi *Santhome* ya Dodoma, walipo tuwaone. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wanakikundi cha *Amadombe Sanaa Group*, kutoka Kata ya Vijibweni wakiongozwa na Ndugu Athuman Ali Ibrahim. Walipo tuwaone. Karibuni. (*Makofi*)

Taarifa za vikao; Mheshimiwa Filipa Geofrey Mturano, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hii kwamba, leo saa 7.00 Mchana watakutana katika Chumba Na. 227 ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala. Inasisitizwa mfike bila kukosa.

Pia Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati, Chumba Na. 219, Jengo la utawala. Mnasisitizwa mfike kwa wakati.

Mheshimiwa Brigedia Mstaafu Hassan Ngwilizi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati, Ukumbi wa Msekwa B. Mnasisitizwa mfike bila kukosa.

Pia Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mwenyekiti wa *Bunge Range Club (BRC)*, anaomba niwatangazie Wanachama wa *Bunge Range Club* kwamba, zoezi la kulenga shabaha litafanyika siku ya Jumapili, tarehe 22 Julai, Makutopora JKT kuanzia saa 4.00 asubuhi. Waheshimiwa Wabunge wenye nia ya kushiriki katika zoezi hili mnaombwa mtie saini na kuthibitisha ushiriki wenu katika zoezi hili kwenye fomu inayozungushwa ndani ya Ukumbi wa Bunge. Naomba wenye nia hiyo wafanye hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yamekwisha.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Mwongozo, Mheshimiwa Machali, atafuatiwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura.

MHE. YAHYA KASIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nipo.

MWENYEKITI: Haya na Mheshimiwa Yahya. Eenh, Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili pengine niweze kuomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Naomba nisiisome ili kuweza kuokoa muda kwa kuwa inaeleweka.

MWENYEKITI: Isome.

MHE. MOSES J. MACHALI: Kanuni ya 68(7) inasema kwamba: “Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa hapohapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati swali Na. 177 lililoulizwa na Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini, wakati akiuliza maswali ya nyongeza amelieleza Bunge lako kwamba, anao ushahidi kwamba, Serikali...

MWENYEKITI: Samahani Mheshimiwa naomba ukae kidogo.

MJUMBE FULANI: Hajamaliza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lukuvi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utaratibu. Kifungu alichokitumia Mheshimiwa Mbunge cha 68(1) kinamtaka Mheshimiwa Mbunge anayetaka kuzungumza jambo hili azungumze wakati Mbunge

mwingine anaongea. Kwa sasa hakukuwa na Mbunge anayeongea.

WABUNGE FULANI: Mmmh!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nikusomee.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa, taarifa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Naomba nisome.

WABUNGE FULANI: Taarifa!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa, taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, naomba umwachie kwanza asome, halafu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Kwanza hakuna taarifa juu ya taarifa!

WABUNGE FULANI: Mmmh!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Na hakuna Mwongozo juu ya Mwongozo.

MWENYEKITI: Eeh, basi kaa chini.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Kwa hiyo, atulie kwanza ili kusudi mwongozo wa awali..

(Hapa Mheshimiwa Mwenyekiti alizima kipaza sauti ili Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa akiongea asisikike)

MWENYEKITI: Naomba niseme kwamba, nitawaacheni wote mjieleze, lakini kubishana siyo vizuri. Naomba tumwachie Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwanza amalize, kila mmoja nitampa nafasi. Mheshimiwa Lukuvi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mbunge yeyote ...

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unamwachiaje azungumze na wakati hoja ya Mheshiwa Machali haijakamilika? Mwongozo haujakamilika, anajuaje? Siyo utaratibu! (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Unapendelea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema amekosea, hii Kanuni haimruhusu..

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizomea)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Naomba nisome Kanuni hii...

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hajamaliza kuzungumza, anapigaje ramli? *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Naomba utulivu, naomba utulivu. Mheshimiwa Kafulila, naomba unisikilize. Unavunja Kanuni kwa kuongea bila idhini ya Kiti, maana yake nini? (*Makofi*)

Halafu wote mnaoongea bila ya utaratibu si vyema, naomba tuzingatie utaratibu wetu na Kanuni zetu. Muacheni Mheshimiwa Waziri aongee...

WABUNGE FULANI: Mmmh!

MWENYEKITI: Msibishe sasa, mbona mnabishana na mimi! Hebu kaeni kimya! Haya Mheshimiwa Waziri Lukuvi, naomba usome Kanuni.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Naomba nisome Kanuni aliyoitumia Mheshimiwa Mbunge ili kuwafahamisha Watanzania ambao hawamo humu ndani ya Bunge. Kifungu cha 68(1) kinasema: “Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno “Kuhusu Utaratibu” ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini, na Spika atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kukumbusha hilo, wewe ndiye ulikuwa unasema, hakukuwa na Mbunge anayesema.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali aliyeomba Mwongozo wangu kwa Kanuni ya 68(7) naomba aendelee. (*Makofi*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kukitendea Kiti chako kwanza haki na kutendea haki Waheshimiwa Wabunge, tunaposimama kwa ajili ya kuomba Mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati swali Na. 177 lilipoulizwa, katika maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa David Kafulila, amelieleza Bunge lako Tukufu kwamba anao ushahidi ambao unaonesha Serikali imehusika kuhakikisha kwamba tunashindwa katika kesi ya *Dowans* na hivyo kupelekea Taifa kuweza kupoteza hizi shilingi bilioni 94 ambazo Taifa kama Taifa ama limeshalipa au linapaswa kulipa. Taarifa hizi ni nzito na kubwa kweli kweli, wakati ambapo Taifa tunapiga kelele kwamba, tumekosa fedha nyingi kwa ajili ya kufanya mambo mbalimbali...

MWENYEKITI: Umetaka Mwongozo wangu sasa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Naendelea na nakuja kwenye Mwongozo wangu.

MWENYEKITI: Muda hatuna, usihutubie sana.

MHE. MOSES J. MACHALI: Naomba nimalizie...

MWENYEKITI: Maliza basi kwa ufupi Mheshimiwa. Ahsante. (*Kicheko*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini Kiti kisiamue Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, akatupa taarifa sahihi zenye ushahidi kuhusiana na suala hili ili Bunge lenye dhamana kwa mujibu wa Ibara ya 93 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya suala la kuisimamia na kuishauri Serikali liweze kuondoa kizungu mkuti kilichojificha na itakumbukwa kwamba, Kaimu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Samuel Sitta ambaye amekuwa Spika wa Bunge hili katika Bunge la Tisa amepata kuzungumzia juu ya utata uliogubika katika suala la *Dowans*?

Nilikuwa naomba Kiti chako kimruhusu Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, atupe ushahidi na taarifa kamili ili tuweze kuondokana na Taifa kupoteza mabilioni ya shilingi ambayo ni ya walipa kodi wa Taifa hili, vinginevyo tutaendelea kupoteza fedha nyingi ndani ya Taifa letu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, umeeleweka. Mheshimiwa *AG*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu ana haki ya kupata taarifa kuhusu kesi ya *Dowans*, lakini Wabunge ambao wanategemewa kuwa na ufahamu mkubwa wa Kanuni na Utaratibu za uendeshaji wa shughuli za

Bunge hapa Bungeni wanatakiwa kuwa makini. Mzungumzaji aliyesema anafahamu kabisa kwamba, kesi ya *Dowans* iko Mahakamani na kama hafahamu afahamishwe kwamba, Serikali si sehemu ya kesi hiyo. Sasa huu ushahidi alionao nafikiri atautoa Mahakamani. (*Makofi*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Taarifa!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Kanuni ya 64(1)(c) inasema: "Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama." Hii ni Kanuni yetu na nakushauri Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kutumia maneno ya kuudhi au kubembeleza bembeleza, Mwongozo ulioombwa hauna manufaa. Hauna manufaa narudia na kwamba, unavunja Kanuni zetu na naomba uukatae. (*Makofi*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Taarifa! (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Naomba kwanza niongee. Naomba nisome hii Kanuni ya 64(1)(c), naomba mnisikilize wote, inasema hivi: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama au jambo lolote ambalo lilijadiliwa na kutolewa maamuzi kwenye Mkutano uliopo au uliotangulia na ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahsusi na

vile vile hatapinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge isipokuwa tu kwa kutoa hoja mahsusi inayopendekeza kuwa uamuzi huo uangaliwe upya.

Sasa kwa sababu tumepewa taarifa na Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu, suala hili la *Dowans* liko Mahakamani na tunavyojua mihimili hii haiingiliani, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuheshimu matakwa ya Kanuni hii. Lakini vile vile tuzingatie hizi Kanuni zetu kwamba, huwa hatuna taarifa juu ya taarifa, hatuna mwongozo juu ya mwongozo. Tukiyajua haya naomba tujaribu sana kuyazingatia ili tufanye kazi yetu ya Kibunge.

Sasa kama Mheshimiwa Kafulila ambaye alisema kwamba, ana ushahidi mwingi kuhusiana na suala hili, kwa sababu suala hili bado liko Mahakamani, bado ataisaidia Mahakama kwa kuipelekea taarifa sahihi juu ya suala hili, naomba afanye utaratibu wa kupeleka ushahidi huu Mahakamani ili tuisaidie Mahakama kufanya maamuzi ya haraka. Naomba tuendelee.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Taarifa!

WABUNGE FULANI: Mmmh!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mnaguna nini! Subiri muelezwe taarifa, nyie hamjui mnapiga kelele.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Taarifa!

MWENYEKITI: Kaa. Naomba pia turudie Kanuni zetu ambazo zinatwambia kwamba, unapotaka kuongea

kwanza, simama kimya na jicho la Spika litakuona na kukuruhusu. Lakini utaratibu wa sasa wa kuanza kuwasha *microphone*, kuongea kabla ya ruhusa tunavunja Kanuni vile vile, naomba tuzilinde Kanuni hizi. Kwa hiyo, kutokana na kwamba muda wetu hauturuhusu naomba nimruhusu Mheshimiwa Sabreena Sungura na baadaye Mheshimiwa Yahya.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo wako kutokana na Kanuni ya 68(7), naomba nisiisome ili kuokoa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ratiba ambazo tunazo Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, leo hii ilikuwa iletwe Mezani Hati kuhusiana na Wizara ya Maliasili na Utalii. Lakini bila taarifa imewasilishwa Hati ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wabunge wengi ambao wamepeleka makaratasi jana kwa ajili ya kuchangia walijikita katika suala zima la hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa mabadiliko haya Wabunge hatunayo. Tulitaka Mwongozo wako kuhusiana na suala hili?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mbunge. Naomba uangalie ratiba mpya ambayo imetolewa na Ofisi ya Bunge.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia kanuni ile ile 68(7) bila ya kurejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili kila mtu ana haki sawa bila ya ubaguzi, bila ya matatizo yoyote kujitokeza ambao tunafuata safu yako ya mbele huko, lakini nimegundua kwa muda mrefu sana katika Bunge hili na Bunge hili limeongezwa idadi ya Wabunge kwa maslahi ya nchi kwamba nchi yetu kubwa sana, lakini sio sababu kwamba Mbunge kukosa haki ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimegundua kwamba mara nyingi Wabunge wanaokaa huku nyuma kama si swali lake la msingi fursa hazitoki. Mara nyingi kwenye Kiti mnaangalia nafasi za mbele tu, wakati yanatokea masuala muhimu sana ambayo Mbunge anahusika nayo katika Jimbo lake, lakini fursa inakosekana. Kwa hivyo, tungependa kupata mwongozo labda kuna vigezo fulani huko ambavyo mnatumia kwa wanaokaa huko mbele. Kwa hiyo, tulitaka kupata mwongozo wako ili na sisi tuelewe huku taratibu zipi ambazo zinatumika ili na zile fursa na sisi tuweze kuzitumia ili tuweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Nashukuru nimepokea, nitatoa Mwongozo wangu baadaye.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2012/2013
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Bunge lako likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika mwaka 2011/2012 na malengo ya Wizara katika bajeti ya mwaka 2012/2013. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Waheshimiwa Wabunge kuwa na afya njema na hivyo kuweza kushiriki mkutano huu wa Nane wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba nitangulize dua zangu kwa Mwenyezi Mungu kuwa azipokee na kuzilaza pema roho za Waheshimwa Wabunge wenzetu waliotangulia mbele ya haki tokea Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2011/2012 ulipofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Daktari Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Daktari Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa uongozi wao mahiri. Nawashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa, ulioniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuongoza sekta hii muhimu na

mtambuka katika maendeleo ya nyanja zote za maisha katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Daktari Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Makamu wake wawili Mheshimiwa Maalim Seif Shariff Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Balozi Ali Idd Seif, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar. (*Makofi*)

Kwa namna ya pekee namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani kubwa aliyoionesha kwangu kwa kuamua niendelee kuongoza Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakati wa mabadiliko ya Baraza la Mawaziri aliyoyafanya mapema mwezi Mei 2012. Napenda kumhakikishia kuwa nitaendelea kujenga timu yenye nguvu ili kwa pamoja tujenge sekta ya ardhi yenye tija kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na taratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Spika kwa umahiri na umakini ambao ameonesha katika kuongoza shughuli za Bunge. Hongera sana na Mwenyezi Mungu aendelee kumwongoza na kumpa hekima zaidi. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa na Naibu Spika wa Bunge letu kwa kazi nzuri katika kuendesha shughuli za Bunge

pamoja na Wenyeviti wote. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Wenyeviti Jenista Joakim Mhagama (Mbunge wa Peramiho), Sylivester Massele Mabumba (Mbunge wa Dole) na Mussa Zungu Azzan (Mbunge wa Ilala), kwa kuongoza vyema shughuli za Bunge tangu wachaguliwe kushika nyadhifa za Uenyekiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza wafuatao kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika Baraza la Mawaziri kufuatia mabadiliko aliyoyafanya mwezi Mei 2012: Mheshimiwa Daktari William Augustao Mgimwa kuwa Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo kuwa Waziri wa Nishati na Madini; Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chiza kuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika; Mheshimiwa Daktari Harrison George Mwakyembe kuwa Waziri wa Uchukuzi; Mheshimiwa Daktari Fenella Ephraim Mukangara kuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Daktari Abdallah Omari Kigoda kuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kuwapongeza wafuatao kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri katika Wizara mbalimbali: Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Wizara ya Fedha; Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Wizara ya Fedha; Mheshimiwa Daktari Seif Suleiman Rashid, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Wizara ya Nishati na Madini;

Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Daktari Charles John Tizeba, Wizara ya Uchukuzi; Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki, Wizara ya Katiba na Sheria; Mheshimiwa Stephen Julius Maselle, Wizara ya Nishati na Madini na Mheshimiwa Mhandisi Daktari Binilith Satano Mahenge, Wizara ya Maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa na walioteuliwa katika kipindi cha mwaka uliopita kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki na Bunge la Afrika. Ni matumaini yangu kuwa watatuwakilisha vyema kwa maslahi na manufaa ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini kwa kunipa ushirikiano wa karibu katika kutimiza majukumu yangu nikiwa Mbunge wao. Pamoja na kuwa na kazi nyingi za Kitaifa, wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini wamekuwa wakinipa ushirikiano mzuri na kujitahidi kukutana nami ninapopata nafasi kufika Jimboni kwa kuhudhuria vikao na mikutano katika Tarafa zao au kupokea wageni na wataalam waelekezi ninaowatuma kufika kusukuma maendeleo yetu. Nawashukuru sana kwa uelewa na ushirikiano na uongozi madhubuti wa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji kuunda Mifuko ya Maendeleo ya Kata ambayo italeta

mapinduzi katika kupunguza umaskini na kutuletea maendeleo endelevu katika Jimbo letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Madiwani ambao tayari wamesajili Taasisi ya Mifuko hiyo katika Kata za Mubunda, Kyebitembe, Rulanda, Muleba, Bureza, Magata Karutanga, Kimwani, Mazinga, Nyakabango, Nshamba, Kishanda, Buganguzi, Burungura, Buhangaza, Kashasha, Ijumbi, Biirabo na Muleba Mjini. Ninawahimiza wale ambao bado hawajakamilisha zoezi hili wakazane tusonge mbele kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natuma salamu kwa vijana wanaoshiriki katika mashindano ya kandanda ya Kombe la Anna Tibaijuka *Cup.* Nawapongeza wale ambao wameshinda mashindano ya Kata na naamini mwisho wa mwaka tutakapocheza fainali washindi wataweza kutoa vijana wa Muleba kujiunga na *Taifa Stars.* Nimefurahi kusikia kwamba na wasichana hawakubaki nyuma wameitikia wito wangu na kushiriki michezo ya riadha inayotangulia mashindano ya mpira. Vijana michezo ni maendeleo. Kwa wenye vipaji, Muleba tusikubali vijana wetu kubaki nyuma kwa kuwa tu tuko mbali na majiji makubwa nchini hususan Dar es Salaam. Kwa kupitia ligi yetu, wenye uwezo wataibuka na kung'ara na kusonga mbele. Aidha, nawashukuru ndugu, jamaa na marafiki walionisaidia na kunipa ushirikiano wa karibu katika kutimiza majukumu ya Uwaziri na Ubunge. Nawashukuru wananchi na kuwahakikishia popote pale mlipo, iwe Tarafa ya Nshamba, Kimwani au Muleba yenyewe, kwamba tutayalinda mafanikio

tuliyoyafikia na kuongeza kasi zaidi ili kufikia malengo ya kulinda amani, utulivu na kufikia maisha bora. Namwomba Mwenyezi Mungu amwezeshe kila mwananchi kulitambua hili na kuchangia katika nafasi yake kwa kadri ya uwezo wake kufikia maisha bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, natuma salamu kwa mama yangu mzazi Mama Aulelia Kajumulo hapo Muleba. Sala zake za kila siku anapokuwa na nguvu zinasikika maana huku mie ni mzima wa afya na mambo yangu sio mabaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako pia nitambue ndugu zangu ambao kwa bahati mbaya hukuwataja Bi Melisa Kataraya na Mr. Nurdin Katombo ambao wamekuja kusikiliza hotuba hii. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa dhati viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi (CCM), viongozi na watendaji wa Serikali kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Kwa namna ya kipekee natoa shukurani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa James Daudi Lembeli (Mbunge wa Kahama), kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Natoa shukurani za pekee kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye (Mbunge wa Arumeru Magharibi) kwa ushirikiano na umoja

tuliojenga kutekeleza majukumu yetu na pia nampongeza kwa Mheshimiwa Rais kuamua aendelee na wadhifa wake huo. Nawashukuru pia Katibu Mkuu Bw. Patrick Rutabanzibwa; Naibu Katibu Mkuu, Bibi Maria Bilia; watendaji katika Idara, Vitengo, Shirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushauri na mshikamano wao katika kupanga na kutekeleza mipango ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Watanzania wengi wanatambua changamoto kubwa zinazoikabili sekta yetu, lakini hakuna kinachoshinda umoja, maana ni nguvu ya pekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la mahitaji ya ardhi kwa matumizi mbalimbali haliepukiki kutokana umuhimu wake kijamii na kiuchumi. Ili kuwezesha wananchi na wawekezaji kupata ardhi wanayohitaji, Wizara imeweka vipaumbele katika kupanga matumizi ya ardhi kwa kuzingatia mazingira na mahitaji halisi, kujenga mfumo utakaorahisisha upimaji na kupunguza gharama za kupima ardhi, kumilikisha ardhi kwa haki, pamoja na kulinda haki za wamiliki halali wa ardhi. Katika kufikia malengo hayo Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kubadilisha utunzaji wa kumbukumbu za sekta ya ardhi kutoka mfumo usio unganishi kwenda kwenye mfumo unganishi wa kielektroniki;

(ii) Kukosekana kwa ardhi iliyopangwa na kupimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali mijini na vijijini ikilinganishwa na mahitaji;

(iii)Kuwepo kwa kasi ndogo ya kutoa elimu kwa umma kuhusu sera, sheria na kanuni za uendelezaji ardhi, nyumba na makazi;

(iv) Kukosekana kwa rasilimali za kutosha kwa ajili ya utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, upangaji wa miji na upimaji wa ardhi nchini;

(v)Kukosekana kwa mipango jumuishi ya kuwezesha kupungua kwa gharama za ujenzi wa nyumba bora mijini na vijijini;

(vi) Kuwepo kwa uwezo mdogo wa utekelezaji na usimamizi wa sera na sheria za ardhi unaosababisha kuwepo kwa ongezeko la ujenzi holela na uvamizi wa maeneo yaliyotengwa kwa matumizi mbalimbali ya jamii mijini na vijijini;

(vii) Kuongezeka kwa migogoro ya ardhi na nyumba mijini na vijijini;

(viii)Kuwepo kwa upungufu mkubwa wa watumishi, vitendea kazi na miongozo ya sekta ya ardhi katika ngazi ya Halmashauri;

(ix) Nakishi ya bajeti inayotengwa kwa sekta ya ardhi na makazi; na

(x) Kuwepo kwa utamaduni ambao bado hauzingatii mfumo wa ubananaji wa makazi ya mijini na kasi yake vinavyolazimisha kuheshimu sheria na taratibu za mipango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni baadhi ya changamoto zinazokwamisha uendelezaji wa dhana halisi za upangaji, upimaji na utawala wa ardhi. Ili kukabiliana na changamoto hizo Wizara imepanga kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuendelea kujenga mfumo unganishi wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi (*Integrated Land Management Information System*) utakaowezesha upatikanaji na utumiaji wa kumbukumbu za sekta ya ardhi kwa ufanisi;

(ii) Kuanza utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (*National Land Use Framework Plan*) kwa kuongeza kasi ya kupanga na kuandaa mipango ya jumla na ya kina na upimaji wa ardhi;

(iii)Kuendelea kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi nchini hususan katika vijiji vilivyopo mipakani;

(iv) Kuendelea na mchakato wa kuanzisha Wakala wa Hazina ya Ardhi (*National Land Bank Agency*) na Mfuko wa Fidia ya Ardhi (*Land Compensation Fund*);

(v)Kuandaa na kutekeleza mpango wa mahitaji ya mafunzo kwa Kamati mbalimbali za usimamizi wa ardhi nchini na programu ya elimu kwa umma kuhusu sera, sheria na kanuni za ardhi, nyumba na makazi;

(vi) Kuendelea na mchakato wa kujenga kituo cha kupokea picha za *satellite* ili kurahisisha utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, upangaji wa miji na upimaji wa ardhi nchini;

(vii) Kubuni mfumo shirikishi wa uendelezaji wa ardhi nchini ambapo watoa huduma wote watashirikishwa katika dhana ya *sites and services;*

(viii) Kuongeza kasi ya kueneza matokeo ya utafiti unaofanywa na Wakala wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi *(NHBRA)* na kuanzisha vikundi vya ujenzi katika ngazi ya Halmashauri na kutoa mafunzo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba bora na vifaa vya ujenzi;

(ix) Kuhakikisha Shirika la Nyumba la Taifa linaendelea kujenga nyumba za kutosha kwa ajili ya kuuza na kupangisha kwa watu wa vipato mbalimbali na kuhimiza Halmashauri kuanzisha vitengo vya nyumba katika Halmashauri zao, yaani *Council Housing* pamoja na kuhamasisha sekta binafsi na Vyama vya Ushirika wa Nyumba (*Housing Cooperatives*) kujenga nyumba za kuuza na kupangisha kwa gharama nafuu;

(x) Kuendelea kutekeleza Programu ya Taifa ya Kurasimisha na Kuzuia Makazi Holela Mijini kwa kushirikiana na Halmashauri;

(xi) Kuandaa utaratibu utakaowezesha mamlaka za upangaji kuweka mfumo wa udhibiti na uendelezaji wa ardhi katika ngazi ya Kata;

(xii) Kuendelea kuimarisha vyombo vya kusimamia maadili na weledi wa wataalam wa sekta ya ardhi katika ngazi zote;

(xiii) Kuendelea kuunda na kuimarisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa;

(xiv) Kubuni mbinu mpya za kisasa za kupata fedha za kuendeleza shughuli za Wizara nje ya bajeti kuu ya Serikali (*extra-budgetary financing mechanisms*) na Serikali za Mitaa, hususan kupitia mikopo ya benki au hisa za makazi (*municipal bonds*); na

(xv) Kutoa elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya mfumo wa makazi kutoka vijijini kwenda mjini na umuhimu wa mabadiliko ya utamaduni, mila na desturi na tabia zinazoendana na hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 23.6 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato katika sekta ya ardhi. Hadi Juni, 2012 jumla ya Shilingi bilioni 17.1 ambazo ni sawa na asilimia 72.5 ya lengo zilikusanywa. Upungufu wa makusanyo ya maduhuli ulitokana na baadhi ya changamoto nilizozieleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013 Wizara imeweka lengo la kukusanya Shilingi bilioni 99.8. Maduhuli haya yatakusanywa kwa kutumia mikakati ifuatayo: Kuongeza kodi ya ardhi na tozo; kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi; kupanga, kupima na kumilikisha maeneo mapya; kukamilisha upimaji na umilikishaji wa viwanja kwenye maeneo ambayo upimaji wake haujakamilika; kuhamasisha wananchi

kulipa kodi ya ardhi na kuwachukulia hatua za kisheria wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuhimiza wananchi kulipa kodi ya pango la ardhi na tozo nyingine kwa mujibu wa sheria za nchi ili kuepuka usumbufu wa kushtakiwa Mahakamani, kunyang'anywa ardhi na kulipa faini. Nasisitiza kwamba muda wa kuvumiliana na wa visingizio umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 50.89. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 9.3 sawa na asilimia 18 ya fedha zilizoidhinishwa zilitengwa kwa ajili ya mishahara, Shilingi 19.6 sawa na asilimia 39 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi bilioni 21.9 sawa na asilimia 43 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Juni, 2012 jumla ya fedha zilizopatikana ni Shilingi bilioni 34.65 sawa na asilimia 68.1 ya fedha zilizoidhinishwa na jumla ya Shilingi bilioni 34.45 zilitumika. Kiasi kilichotumika ni sawa na asilimia 99.4 ya fedha zilizopatikana. Kati ya fedha zilizotumika Shilingi bilioni 8.96 zilitumika kwa ajili ya mishahara, Shilingi bilioni 19.49 kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi bilioni 6.0 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za maendeleo zilizopatikana zilikuwa sawa na asilimia 28 tu ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wote wanatambua mchango mkubwa ambao rasilimali ardhi inatoa katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Kutokana na umuhimu huo, Wizara yangu imeendelea

na jukumu la kuhakikisha usalama wa milki kwa kutoa hati, kukagua na kuhakiki milki. Majukumu mengine ni pamoja na kutwaa ardhi kwa manufaa ya umma na kubatilisha milki kwa wanaokiuka masharti ya milki zao. Vilevile, Wizara inatoa elimu na miongozo kuhusu sera, sheria na kanuni za ardhi. Pia, inatoa vibali vya uhamisho wa milki na kuratibu utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Hati za Hakimiliki ya Kimila kwa kushirikiana na mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria za Ardhi, mamlaka za ugawaji wa ardhi ziko katika ngazi tatu za vijiji; Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji; na Taifa. Majukumu ya mamlaka hizi yameainishwa katika Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 na Kanuni za sheria hizo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 76 ya Kanuni za Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Halmashauri ya Kijiji ina uwezo wa kugawa ardhi kwa mwanakijiji au mtu yeyote ilimradi awe ni raia wa Tanzania na ardhi iwe na ukubwa usiozidi hekta 21 kama eka 50 hivi. Halmashauri ya Wilaya, kupitia Kamati yake ya kugawa ardhi, ina mamlaka ya kugawa ardhi ya Kijiji yenye ukubwa wa kati ya hekta 21 na 50. Ardhi ya Kijiji yenye ukubwa wa zaidi ya hekta 50 inagawiwa kwa ridhaa ya Kamishna wa Ardhi.

Kwa upande wa ardhi ya kawaida Halmashauri ya Kijiji inaruhusiwa kugawa ardhi yenye ukubwa usiozidi hekta 21. Halmashauri ya Wilaya inaruhusiwa kugawa ardhi yenye ukubwa wa kati ya hekta 21 na hekta 202. Mapendekezo ya kugawa ardhi katika fukwe, visiwa vidogo na kwa ajili ya uwekezaji kupitia Kituo cha

Uwekezaji Tanzania *(TIC)* yanatakiwa yawasilishwe kwenye Kamati ya Taifa ya Kugawa Ardhi ambayo Mwenyekiti wake ni Kamishna wa Ardhi. Wajumbe wa Kamati hiyo wanatoka Wizara za Ulinzi, Kilimo, Mifugo na Viwanda, na Tume ya Mipango. Kamati hiyo huteuliwa na Waziri wa Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na sheria kuonesha bayana majukumu ya mamlaka husika, kumekuwepo na tabia ya baadhi ya mamlaka kugawa ardhi inayozidi mamlaka yake. Aidha, baadhi ya mamlaka zikiwemo za vijiji zimekuwa zikitoa ardhi kwa waombaji ambao si raia wa Tanzania, kinyume cha sheria. Tabia hii husababisha migogoro na hasara kwa waliopewa ardhi bila kufuata utaratibu. Kupitia Bunge lako Tukufu naziagiza mamlaka za vijiji na Halmashauri kufuata sheria, kanuni na taratibu za kugawa ardhi ili kuepusha malalamiko na migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza kuwa ardhi kwa ajili ya wawekezaji hutolewa na Kamishna wa Ardhi kwa mamlaka ambayo yako chini ya Rais. Hakuna tena njia nyingine ya kugawa ardhi nje ya utaratibu huu. Ukiwa na ardhi yako ukaamua kumpa mtu mwingine huna budi kuirudisha kwa Kamishna (*surrender*) ili igawiwe upya kwa mtu mwingine. Tofauti ni kuhamisha miliki yote ya ardhi yako kwa mtu mwingine kwa kumuuzia. Makubaliano yanayofanyika kati ya Halmashauri na Wawekezaji au Wamiliki wengine na wawekezaji nje ya utaratibu huu ni batili, sharti yapate baraka za Kamati ya Kugawa Ardhi ya Taifa kabla hatimiliki mpya hazijatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikuwa na lengo la kutoa hatimiliki 21,000. Hadi kufikia Juni, 2012, Wizara ilitoa hatimiliki 23,610 sawa na asilimia 112.4 ya lengo, kwa hiyo, tumepita malengo. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu inatarajia kutayarisha na kutoa hatimiliki 40,000. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa zinamilikisha viwanja vyote vilivyopimwa na kuandaa hati ili wananchi waweze kuwa na milki salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu iliahidi kufungua Ofisi ya Ardhi ya Kanda ya Magharibi Mjini Tabora itakayohudumia Mikoa ya Tabora, Katavi, Shinyanga na Kigoma. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Jengo la Ofisi limepatikana Mjini Tabora na ofisi hiyo itaanza kutoa huduma mwaka huu wa fedha. Huduma hizo ni za mipangomiji na vijiji, upimaji, umilikishaji, usajili, uthamini na ushauri kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 inatambua kuwa ardhi yote ni mali ya umma, hivyo mfumo wa kumiliki ardhi ni ule wa haki ya kutumia na siyo kuhodhi. Kwa maana hiyo, kila anayemilikishwa ardhi ana wajibu wa kuiendeleza kwa matumizi yaliyopangwa na asipofanya hivyo hatua za kufuta milki hizo zitachukuliwa na kurudishwa ardhi husika mikononi mwa Mheshimiwa Rais. Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Utwaaji Ardhi, Na. 47 ya mwaka 1967 (Sura ya 118) pale ambapo ardhi itahitajika kwa manufaa ya umma itatwaliwa kwa mujibu wa sheria hii.

Utaratibu wa utwaaji na ubatilishaji unaanzia ngazi ya Halmashauri hadi ngazi ya Taifa. Katika kutekeleza majukumu haya kwa mwaka 2011/2012, ilani za ubatilisho zilizotumwa ni 792 na jumla ya milki 72 zilibatilishwa na kutwaliwa na milki 1,512 zilihamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kutwaa ardhi na kubatilisha milki kwa mujibu wa sheria na inatarajia kushughulikia maombi 1,700 ya uhamisho wa milki. Ili kuhakikisha kuwa ardhi inatumika kwa ufanisi natoa agizo kwa Halmashauri zote nchini kuwasilisha Wizarani taarifa za viwanja na mashamba yaliyotelekezwa au kutumika kinyume na masharti ya milki ili taratibu za kubatilisha milki ziweze kuchukuliwa. Nifafanue hapa kwamba kuna wengi wanaolalamika kwamba Wizara ya Ardhi haijamwona mtu ambaye atumie ardhi. Ardhi tunalinda wote kila mtu hapa ni askari ardhi. Kama kuna mtu ana shamba na halimi utuletee taarifa uwe *pro-active*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999, Wizara yangu inaendelea kutoa elimu kwa wananchi, kupima na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji, kuhakiki mashamba na kuratibu utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Hati za Hakimiliki ya Kimila. Utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji unaviwezesha vijiji kutambua maeneo yao kiutawala na kuwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi. Vile vile, utoaji wa hati za hakimilki za kimila unawezesha wananchi kuwa na milki salama na kuwawezesha kutumia ardhi kama mtaji, hivyo kuwawezesha kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliweka lengo la kutoa Vyeti 3,732 vya Ardhi ya Kijiji. Hadi Juni 2012 ilitoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji 1,950. Idadi hii inafanya jumla ya Vyeti vya Ardhi ya Kijiji vilivyotolewa kufikia 9,460 kati ya Vijiji 11,817 vilivyosajiliwa nchini. Pia, Wizara iliandaa, kusajili na kutoa Hati za Hakimilki ya Kimila 21,169, kati ya lengo la hati 45,000. Natoa pongezi kwa Halmashauri zote zinazoendelea na utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 kwa kutenga fedha kwa ajili ya uhakiki na upimaji wa mashamba pamoja na utoaji wa hatimilki za kimila kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri hizo ni: Moshi Vijijini, Mwanga, Hai, Babati, Nachingwea, Ruangwa, Lindi Vijijini, Mtwara Vijijini, Masasi, Newala na Nanyumbu. Halmashauri nyingine ni Kasulu, Kigoma Vijijini, Kibondo, Bunda, Kilolo, Iringa Vijijini, Ludewa, Njombe, Mpanda na Singida Vijijini. Natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini kuiga mfano huu kwa kutenga fedha kwa ajili ya kupima na kuhakiki mashamba ya wananchi na kuwamilikisha. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa nafasi zao kama wajumbe wa Baraza la Madiwani kuhamasisha wananchi kudai kumilikishwa ardhi yao na kuhimiza Halmashauri za Wilaya zao kutoa huduma za upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi kwa wananchi. Napenda kuwahakikishia ushirikiano kutoka Wizara yangu mtakapohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itakamilisha utayarishaji na utoaji wa

Vyeti vya Ardhi ya Vijiji kwa Vijiji 2,007 vilivyopimwa. Pia, Wizara yangu kwa kushirikiana na MKURABITA, Halmashauri za Wilaya na wadau wengine itaendelea kuratibu utayarishaji na utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila 50,000 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilipanga kusajili nyaraka za kisheria 60,000 katika mwaka 2011/2012. Hadi kufikia mwezi Juni 2012, nyaraka za kisheria 64,632 zilisajiliwa. Kati ya nyaraka zilizosajiliwa, 27,452 ni hatimiliki na 28,990 ni nyaraka nyingine zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334). Vilevile, nyaraka 7,280 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 117) na nyaraka 910 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika (Sura ya 210). Kwa mwaka 2012/13, Wizara inakusudia kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria 75,000. Kati ya hatimiliki na nyaraka hizo, 35,000 zinatarajiwa kuwa hatimiliki na 40,000 ni nyaraka nyingine za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanahamasishwa kupima maeneo yao na kupata hatimiliki, kwani hati hizi zina umuhimu mkubwa ni pamoja na kuwawezesha kutumia kama dhamana za mikopo kwenye taasisi za kifedha na kuepusha migogoro ya ardhi. Natoa rai kwa wananchi kufanya uhakiki kwenye ofisi za usajili wa hati wanapokusudia kufanya miamala inayohusu ardhi. Hii itasaidia kuwaepusha na wimbi la utapeli ambao umepelekea kuwepo kwa hatimiliki za kughushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uthamini wa Mali. Wizara yangu inahusika kufanya na kuidhinisha taarifa za uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika na kusimamia utendaji wa taaluma nchini. Uthamini wa mali unafanyika ili kuwezesha maamuzi ya miamala mbalimbali ya mali kufanyika. Zipo aina kuu mbili za uthamini ambazo ni Uthamini wa Ujumla na Uthamini wa Kisheria. Uthamini wa Ujumla ni ule unaofanyika kwa kuzingatia misingi ya kitaaluma na hazina maelekezo maalum ya kisheria. Mifano ni uthamini kwa ajili ya kuwezesha maamuzi ya mauzo au manunuzi ya mali, kuweka mali rehani, kuomba mikopo benki, dhamana ya mahakama, mizania na bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthamini wa Kisheria ni ule ambao pamoja na misingi ya kitaaluma unazingatia maelekezo maalum ya sheria mahsusi ya Bunge kwa mfano ni uthamini kwa ajili ya fidia, kukadiria kodi za mapato, ushuru wa serikali, kodi za majengo na kodi za viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthamini wa mali unategemea maombi yanayowasilishwa kutoka kwa wadau mbalimbali ambao ni taasisi za umma, makampuni na watu binafsi. Hata hivyo, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu ililenga kufanya na kuidhinisha taarifa za uthamini wa Jumla wa mali zipatazo 13,000. Hadi Juni 2012, Wizara iliidhinisha taarifa za uthamini 11,445 ambazo kati yake taarifa 1,507 ziliandaliwa na Wizara na 9,938 zilipokelewa kutoka kampuni binafsi za uthamini na Halmashauri za Miji na Wilaya. Kwa mwaka 2012/13 Wizara yangu

imelenga kuthamini na kuidhinisha taarifa za uthamini wa mali zipatazo 14,000 kwa madhumuni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia inaandaa na kuidhinisha taarifa za uthamini, hususan uthamini kwa ajili ya ulipaji fidia kwa wananchi wanaoguswa na utekelezaji wa miradi yenye manufaa kwa umma. Katika mwaka wa fedha 2011/12, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini wa mali 11,256 ikilinganishwa na lengo la 9,000 la waliloguswa na miradi ya Kitaifa iliyojumuisha uwekezaji kwenye maeneo ya migodi katika Vijiji vya Katoma na Nyamalembo Wilayani Geita, Nyamongo *North* Mara na Nyalanguru Wilayani Tarime; uwekezaji kwenye eneo la mtambo wa gesi asilia huko Mnazi Bay na njia ya bomba la gesi eneo la Somanga-Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, uthamini ulifanyika kwenye eneo linalotarajiwa kumilikishwa kwa Kampuni ya *Ecoenergy* kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha miwa na Kiwanda cha Sukari kilichopo katika Kijiji cha Makurunge, Wilayani Bagamoyo. Vilevile, maeneo ya barabara chini ya *TANROADS* zinazojumuisha barabara za Babati-Singida, Dumila-Rudewa na Mangaka-Nanyumbu-Mtambaswala na maeneo ya miradi ya upimaji viwanja Wilaya za Masasi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, Wizara imelenga kufanya uthamini wa fidia kwa mali zipatazo 15,000 kutokana na miradi mbalimbali itakayokuwa inatekelezwa nchini ikiwepo mradi wa kuendeleza eneo la Kigamboni na mradi wa ujenzi wa

Kituo cha Kimataifa cha Biashara Kurasini, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ni msimamizi wa taaluma ya uthamini. Imeendelea na jukumu la kujenga Hazina ya Takwimu za Uthamini (*Valuation Database*) kwa lengo la kuwa na takwimu madhubuti za ukokotoaji wa thamani ya ardhi, majengo, mazao na mimea kwa kiwango cha soko. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri iliandaa viwango elekezi vya thamani ya ardhi katika Miji 10 ambayo ni Jiji la Dar es Salaam, Mbeya, Tanga na Arusha; Manispaa ya Morogoro, Iringa, Sumbawanga, Lindi na Bukoba na Halmashauri ya Mji wa Kibaha. Ili kuwajengea uwezo na kuimarisha ushiriki wa wathamini katika zoezi la kujenga Hazina ya Takwimu za viwango vya thamani vya soko, Wizara iliendesha mafunzo kwa wathamini katika Kanda za Mashariki (Dar es Salaam), Kaskazini, (Moshi), Ziwa (Mwanza) na Kusini Magharibi (Mbeya).

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuhuisha viwango vya thamani ni la kudumu na litaendelea kila mwaka kwa vile thamani ya ardhi na majengo katika soko hubadilika kutokana na sababu mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa kadri miaka inavyopita. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kuandaa viwango elekezi kwa miji ya Mikoa 11 sambamba na uchambuzi wa kina wa takwimu kwenye miji yenye viwango elekezi. Aidha, Wizara itaandaa mfumo wa uthamini wenye uwezo wa kutunza, kuchambua na kutoa taarifa ya takwimu hizo kwa wadau mbalimbali

wa huduma za uthamini na kuhuisha viwango hivyo kwa kuzingatia mwenendo wa soko la mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa, Wataalam wa uthamini nchini watatumia ujuzi walioupata kutokana na mafunzo hayo kushiriki kikamilifu katika zoezi la kujenga mifumo ya kukusanya, kutunza na kutumia takwimu za viwango vya thamani katika maeneo yao. Vile vile, nazishauri Halmashauri za Miji na Wilaya zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha wataalam wa uthamini kutekeleza majukumu yao hususan hili la kusimika viwango vya thamani ya ardhi na mazao katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzishwa kwa Hazina ya Ardhi (*Land Bank*). Ili ardhi iweze kuingizwa kwenye hazina ya ardhi, ni lazima ardhi hiyo iwe imepangwa, imepimwa na imesajiliwa na haina mgogoro kuhusu umiliki wala matumizi yake na iwe na ukubwa wa kutosha kulingana na matumizi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012, Wizara iliahidi kuanzisha chombo kwa ajili ya kusimamia Hazina ya Ardhi na kuanzisha Mfuko wa Fidia ya Ardhi. Kazi hiyo imeanza na kwa mwaka 2012/2013 Wizara inatarajia kukamilisha uanzishaji wa chombo hicho na Mfuko wa Fidia ya Ardhi. Chombo hicho kitasimamia utoaji wa ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje kwa misingi ya kuingia ubia wa kumiliki pamoja hisa kati ya wananchi na wawekezaji hao (*land for equity*), ambapo hisa zitatolewa kwa uwiano na thamani ya

mtaji wa mwekezaji (*Invested value method of land valuation)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika zaidi na ardhi katika maeneo yao na kuongeza usalama wa miradi ya wawekezaji (*Sustainability of extensive land-based investments)*. Kiwango cha chini cha hisa za Serikali katika ubia huo kitakuwa asilimia 25, na kati ya hizo mapendekezo ni kwamba angalau asilimia tano zitagawiwa kwa Halmashauri yenye eneo hilo, asilimia tano zitauzwa kwa bei ya soko kwa wananchi watakaotaka kushiriki katika miradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa Bunge lako Tukufu kuunga mkono utaratibu mpya wa kutoa ardhi kwa wawekezaji kwa msingi wa kugawana hisa utakaofuta taratibu zinazotumiwa na Halmashauri na Vijiji kwa sasa za kupewa gawio lisilozingatia msingi ya kichumi. Kwa mfano, wawekezaji kutoa zawadi ndogondogo kama visima vya maji, madarasa na kadhalika. Taratibu zitakapokamilika tutawasilisha Muswada wa Sheria ya kuanzisha rasmi chombo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kumbukumbu za Ardhi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Katika Hotuba yangu ya mwaka 2011/2012, niliahidi kuendelea na zoezi la kuweka mfumo wa kompyuta kwa ajili ya kukusanya kutunza na kukadiria kodi ya pango la ardhi kwenye Halmashauri kumi, pamoja na kuunganisha Ofisi za Ardhi za Kanda za Kaskazini na Ziwa kwenye mtandao wa kompyuta wa Wizara na kuweka mfumo mmoja wa kielektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi kufikia Juni, 2012, Wizara yangu ilikuwa imekamilisha kuweka mfumo wa kompyuta wa *Land Rent Management System (LRMS)* katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri kumi na moja (11) za Hanang, Njombe, Makambako, Same, Hai, Mbeya (W), Muheza, Kilosa, Masasi, Mpanda na Manispaa ya Dodoma na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa mfumo huo. Sambamba na hilo mfumo wa kompyuta wa *LRMS* wa vituo 17 kati ya 29 iliboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivyo ni pamoja na Jiji la Mbeya, Mwanza, Tanga, Arusha, Manispaa za Bukoba, Sumbawanga, Kigoma, Singida, Songea, Moshi, Shinyanga, Mji wa Babati, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Kilombero, Kahama, Bagamoyo na Kibaha. Aidha, Wizara imesaini mkataba na mtaalam mshauri atakayesanifu na kusimika mfumo unganishi wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi *Integrated Land Management Information System - ILMIS*. Mtaalam huyo anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo katika kipindi cha miezi 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/13, Wizara itaendelea na kazi ya kujenga mfumo wa *ILMIS*. Vilevile, itaendelea kuweka na kuhuisha mfumo wa kutunza kumbukumbu wa *LRMS* katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri 30. Mpango huu utafanikiwa tu ikiwa Halmashauri zote nchini zitaandaa na kutekeleza mpango endelevu wa kuweka na kutunza kumbukumbu sahihi za mashamba na viwanja vilivyopimwa na kumilikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi ya Nyumba na Wilaya. Wizara yangu ndiyo yenye dhamana ya kuunda na kusimamia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikamilisha taratibu za kuunda Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Wilaya tatu (3) za Nzega, Kilosa na Manyoni kama nilivyoahidi na yataanza kutoa huduma katika mwaka huu 2012/2013. Vile vile, tutaimarisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya za Kinondoni na Ilala kwa kuyapatia majengo yenye kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuanzishwa kwa Mabaraza mapya matatu (3), kwa sasa nchi nzima inayo Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 42. Pia, Wizara yangu inakusudia kukamilisha uundaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya sita za Ngorongoro, Tunduru, Mpanda, Muleba, Karagwe na Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya iliendelea kushughulikia migogoro 15,754 ya ardhi na nyumba iliyokuwepo mwezi Juni, 2011 na mingine 10,428 iliyopokelewa hadi Juni, 2012. Mwaka 2011/2012 mashauri 8,528 yaliamuliwa na mashauri 17,654 yanaendelea kusikilizwa. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuimarisha Mabaraza yaliyopo kiutendaji ili kupunguza mlundikano wa mashauri katika Mabaraza hayo. Pia, itasikiliza na kutolea maamuzi mashauri 17,654 yaliyopo. Ili kupunguza kiwango cha mashauri yanayokatiwa rufaa kwenye Mabaraza ya

Ardhi na Nyumba ya Wilaya na hivyo kuongeza ufanisi wao nahimiza Halmashauri zote nchini kuwa ziandae mpango utakaowezesha kuyaimarisha Mabaraza ya Vijiji na Mabaraza ya Kata ili yaweze kushughulikia migogoro ya ardhi kwa ufanisi katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuhimiza Wenyeviti wa Mabaraza haya kutambua kwamba wananchi wamekuwa wakiilalamikia Wizara kuhusu uadilifu na utendaji usioridhisha wa baadhi yao. Bila kupenda kuingilia uhuru wa Mabaraza, nimelazimika kuunda Tume ya Kuchunguza baadhi ya Malalamiko. Wale watakaobainika wana makosa watachukuliwa hatua stahiki. Mantiki ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ni kusogeza huduma ya utoaji haki karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hadi sasa hatuna uwezo wa kuanzisha Mabaraza kila Wilaya, Mabaraza mengi yanafanya kazi kimkoa na hii imekuwa ni usumbufu kwa wananchi. Tunawasiliana na Wizara ya Katiba na Sheria kuangalia utaratibu wa kutumia Mahakimu Wakazi wa Wilaya kwa wakati huu ambapo mtandao wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya bado haujafikia Wilaya nyingi. Migogoro ya ardhi ni mingi sana na wanaopendekeza kwamba Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yafutwe wasisahau kwa nini yaliundwa. Ilikuwa ni kwa lengo la kupunguza msongamano wa kesi za ardhi katika Mahakama zetu ambazo zina mambo mengine mengi na nyeti ambayo nayo yamerundikana huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za Upimaji na Ramani. Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani za msingi kwa nchi nzima ambazo huonesha hali halisi ya sura ya nchi na maendelezo yaliyo juu yake. Ramani hizo ni chanzo muhimu cha taarifa zinazohitajika katika kubuni na kutayarisha mipango ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utayarishaji ramani. Mahitaji ya huduma ya upimaji ardhi nchini yanaongezeka kwa kasi kutokana na mwamko mkubwa kati ya wananchi wa kutaka kumilikishwa ardhi ili waweze kuitumia katika kupambana na umaskini. Vilevile, mahitaji ya ramani na taarifa za kijiografia yanaongezeka kwa kasi kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Ramani za nchi zinahitajika kwa matumizi mbalimbali katika sekta zote. Baadhi ya sekta hizo ni ardhi na makazi, madini, nishati, ujenzi, maliasili, kilimo, maji, elimu na ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utayarishaji wa ramani unastahili kupewa umuhimu ili kuratibu vema mipango endelevu ya matumizi ya raslimali za nchi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliahidi kufunga mtambo mpya wa kisasa wa kuchapisha ramani kwa mahitaji mbalimbali nchini na kujenga kituo cha kupokelea picha za *satellite (Satellite Image Receiving Station)* ili kupata takwimu mbalimbali za ardhi kwa ajili ya kuhuisha na kutengeneza ramani mpya za nchi. Mchakato wa kutafuta fedha za utekelezaji wa

mpango wa kujenga kituo cha kupokelea picha za *satellite* unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikiainisha mipaka ya Mikoa, Wilaya, Vijiji na Hifadhi za Taifa. Uwekaji wa mipaka hiyo umekuwa ukifanyika kwa kufuata matangazo ya Serikali ambayo hutoa maelezo yanayozingatia alama mbalimbali za asili kama vile mito, maziwa, mabonde, milima na kadhalika. Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, baadhi ya alama hizo wakati mwingine hubadilika au kutoweka na kusababisha migogoro ya kiutawala katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za mipaka ndani ya nchi, matumizi ya teknolojia ya kisasa ni muhimu. Kwa hali hiyo, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itajenga na kuimarisha taarifa za kijiografia *(geo-database*). Taarifa hizo zitatumika kutafsiri Matangazo ya Serikali yanayoainisha mipaka ya kiutawala ndani ya nchi ili mipaka hiyo iweze kueleweka kwa wahusika wote. Kazi hii itaanza kwa Mikoa na Wilaya mpya zilizoanzishwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipaka ya Kimataifa. Wizara yangu ina jukumu la kuweka na kutunza alama za mipaka ya Tanzania na nchi jirani. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliahidi kufanya mazungumzo na nchi jirani katika juhudi za kukamilisha makubaliano juu ya mipaka yetu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa majadiliano na nchi za Comoro na Msumbiji yalikamilika. Mkataba wa kwanza

kati ya Tanzania, Msumbiji na Comoro kwenye alama ya utatu baharini inayotenganisha nchi hizi tatu ulikamilika na kutiwa saini tarehe 5 Desemba, 2011. Mkataba wa pili kati ya Tanzania, Shelisheli na Comoro ulitiwa saini tarehe 17 Februari, 2012. Kwa mantiki hiyo Tanzania imekamilisha upimaji wa mipaka katika Bahari ya Hindi na itatangaza eneo lake lote la ukanda wa kiuchumi baharini (*Economic Exclusive Zone*) bila ya pingamizi kutoka kwa nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya mazungumzo na nchi za Burundi na Kenya juu ya uimarishaji wa alama za mipaka. Tanzania na Kenya zimekubaliana kuanza kazi ya uimarishaji wa alama kuanzia Jasini katika Mkoa wa Tanga hadi Mkomazi katika Mkoa wa Kilimanjaro. Sehemu hiyo ina urefu wa kilometa 100 na alama nyingi zimeharibiwa na ujenzi wa nyumba kwa pande zote za mpaka. Kazi hii itafanyika mwaka 2012/2013. Ukaguzi na uimarishaji wa mpaka kati ya Tanzania na Burundi vile vile utafanyika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upimaji ardhi chini ya maji. Wizara yangu ina jukumu la kupima ardhi chini ya maji na kutayarisha ramani. Ramani hizo huonesha kina cha maji, miamba iliyopo na hutumika katika kuongoza vyombo ndani ya maji, kubaini maeneo yanayofaa kwa bandari na utafiti wa aina mbalimbali. Katika mwaka 2011/2012 watumishi watatu walihudhuria mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi yaliyohusu upimaji ardhi katika maji yenye kina kifupi baharini. Katika mwaka 2012/2013 Wizara yangu inatarajia kununua kifaa cha kupimia vina vya maji

(echo sounder). Aidha, Wizara itaendelea kuwapatia mafunzo wataalam katika fani hii ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza eneo nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini. Katika mwaka wa 2011/2012, Wizara yangu iliahidi kukamilisha na kuwasilisha Umoja wa Mataifa Andiko la kudai eneo la nyongeza nje ya maili 200 za ukanda wa kiuchumi baharini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa niliongoza ujumbe wa Tanzania kuwasilisha Andiko hilo tarehe 18 Januari 2012. Hivi sasa Tume ya Mipaka ya Baharini ya Umoja wa Mataifa inapitia andiko hilo. Serikali ya Tanzania inatakiwa kwenda tena Umoja wa Mataifa kutetea hoja ya kudai eneo hilo tarehe 7 Agosti, 2012. Natarajia kuongoza tena ujumbe wa Tanzania kwenye utetezi wa hoja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwatambua na kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, Kamati ya Ufundi na Kikosi Kazi cha Mradi huu. Kwanza, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge walioshiriki katika ziara yangu kuwasilisha andiko letu Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mbunge wa Mafia na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mbunge wa Kuteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimtambue Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi iliyoongozwa na Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Ufundi, Ndugu

Haji Adam Haji aliyekuwa Mkurugenzi wa Upimaji na Mipangomiji Zanzibar na Daktari Sellasie David Mayunga, Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mwenyekiti wa Kikosi Kazi kilichoandaa Andiko, Profesa Evelyne I. Mbede wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Sayansi na Teknolojia katika Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Katibu wake Bwana Justo Lyamuya kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wajumbe ambao ni Bwana John A. Msemwa wa Wizara ya Ardhi; Bwana Abdon D. Makishe, Bwana Omary J. Mtunguja na Bwana Kelvin R. Komba wote kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Profesa Desiderius C.P. Masalu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Mhadhiri Bwana Issa A. Hemedi wa Chuo Kikuu cha Ardhi; Bw. Adam I. Zuberi wa Wizara ya Nishati na Madini; Bwana Donald L. Chidowu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bwana Richard A. Maridadi, Mwanasheria wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Bwana Pandu S. Makame, Mwanasheria aliyekuwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hizi zimefanya kazi nzuri ambayo imewezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukamilisha Andiko la kudai kuongeza eneo ndani ya bahari lenye ukubwa wa kilomita za mraba 61,000. Eneo hili litakapopatikana litaiwezesha

Tanzania kuvuna rasilimali mbalimbali chini ya bahari kwa manufaa ya sasa na ya vizazi vijavyo. Ni sifa kubwa kwa nchi yetu kufanikisha kazi hii kwa kutumia wataalam wetu wazawa. Nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati waajiri wa wajumbe wa Kikosi Kazi kwa kuwaruhusu watumishi hawa kufanya kazi hii na nawaomba wasichoke kuendelea kutoa ushirikiano hadi kazi hii itakapokamilika na eneo kupatikana. *Inshallah* eneo hilo litapatikana kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatumia uzoefu wangu katika Umoja wa Mataifa katika kutekeleza kazi hii nyeti na muhimu. Niwaombe Watanzania wote wa bara na visiwani kutambua kwamba tunachoshughulikia sasa ni maombi ya eneo ambalo tusipofanikiwa kulipata litabaki chini ya himaya ya Umoja wa Mataifa ambapo Mataifa makubwa yatalifaidi. Nashukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kufafanua kwamba kazi hii imeshirikisha pande zote za Taifa letu ipasavyo na kufuta hisia potofu zilizokuwa zimeibuka zikidai vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa mipaka ya vijiji nchini huwezesha kutolewa kwa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji, kupanga matumizi bora ya ardhi na hatimaye kuweza kutolewa kwa Hati za Hakimilki ya Kimila. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliahidi kupima mipaka ya Vijiji 350 ambapo hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya Vijiji 206 vimepimwa katika Wilaya za Same (12), Arumeru (28), Longido (10), Mbulu (64), Uyui (66) Manyoni (22) na Kiteto (4). Kutokana na upimaji huo, mpaka sasa jumla ya Vijiji vilivyopimwa mipaka nchini

ni 11,467. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea na upimaji wa mipaka ya Vijiji 200. Aidha, upimaji wa mipaka ya Vijiji utaendelea kwa kadri vitakavyokuwa vikiongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upimaji milki. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu imeratibu na kuidhinisha upimaji wa viwanja 34,049 na mashamba 2,169 kati ya lengo la viwanja 35,000 na mashamba 800. Katika utunzaji wa kumbukumbu jumla ya plani za viwanja 15,116 zimeingizwa, hivyo kufanya jumla ya viwanja vilivyoingizwa katika mfumo wa kielektroniki kuwa 30,304. Vile vile, plani za hati (*deed plans*) 1,685 kwa viwanja vilivyopimwa nchini zilitayarishwa. Kwa sasa utoaji wa plani za hati unafanyika haraka zaidi kutokana na matumizi ya teknolojia ya digitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013 Wizara yangu inatarajia kuidhinisha upimaji wa viwanja 40,000 na mashamba 1,000 kutoka katika miji na vijiji mbalimbali nchini. Pia, Wizara itajenga alama 300 za vianzio vya upimaji *(Control points densification)* katika miji 50 ili kurahisisha upimaji ardhi nchini. Vilevile, Wizara yangu itaendesha mafunzo ya utumiaji wa mtandao mpya wa upimaji ardhi nchini kwa wapima ardhi. Ili kuharakisha upangaji na upimaji wa ardhi Halmashauri zote nchini zinashauriwa kununua vifaa vya kisasa vya upimaji ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kwamba katika Halmashauri kadhaa wapimaji hawana hata darubini ya kawaida, achilia mbali vifaa vya kisasa kama *GPS* (*Global Positioning System)* na *Total*

Station. Hii si kwa sababu ya umaskini bali kutoelewa kwamba fani hii haiwezi kuwa na manufaa bila kuwa na vifaa vya msingi hatuwezi kupima kwa macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kusimamia Mfuko wa Mzunguko wa Kupima Viwanja *(Plot Development Revolving Fund – PDRF)* unaozipatia mikopo Halmashauri kwa ajili ya kutayarisha michoro ya mipango miji, kulipa fidia, kupima viwanja na kumilikisha. Hadi Juni 2012 Mfuko wa *PDRF* ulikuwa na jumla ya Shilingi milioni 606. Aidha, Halmashauri 29 hazijarejesha jumla ya Shilingi milioni 466.6. Wizara imepokea maombi kutoka Halmashauri nane ya jumla ya Shilingi milioni 5,050. Kwa sasa Wizara inachambua maombi hayo na kutayarisha utaratibu mpya utakaowezesha kukopesha na kurejesha kwa wakati. Napenda kurudia maelekezo yangu kwa Halmashauri zilizokopeshwa kurejesha mikopo hiyo kwa wakati ili kuziwezesha Halmashauri nyingine kukopa kwa ajili ya kutwaa maeneo na kupima na kumilikisha ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mradi wa viwanja 20,000, Wizara yangu ilizikopesha Halmashauri nne jumla ya Shilingi bilioni 1.87. Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya kuandaa ramani za mipango miji, kulipa fidia, kupima na kumilikisha viwanja. Hadi Juni, 2012, jumla ya Shilingi milioni 650 zimerejeshwa na Shilingi bilioni 1.22 hazijarejeshwa. Halmashauri ambazo bado hazijarejesha ni za Manispaa ya Morogoro (Shilingi milioni 50); Mji wa Kibaha (Shilingi milioni 270.4);

Manispaa ya Kinondoni (Shilingi milioni 500) na Manispaa ya Ilala (Shilingi milioni 400).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) zitaweka utaratibu utakaozilazimisha Halmashauri zilizokopeshwa kurejesha mikopo hiyo kwa wakati. Napenda kuzikumbusha Halmashauri kutumia fursa hii kutambua kwamba kushindwa kurejesha mikopo hiyo kunaathiri utendaji kazi wa Wizara yangu na kuzinyima haki Halmashauri nyingine ambazo zingekopeshwa kama mikopo ingerejeshwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua pia fursa hii kutangaza kuwa nimeagiza kwamba Wizara yangu ikate madeni ya wadaiwa hawa sugu kwenye mgao wao wa asilimia 30 ya makusanyo ya kodi za ardhi kabla ya kuwalipa. Sina budi kuzipongeza Halmashauri za Bagamoyo na Manispaa ya Temeke, kwa kumaliza kulipa madeni yao. Jambo hili nalo si umaskini bali ukosefu wa nidhamu ya kifedha (*financial indiscipline).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mipango Miji na Vijiji, Wizara yangu ina jukumu la kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji ili wananchi wawe na makazi nadhifu na yaliyopangwa. Majukumu hayo yanaratibiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na taratibu za uendelezaji wa miji na vijiji zilizopo zikiwemo Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000, Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

ya mwaka 2007 na Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watu nchini imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kulingana na takwimu ya sensa ya watu ya mwaka 1957; Tanzania Bara ilikuwa na watu 8,788,466 kati yao watu 276,362 sawa na asilimia 3.1 walikuwa wakazi wa mijini. Idadi ya wakazi hao iliongezeka hadi kufikia 679,291 sawa na asilimia 5.7 mwaka 1967 na kufikia watu 7,970,000, sawa na asilimia 23.1 mwaka 2002. Ongezeko hilo la watu limesababisha miji yetu kukua kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama miji yetu itaendelea kukua kwa kasi ya sasa ya asilimia 4.5 kila mwaka, ifikapo mwaka 2025, zaidi ya nusu ya wananchi wote hapa nchini watakuwa wanaishi mijini. Kasi kubwa ya ongezeko la watu mijini imefanya mamlaka za upangaji ambazo ni mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kumudu kupanga, kupima na kuweka miundombinu na huduma za msingi. Hali hii inaonesha kuwa makazi mijini yatakabiliwa na changamoto nyingi, hivyo kuna umuhimu wa kubuni mbinu za kisasa za kupanga na kuendeleza miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Uendelezaji Miji; katika upangaji wa miji, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri huandaa mipango ya jumla *(General Planning Schemes)* ya aina mbili ya kuongoza uendelezaji wake. Mipango hiyo ni ya muda mrefu *(Master Plans)* ambayo hutoa mwongozo wa

uendelezaji kwa miaka ishirini na ya muda mfupi *(Interim Land Use Plans)* ambayo ni ya miaka kumi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi ilikamilisha uandaaji wa Mpango wa muda mfupi wa Mji Mdogo wa Kyaka - Bunazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Tanga ilikamilisha uandaaji wa Mpango kabambe wa Jiji la Tanga na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo iliendelea na maandalizi ya Mpango Kabambe wa Mji wa Bagamoyo. Pia, Mtaalam mshauri anayeandaa Mpango Kabambe wa Jiji la Dar es Salaam aliwasilisha rasimu ya awali ya mpango huo ambao ataukamilisha mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo itakamilisha Mpango Kabambe wa mji mdogo wa Bagamoyo na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mbeya itaandaa Mpango Kabambe wa Jiji hilo. Vile vile, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe katika kuandaa mpango wa Mji Mdogo wa Makambako na Halmashauri ya Wilaya ya Mafia katika ukamilishaji wa Mipango ya miji hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni iliendelea kuandaa mpango wa uendelezaji upya eneo la Manzese na ilikamilisha maandalizi ya mpango wa Makongo Juu na kuanza

maandalizi ya kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Njombe, ilianza uandaaji wa mpango wa uendelezaji upya wa eneo la kati la mji huo. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri hizo kukamilisha na kutekeleza mipango hiyo. Natoa wito kwa Mamlaka zote za Miji na Wilaya nchini kutenga fedha za kuandaa na kutekeleza mipango hiyo ambayo ni msingi wa usimamizi wa uendelezaji wa miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize tu kuwa kugawa viwanja siyo kupanga miji lazima uwe na *master plan*. Kwa hiyo, wale wanaogawa viwanja bila kuwa na *master plan* hao wanataka ugomvi na mimi huko mbele. Kwanza, tunakuwa na *master plan* halafu ndiyo tunagawa viwanja naomba Bunge hili Tukufu liunge mkono katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa uendelezaji upya eneo la Kurasini ulioanza mwaka 2006 na fedha zimetengwa. Kwa sasa tunaamini kwamba tutakamilisha kwa lengo la kuwezesha eneo hilo kutumika kikamilifu kwa upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na kuifanya iwe lango kuu la biashara Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara ililipa fidia ya jumla ya Shilingi milioni 550 kwa wakazi wa Mtaa wa Kurasini na waliopo jirani na mabwawa ya majitaka. Pia, kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi imetayarisha michoro inayoonesha ukanda wa barabara inayounganisha barabara ya

Mandela na daraja la Kigamboni kwa upande wa Kurasini na kutambua ardhi na mali zilizopo katika ukanda huo wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya maandalizi ya eneo la ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Biashara kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya upanuzi wa Bandari Kurasini Jijini Dar es Salaam. Aidha, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imetenga fedha kwenye bajeti ya mwaka 2012/2013 chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi huo katika eneo la Kurasini na Shimo la Udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu urasimishaji makazi holela; katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu ilikamilisha uandaaji wa Programu ya Taifa ya kuzuia na kurasimisha makazi holela na iko katika hatua ya utekelezaji. Pia, kwa kushirikiana na Jiji la Mwanza ilirasimisha makazi 2,810. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni ilihakiki mipango ya urasimishaji 16 katika Mitaa ya Makabe na Mshikamano Kata ya Mbezi Luis na Mitaa ya Malamba Mawili na Msigani. Mipango hiyo iko katika hatua ya kuidhinishwa ili wananchi waweze kupimiwa maeneo yao na kuandaliwa hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, Wizara itachapisha, kusambaza na kuanza utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kuzuia na Kurasimisha Makazi Holela mijini kwa kushirikiana na MKURABITA,

Halmashauri za Miji na Wilaya na wadau wote. Pia itarasimisha makazi 4,000 katika Jiji la Mwanza. Halmashauri zote nchini zinaagizwa zihakikishe kuwa zinapima viwanja na kuvigawa kwa wananchi ili kuepusha ujenzi holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaokaidi mipangomiji na kujenga kiholela, kuvamia maeneo ya wazi na kujenga katika maeneo yanayolindwa kisheria hususan fukwe na maeneo hatarishi, wasitegemee kupewa fidia wakati wa kuhamishwa. Tuko tayari kupokea maombi yenu kupewa viwanja au nyumba kuliko kupoteza akiba yenu kujenga visivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji Miji Mipya na Vituo vya Huduma; katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam katika kutekeleza mkakati wa kuanzisha vituo vya huduma kwenye maeneo ya pembezoni mwa miji kwa kushirikisha sekta binafsi. Kwa upande wa Kituo cha Huduma cha Luguruni, Wizara imekamilisha mchakato wa kupata mwendelezaji mwenza *(Co-Master Developer)* ambaye ni kampuni binafsi itakayoshirikiana na Serikali katika uendelezaji wa kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imeainisha eneo jipya la Mikwambe kwa ajili ya kujenga kituo cha huduma katika Manispaa hiyo badala ya Kongowe. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni itaanza utekelezaji wa ujenzi wa Kituo cha

Huduma cha Luguruni kwa ushirika kati ya Sekta binafsi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango Kabambe wa Mji Mpya wa Kigamboni uliandaliwa kwa kuzingatia Sheria ya Mipangomiji, Sura Na. 8 ya 2007 kama historia yake inavyoonesha. Yafuatayo yalifanyika: Kuitisha mkutano wa wakazi wa Temeke, kutangaza mipaka ya eneo kwenye Gazeti la Serikali, kuandaa andiko na kufanya uhamasishaji katika ngazi zote. Uhamasishaji ngazi ya Mkoa ulifanyika tarehe 2 Desemba, 2008 katika Ukumbi wa Mkuu wa Mkoa. Washiriki katika mkutano huo ni Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri zote za Dar es Salaam na Katibu Tawala wa Wilaya ya Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano katika ngazi ya Wilaya ulifanyika katika Ukumbi wa JKT Mgulani tarehe 11 Januari, 2009 na walihudhuria Wabunge, Madiwani na watendaji wa Wilaya ya Temeke; Mkutano wa kujenga uelewa wa pamoja ulifanyika katika ukumbi wa Manispaa ya Temeke tarehe 14 Januari, 2009 na wadau walitoka Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na viongozi wa Manispaa ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mkutano wa ngazi ya Kata ulifanyika tarehe 16 Januari, 2009 Kigamboni na viongozi wa ngazi ya Kata walishirikishwa; Mikutano katika ngazi ya mitaa ilifanyika kati ya tarehe 18-24 Machi, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 20 Januari, 2009 katika kikao chake cha kawaida, Halmashauri ya

Manispaa ya Temeke ilijadili na kuridhia mpango wa uendelezaji wa mji wa Kigamboni. Tarehe 9 Mei, 2009 kilifanyika kikao cha kutoa taarifa ya kuanza kutambua mali na milki kwenye eneo lote la mpango. Kutokana na maazimio ya kikao hicho kazi ya kutambua mali na milki kwenye eneo la mpango ilianza tarehe 12 Mei, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya milki 32,000 zilitambuliwa katika Kata zote sita za Kigamboni, Mji Mwema, Vijibweni, Kibada, Somangila na Gezaulole. Mtaalam Mwelekezi aliwasilisha mpango katika ngazi zote kama ilivyokuwa awali kati ya tarehe 2 Desemba 2009 hadi 28 Juni, 2010. Tarehe 4 Julai 2010 Waheshimiwa Wabunge walifanyiwa semina kwenye ukumbi wa Pius Msekwa, Dodoma kuhusu mpango wa uendelezaji wa mji mpya wa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, ilikamilisha maandalizi ya msingi ya kuwezesha kutekeleza Mpango Kabambe wa Mji Mpya wa Kigamboni. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara itasimamia uundwaji wa Wakala; Kuidhinisha mpango na kuanza utekelezaji; Kufanya uthamini wa mali zilizomo katika maeneo ya miundombinu, huduma za jamii na eneo la makazi mbadala *(resettlement area);* Kulipa fidia kwa mali zilizomo katika maeneo yaliyofanyiwa uthamini; Kuandaa michoro ya kina; kupima na kuandaa ramani za ujenzi zilizomo katika eneo la makazi mbadala; Kupima maeneo nje ya maeneo ya miundombinu kwa awamu na kuendelea na utekelezaji kwa awamu tatu.

Awamu ya kwanza ni kati ya 2012-2022, awamu ya pili ni kati ya 2022- 2027 na awamu ya tatu ni 2027-2032.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara yangu itaendelea kutafuta fedha za kuendeleza eneo la mpango kwa kuuza *Municipal bonds*. Gharama ya mradi inakisiwa kufikia Shilingi trillion 11.6. Pamoja na kwamba asilimia 59 ya bajeti ya Wizara, takriban bilioni 60, zimetengwa kwa ajili ya Mradi wa Kigamboni, kiasi hiki ni asilimia 10 tu ya pesa zinazohitajika mwaka huu. Kwa hiyo, tutatumia mbinu za kisasa kutafuta pesa nyingine, takribani bilioni 605 nje ya bajeti kutekeleza mradi huu bila kuchelewa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi utahitaji kiasi hicho cha fedha kwa miaka mitatu ya kwanza. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Kigamboni kwa uvumilivu wao na ushirikiano wanaotuonesha na nawahakikishia kuwa Serikali sasa imetenga bajeti ya kuhakikisha utekelezaji wa mpango huu unaanza na kushamiri. Nitasimamia mradi huu kwa karibu, kwa kasi, ari na nguvu mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuanza na ziara za mafunzo *(study tours)* kwa wawakilishi kutoka Kigamboni kutembelea miji mipya ili tuwe na uelewa wa pamoja juu ya kazi iliyo mbele yetu. Aidha, wawekezaji wa ndani na nje ya nchi watapewa maeneo ya kuanza kujenga makazi ambayo yatatumika kuwahamisha wananchi watakaopenda kubaki Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri ikiwezekana wote wachague kubaki maana hivi sasa kuna wananchi takribani 82,000, wakati tunajenga mji mpya wenye uwezo wa wakazi 400,000. Hakuna sababu ya wananchi kuhama eneo hili ila makazi yao yatapangwa upya na kuboreshwa. Serikali imeamua kuunda Wakala mpya, Kigamboni *Development Agency (KDA)* kusimamia mradi huu wa kipekee katika historia ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi ambao hawajakiuka maagizo ya mradi kwa kufanya maendelezo haramu, wasiwe na wasiwasi kuhusu fidia kwa sababu mradi utazingatia haki zao na ni endelevu. Fidia itatolewa kwa mujibu wa sheria, kwa tathmini ya kiujumla ambayo itakokotolewa kutokana na viwango vya soko na kuhuishwa ili iwe sahihi *(land values under mass valuation)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usimamizi wa uendelezaji Miji; katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikamilisha uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Mipangomiji (Na. 8) ya mwaka 2007. Vile vile, Wizara imetafsiri kwa Kiswahili Sheria ya Mipangomiji na rasimu yake inafanyiwa maboresho. Kwa mwaka 2012/2013 Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 2007 na kanuni zake, pamoja na miongozo mbalimbali inayohusiana na masuala ya uendelezaji na upangaji wa ardhi mijini na vijijini ili kurahisisha utekelezaji wake. Aidha, Wizara inakusudia kuanzisha Ofisi za Kanda kwa wataalam wa Mipangomiji kwa lengo la kukasimu

mamlaka ya kuidhinisha Mipango ya Uendelezaji Miji kutoka kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliajiri Askari Ardhi *(Land Rangers)* 15 waliohitimu kutoka Chuo cha Ardhi Tabora na Morogoro kwa mikataba ya muda mfupi. Askari hao walipangwa katika Halmashauri za Manispaa za Jiji la Dar-es-Salaam (Temeke, Kinondoni na Ilala) kwa ajili ya kufanya kazi ya ufuatiliaji wa maendelezo mbalimbali Jijini pamoja na ukaguzi wa matumizi mbalimbali ya ardhi kwenye maeneo yaliyopangwa ili kupunguza kasi ya uvamizi wa maeneo ya wazi na ujenzi holela kwenye maeneo yenye mipango miji. Aidha, Wizara imeandaa muundo wa utumishi wa kada hii na utawasilishwa katika Mamlaka husika kwa ajili ya kuidhinishwa na kuanza kutumika. Nashauri Halmashauri zote ziweke utaratibu wa kuajiri na kuwatumia watumishi wa kada hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Mto Msimbazi ni eneo ambalo lilibainishwa kuwa wazi katika mpango kabambe wa Jiji la Dar es Salaam wa mwaka 1979. Hata hivyo, eneo hilo limeendelezwa kwa matumizi mbalimbali ambayo yanakinzana na mpango huo. Kutokana na uvamizi huo, madhara makubwa hutokea katika eneo hilo. Mfano, mwezi Desemba mwaka 2011 watu walipoteza maisha na mali kutokana na mafuriko katika eneo hilo. Hali hii iliigharimu Serikali fedha nyingi katika kuwaokoa, kuwahifadhi na kuwatafutia makazi wahanga wa mafuriko. Natoa pole kwa waathirika wa mafuriko hayo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa za Ilala na Kinondoni ilianza maandalizi ya mpango wa kuhifadhi Bonde la Mto Msimbazi kuwa eneo la kijani. Eneo hilo linaanzia milima ya Pugu hadi Daraja la Salenda lina hekta 1,924. Mchakato wa kuhifadhi bonde hilo utafanyika kwa awamu mbili, awamu ya kwanza itaanzia kwenye Daraja la Salenda Upanga hadi Vingunguti lenye ukubwa wa hekta 1,121.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili itaanzia Vingunguti hadi milima ya Pugu. Hadi sasa Wizara imebainisha mipaka na kuandaa mchoro wa eneo la mpango na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali (*GN* Na. 227) la tarehe 5 Aprili, 2011. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na Kinondoni zitaendelea na uandaaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza tena kuwa eneo la Bonde la Mto Msimbazi ni eneo hatarishi kwa makazi ya binadamu, hivyo mamlaka za upangaji zichukue hatua za haraka kuondoa makazi na maendelezo yote yaliyofanyika humo kwani hayana mustakabali. Ni dhahiri kwamba maafa ya mara kwa mara katika eneo hilo hayaepukiki hasa ukizingatia mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, naagiza Halmashauri zote kuainisha maeneo yote hatarishi hususan mabonde na milimani na kuyawasilisha kwangu kwa ajili ya kuyatangaza kwenye Gazeti la

Serikali. Natoa wito kwa wadau wote, kutoa ushirikiano unaostahili ili kuhakikisha kuwa zoezi hilo linafanyika kwa manufaa ya wakazi wote wa Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi; Wizara yangu ina jukumu la kusimamia na kuratibu kazi za uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji. Lengo ni kuziwezesha mamlaka za upangaji zikiwemo Halmashauri za Wilaya na Vijiji kupanga, kutekeleza na kufuatilia uendelezaji wa Mipango ya makazi vijijini katika maeneo yao ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hiyo ni nyenzo muhimu katika kuendeleza ardhi na rasilimali zake kwa ufanisi, kuzuia migogoro baina ya watumiaji ardhi, kuimarisha milki za ardhi hususan za kimila, kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji, kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji na kuongeza ustawi wa jamii na maendeleo ya kiuchumi kwa watumiaji wa ardhi ambao wengi wao ni wananchi wa kawaida wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ilitoa mafunzo kuhusu Sheria za Ardhi, matumizi ya teknolojia ya utunzaji wa kumbukumbu *(Geographical Information System*) na mbinu shirikishi za utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Katika kipindi hicho, jumla ya watendaji 51 kutoka Halmashauri za Wilaya 14 za ukanda wa Pwani walipatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ilifanya tathmini ya uwezo wa rasilimali za ardhi ngazi ya Kijiji katika Vijiji 18 vya Wilaya za Pangani, Muheza, Mkinga, Rufiji na Mafia kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Matokeo ya tathmini hiyo ni kufahamika kwa uwezo wa rasilimali ardhi pamoja na vikwazo vinavyoathiri uwezo wa ardhi kwa matumizi mbalimbali endelevu (kama vile kilimo, upandaji wa miti, makazi, viwanda na ufugaji) na kuwezesha kijiji kufanya maamuzi sahihi juu ya mgawanyo na matumizi ya rasilimali ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya na Vijiji; katika mwaka 2011/12, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wadau mbalimbali katika kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi za Vijiji na Wilaya. Katika kipindi hicho mipango ya matumizi ya ardhi iliandaliwa katika Vijiji 82 kwenye Wilaya 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vijiji hivyo, maeneo ya makazi, huduma za jamii, hifadhi za vyanzo vya maji, misitu, ufugaji, wanyamapori, mashamba makubwa na maeneo ya kilimo cha umwagiliaji yametengwa kwa kuwashirikisha wananchi. Vile vile, Wizara iliendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mipango iliyoandaliwa ya vitovu vya vijiji na vituo vya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ilitekeleza ombi la Mkoa wa Tabora la kuandaliwa Mipango ya kina ya makazi ya vijiji vinavyozunguka hifadhi ya misitu kwenye vijiji vinne katika Wilaya ya Urambo. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaandaa taarifa mbalimbali za vijiji nchini ili kuwa na kumbukumbu sahihi zitakazosaidia katika uandaaji wa mipango ya makazi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Tume itatekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi kwa kutayarisha mipango ya matumizi ya ardhi kwa ushirikishwaji katika vijiji 150. Mipango hiyo itaandaliwa katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Rufiji ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya *Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)*. Aidha, vijiji vingine vya mipakani katika wilaya 16 za Tarime, Rorya, Same, Kibondo, Ngara, Misenyi, Longido, Ngorongoro, Rombo, Mwanga, Hai, Momba, Kyerwa, Karagwe, Karambo na Kakonko vitaandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hiyo itaandaliwa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika. Vile vile, itaandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya nne za Mpanda, Chunya, Kilombero na Ulanga na kutoa mafunzo kwa watendaji katika Wilaya hizo kuhusu matakwa ya Sheria za Ardhi na mbinu shirikishi za utayarishaji wa mipango hiyo. Pia, Wizara itaendelea kutekeleza programu za kilimo, maji na mifugo kwa kushirikiana na Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuzipongeza Halmashauri za Wilaya zilizokuwa zimetenga fedha katika mwaka 2011/2012 kwa ajili ya kutayarisha mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi za vijiji ambazo ni Tandahimba, Korogwe, Monduli na Songea Vijijini. Napenda kuendelea kusisitiza umuhimu wa Halmashauri za Wilaya kutenga bajeti kwa ajili ya kupanga mipango ya matumizi ya ardhi ngazi ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya nyumba; upatikanaji wa nyumba bora za bei nafuu kwa wananchi walio wengi ni moja ya kiashirio cha kukukua kwa uchumi na maendeleo ya jamii. Ubora wa mazingira, zikiwemo nyumba unachangia kulinda afya ya jamii na kuongeza uwezo wa kufikiri na kutafakari. Sekta ya nyumba inatoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi, mapato ya Serikali, kuongeza nafasi za ajira na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mchango wa sekta ya nyumba kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Serikali inajielekeza katika kuweka mazingira wezeshi ya uendelezaji wa sekta hii. Changamoto kubwa zinazoikabili sekta ya nyumba ni namna ya kukabili ongezeko katika gharama za ujenzi wa nyumba, upatikanaji wa miundombinu na huduma za jamii katika maeneo ya makazi, upungufu wa nyumba bora na za bei nafuu na riba kubwa katika mikopo ya nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuelekeza na kuhamasisha Serikali za

Mitaa kuratibu na kusimamia upatikanaji wa ardhi na uendelezaji wa miundombinu ili kuwezesha makampuni ya uendelezaji milki na watu binafsi kujenga nyumba na uendelezaji miji kwa namna bora na endelevu. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 tayari baadhi ya Halmashauri zimeanza kuomba mikopo kutoka mabenki kwa ajili ya uendelezaji wa ardhi na kuweka miundombinu. Halmashauri hizo ni pamoja na Temeke na Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa mtaji wa kukopesha kwa muda mrefu, Serikali ilianzisha *Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC)* mwaka 2010, ambayo imeendelea kuvutia uwekezaji wa mabenki zaidi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya mabenki na vyombo vya fedha vimekubali kutoa mikopo kwa wananchi ili kuwawezesha kununua nyumba kwa kutumia mikopo ya muda mrefu hadi kufikia miaka 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuyapongeza mabenki yaliyojitokeza kutoa mikopo kwa ajili ya kuendeleza nyumba. Kwa upande wetu Wizara itaendelea kuboresha mazingira kwa mabenki kutoa mikopo ya kujenga na pia kununua nyumba kwa kuhimiza Wizara ya Fedha na Benki kuu kuunda chombo cha kutoa bima ya mikopo ya nyumba *(housing loans insurance mechanism).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu, kwa kutambua faida za ushirika, inahimiza uanzishwaji na uendelezaji wa Vyama vya Ushirika wa nyumba ili kuwawezesha wananchi hasa wenye kipato cha chini

kupata nyumba bora kwa gharama nafuu. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilikamilisha kuandaa mwongozo wa kuunda na kuendesha Vyama vya Ushirika wa Nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo huo utatumika wakati wa uhamasishaji wa wananchi kuunda Vyama vya Ushirika wa Nyumba. Kwa wananchi wanaofanya kazi za kujiajiri wanashauriwa waanzishe vikundi vya ushirika wa nyumba katika maeneo yao. Chama cha Ushirika wa Nyumba kinaweza kusajiliwa ikiwa idadi ya wanachama waanzilishi inatimia watu kumi (10) au zaidi. Natoa wito kwa waajiri kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika wa nyumba kwenye sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu ilikusanya takwimu za hali ya nyumba katika Miji ya Shinyanga, Musoma, Bukoba, Tabora, Singida, Mtwara, Songea, Lindi, Njombe, Kigoma, Manyara, Rukwa, Bagamoyo na Kibaha. Taarifa zilizopatikana zitaiwezesha Serikali na wadau wengine wakiwemo waendelezaji milki na benki kufanya maamuzi yanayohusu nyumba kwa kuzingatia takwimu za uhakika. Pia, taarifa hizo zitawezesha nchi yetu kupima mafanikio yake Kikanda na Kimataifa katika sekta ya nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya uendelezaji wa nyumba kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu mfumo wa mikopo ya nyumba (*mortgage*

finance) na utaratibu wa kumiliki sehemu ya jengo (*condominium housing);* kuandaa taarifa ya hali ya nyumba nchini na kuhamasisha uundaji wa Vyama vya Ushirika wa Nyumba na waendelezaji milki *(Real Estate Developers)* hasa wanaojenga nyumba za gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imekamilisha maandalizi ya rasimu ya Sera ya Taifa ya Nyumba. Sera hiyo inaweka msingi wa kuongoza na kusimamia uendelezaji wa nyumba. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaratibu ukamilishaji wa Sera ya Nyumba na kutayarisha mpango mkakati na programu ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, itaanza mchakato wa kutunga Sheria ya Nyumba. Sheria itakayotungwa, itaweka utaratibu au kuanzisha chombo kitakachosimamia masuala ya mahusiano kati ya mpangaji na mmiliki wa nyumba na viwango vya ubora wa nyumba za kuuza na kupangisha bila kuathiri motisha wa kujenga nyumba za kupangisha au kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi *(NHBRA)* una jukumu la kutafiti, kukuza, kushauri, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utaalam wa ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu nchini. Kazi hizo zikifanyika kikamilifu zitainua na kuboresha viwango vya nyumba zinazojengwa kwa kutumia vifaa vinavyopatikana hapa nchini na kuinua maisha ya wananchi wanaoishi vijijini na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu kupitia Wakala iliendelea kufanya utafiti na kubuni mbinu za kujenga nyumba kwa gharama nafuu kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini. Utafiti ulifanyika ndani na nje ya maabara. Vile vile, kazi za ushauri zilifanyika kwa wateja mbalimbali zikiwemo Ofisi za Serikali na watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 mafunzo ya vitendo yalifanyika kwa vijana 380 kutoka katika Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Pwani. Mafunzo hayo yaliwezesha kuanzishwa kwa vikundi 38 vya ujenzi wa nyumba na uzalishaji wa vifaa vya ujenzi na vilipatiwa mashine 114 za kufyatulia matofali yanayofungamana na mashine 28 za kutengenezea vigae vya kuezekea pamoja na kalibu za vigae 1,400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mashine za uzalishaji wa vifaa vya ujenzi zilisambazwa katika maeneo mbalimbali nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa teknolojia ya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu inawafikia wananchi walio wengi. Wakala ulijitangaza kwa kutumia vyombo vya habari na maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kueneza matokeo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, semina za uhamasishaji na kueneza teknolojia za ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu zitafanyika katika Wilaya za Arusha Vijijini, Nkasi, Kishapu, Chunya, Tandahimba na Muleba. Pia, Wizara itafanya uhamasishaji wa kuanzisha vikundi vya ushirika vya

ujenzi na uzalishaji wa vifaa vya ujenzi na kuvitumia katika ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya itaimarisha vikundi vya ujenzi wa nyumba vilivyoanzishwa na itaendelea kutangaza huduma zinazotolewa kupitia vyombo ya habari kama televisheni, vipeperushi na magazeti na kwa kushiriki katika maonesho ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala itaendelea kutoa huduma ya upimaji wa ubora wa vifaa mbalimbali vya ujenzi kutoka kwa wateja kwa kutumia maabara katika maeneo ya ujenzi. Pia, ushauri wa kitaalam wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu utaendelea kutolewa kwa wateja. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuzishauri na kuzihamasisha Halmashauri za Majiji, Miji na Wilaya zitumie huduma za Wakala kwa kazi za ujenzi wa majengo yao na ya Serikali ili wanufaike na huduma za Wakala ambazo ni za gharama nafuu ikilinganishwa na bei za soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazishauri Idara za Serikali na Taasisi za Umma zitoe kipaumbele kwa matumizi ya teknolojia iliyobuniwa na Wakala ili kupunguza gharama za usanifu na ujenzi wa nyumba na majengo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha utendaji kazi wa Shirika la Nyumba la Taifa katika mwaka 2011/2012. Shirika la Nyumba la Taifa liliendelea na

utekelezaji wa mpango mkakati wa kipindi cha miaka mitano (2010/2011-2014/2015). Kulingana na malengo ya mpango huu, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa, iliimarisha ufanisi wa utendaji kazi kwa kuweka mfumo wa tathmini na ufuatiliaji na kuboresha utendaji wao; kuwapatia mafunzo wafanyakazi 535 kati ya 546 kuhusu mbinu za utendaji wa kisasa na kuingia mikataba ya kiutendaji; kufuta mikataba ya ubia 59 isiyokuwa na tija kwa Shirika na kurekebisha mikataba 311 kati ya Shirika na wadau wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Wizara iliendelea na zoezi la kuhuisha mikataba ya pango katika nyumba zake; kuanzisha kitengo cha huduma kwa wateja; kurekebisha miongozo ya Shirika; kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha na mali za Shirika; kuanzisha mfumo mpya wa mawasiliano ya kompyuta hasa utambuzi wa kijiografia wa nyumba za Shirika na kupunguza kesi zilizoko Mahakamani kutoka 288 na kufikia 167. Juhudi hizi zimeliwezesha Shirika kuongeza ufanisi katika utendaji na kuboresha taswira yake kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ardhi kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba; katika mwaka 2011/2012, Shirika limeanza utekelezaji wa jukumu la kuwa Mwendelezaji Mkuu (*Master Developer).* Katika kutekeleza jukumu hili, Shirika lilinunua ardhi yenye ukubwa wa ekari 1,372.1 katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Lengo la ununuzi huu, ni kuongeza hazina ya ardhi. Vilevile, ununuzi wa maeneo mengine yenye ukubwa wa ekari 26,887.9 katika Wilaya

mbalimbali nchini uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za upatikanaji wa ardhi zinafanyika sambamba na upangaji wa maeneo; upimaji; utayarishaji wa michoro ya kiusanifu na kiufundi na upatikanaji wa vibali mbalimbali kama vile vya mazingira, ujenzi na motisha za uwekezaji kutoka Kituo cha Uwekezaji cha Taifa *(TIC)*. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa itaendelea na ununuzi wa vipande vya ardhi vilivyotambuliwa katika maeneo mbalimbali nchini. Natoa wito kwa Halmashauri za Miji na Wilaya kutenga ardhi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa pamoja *(Real estate)* utakaofanywa na Shirika la Nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa nyumba za biashara na makazi. Katika mwaka 2011/2012, Shirika liliendelea na matayarisho ya miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi na biashara 9,000 katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya nyumba hizo, ujenzi wa nyumba 1,620 ulikamilika. Miradi iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa iko katika maeneo mbalimbali nchini zikiwemo Wilaya mpya ambazo ni Mvomero, Kongwa, Longido na Ilembo – Mpanda. Kwa mwaka 2012/2013, Shirika litaendelea utekelezaji wa ujenzi wa nyumba 7,380 katika Wilaya mbalimbali nchini ikiwemo Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Shirika liliendelea na utekelezaji wa miradi kumi ya ujenzi yenye jumla ya nyumba za makazi 823 katika

maeneo mbalimbali nchini. Kati ya miradi hiyo, mitatu yenye jumla ya nyumba za kuuza 86 ilikamilika. Shirika pia liliweza kukamilisha mradi wa jengo la biashara lenye ghorofa nne lililoko Mtaa wa Lumumba mjini Kigoma. Kwa mwaka 2012/2013, Shirika litakamilisha miradi saba yenye nyumba 737 na miradi mipya 38 yenye jumla ya nyumba 4,114 ikiwa ni jumla ya miradi 45 yenye nyumba 4,877. Kwa kuwa Shirika lipo tayari kujenga nyumba katika sehemu mbalimbali nchini, ni vyema Halmashauri zitakazohusishwa, zikalitengea ardhi kulingana na mahitaji. Pia, Shirika litaanza utekelezaji wa miradi mingine 14 ya majengo ya biashara katika maeneo mbalimbali nchini

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, ililiruhusu Shirika kukopa kiasi cha Shilingi bilioni 300 kutoka kwenye vyombo vya fedha vya ndani na nje ya nchi. Kutokana na kibali hicho, benki 15 za ndani na nje ya nchi zilikubali kulikopesha Shirika kiasi hicho. Hadi Juni, 2012 Shirika liliingia mikataba na benki tisa (9) zilizokubali kutoa mikopo ya jumla ya Shilingi bilioni 165.4. Fedha hizi zinatumika kwa ajili ya kuongeza hazina ya ardhi na kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba. Sambamba na juhudi hizi, Shirika pia liliingia makubaliano na benki tisa (9) kwa ajili ya kuwakopesha wanunuzi wa nyumba zinazojengwa na Shirika. Benki hizo ni *Azania Bank, Bank of Africa (BOA), Commercial Bank of Africa* (*CBA*), Benki ya *CRDB, Exim Bank*, Kenya *Commercial Bank (KBC*), Benki ya *NBC*, Benki ya *NMB* na *Stanbic*. Benki hizi zimeanza kutoa mikopo kwa wanunuzi wa nyumba zinazojengwa na Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa itaendelea kuzihamasisha benki nyingine kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na kuwahamasisha wananchi kununua nyumba zinazojengwa na Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa za ununuzi wa ardhi; upatikanaji wa vibali vya ujenzi na gharama za uwekezaji kwenye miundombinu, ni kati ya changamoto zinazolikabili Shirika la Nyumba la Taifa katika suala zima la ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya kutatua changamoto hizi ili kuliwezesha Shirika hili kuharakisha utekelezaji wa miradi yake na kupunguza gharama. Natoa wito kwa taasisi zinazohusika na uendelezaji wa sekta ya nyumba hususani Halmashauri za Miji na Manispaa pamoja na mamlaka za huduma za maji na umeme, kutoa huduma zinazowahusu ili kuliwezesha Shirika kutekeleza miradi yake kwa ufanisi na kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Shirika lilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 43.14 kutokana na kodi za pango la nyumba linazozimiliki. Hadi Juni, 2012, Shirika lilikusanya jumla ya Shilingi bilioni 53.17 sawa na asilimia 123 ya lengo**.** Ongezeko hili, linatokana na kuongezwa kwa viwango vya kodi kwa baadhi ya nyumba kutoka wastani wa asilimia 25 ya kodi za soko hadi asilimia 60. Pia, ongezeko la makusanyo linatokana na ukusanyaji wa kodi na malimbikizo ya madeni kwa kila mwezi. Pia, Shirika

lilichangia jumla ya Shilingi bilioni 11.47 kwenye pato la Serikali kutokana na kulipa kodi mbalimbali kutokana na shughuli zake. Kwa mwaka 2012/2013, Shirika linatarajia kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 52.97 kutokana na kodi ya pango la nyumba zake na kuchangia mapato ya Serikali jumla ya Shilingi bilioni 24.2 kwa kulipa kodi ya pango la ardhi, kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Shirika lilitenga kiasi cha Shilingi bilioni 6.8 kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya nyumba zake 16,324 zilizoko kwenye majengo yake 2,392. Katika kipindi hicho, jumla ya nyumba 1,400 na majengo 140 yalifanyiwa matengenezo ya kawaida na makubwa. Kwa mwaka 2012/13, Shirika litaendelea kutenga jumla ya Shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo nyumba na majengo ya Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa Shirikika la Nyumba la Taifa, Ndungu Nehemia Kyando Mchechu na timu yake kwa kufanikiwa kubadilisha sura ya Shirika la Nyumba kwa muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingi zimejitokeza katika kuleta mabadiliko hayo lakini ubunifu na bidii inayoshuhudiwa, unaridhisha na kuashiria mageuzi makubwa zaidi hasa kama mikopo ya benki iliyochukuliwa italipwa kama ilivyopangwa na kukomesha ukata uliotishia uhai wa Shirika kabla ya mageuzi haya. Bila kuingilia menejimenti ya siku hadi siku, Wizara inasimamia kwa karibu masuala ya kisera

ikiwemo kuanzisha utaratibu wa kuwapunguzia kodi wale ambao kwa sababu za msingi watashindwa kulipa kodi mpya za pango la Nyumba za Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kisheria. Wizara yangu ilianzisha Kitengo cha Sheria *(Legal Services Unit)* kwa lengo la kutoa huduma mbalimbali za kisheria katika Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Huduma za Kisheria zinajumuisha uhuishaji wa sheria na usimamizi wa mashauri yanayohusu Wizara. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikamilisha marejeo ya Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007 na kuiwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili iandaliwe Muswada wa Sheria. Vilevile, rasimu ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334), Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 117) na Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika (Sura ya 210) ziliandaliwa ili ziendane na mabadiliko ya sera na sheria nyingine za sekta ya ardhi. Aidha, Rasimu ya Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini iliandaliwa na inaboreshwa kwa kuzingatia maoni ya wadau na Kamati ya Wataalam iliundwa ili ipitie upya na kupendekeza marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 na Sheria ya Mahakama za Ardhi ya mwaka 2002 ambayo yataziwezesha kukidhi changamoto zilizojitokeza katika sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itakamilisha marejeo ya Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007; Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334); Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya

117); na Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika (Sura ya 210). Pia itakamilisha Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini na kuendelea kuzifanyia mapitio Sheria za Ardhi ili ziendane na matakwa ya wadau. Natoa wito kwa wadau wa sekta ya ardhi kutoa maoni yao mara watakaposhirikishwa ili kuboresha sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano Serikalini. Wizara yangu inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia vyombo vya habari: redio, *televisioni* na magazeti, ilitoa elimu kwa umma kuhusu huduma zake, sera, mikakati, sheria na kanuni. Kadhalika ilitoa machapisho mbalimbali na kuyasambaza wakati wa maonesho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuimarisha Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kwa kuajiri wataalam wa mawasiliano na kuongeza vitendea kazi. Wizara itahuisha Mkakati wa Mawasiliano *(Communication Strategy)* kwa kupanua ushirikishaji wa wadau wa sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za utawala na rasilimali watu. Wizara yangu iliendelea kuboresha na kusimamia rasilimali watu kwa kutoa mafunzo kwa watumishi, kuboresha mazingira ya kazi na kutoa vitendea kazi, kuwapatia watumishi stahili zinazoendana na ajira zao, kusimamia nidhamu ya watumishi, kusisitiza kuhusu utawala bora, kupiga vita rushwa na kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kuwawezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika kipindi hicho jumla ya watumishi 190 walipandishwa vyeo na watano (5) walithibitishwa kazini. Aidha, watumishi 586 walihudhuria mafunzo mbalimbali kama ifuatavyo:- Mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi watumishi 60, mafunzo yaliyohusu maadili katika utumishi wa umma watumishi 206, mafunzo elekezi ya awali kwa waajiriwa wapya 106 na mafunzo kuhusu utunzaji wa siri na nyaraka za serikali kwa watumishi 214 Kwa mwaka 2012/2013, Wizara inatarajia kuwapatia mafunzo watumishi 400 katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara yangu iliendelea na ujenzi wa kituo cha huduma kwa mteja *(customer service centre)* Makao Makuu ya Wizara. Kazi hii ipo katika hatua za mwisho kukamilika. Kituo hiki kitawezesha mteja kupata huduma za ardhi sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa michezo kwa afya za watumishi, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu ilishiriki katika mashindano ya SHIMIWI na kufanikiwa kupata ushindi wa pili katika mpira wa pete na ushindi wa tatu katika mpira wa miguu. Wizara ilizawadiwa vikombe na medali. Aidha, Wizara imeendelea kuelimisha watumishi juu ya namna ya kujihadhari na UKIMWI na kuhamasisha watumishi kupima afya zao. Watumishi waliojitambulisha kuwa wanaishi na virusi vya UKIMWI wameendelea kupatiwa huduma na msaada wa fedha kwa ajili ya dawa na lishe. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea

kushiriki katika michezo na kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI na kuendelea kuhamasisha upimaji wa afya za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Ardhi; Wizara yangu inasimamia Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya Stashahada *(Ordinary Diploma*) katika fani za urasimu ramani na upimaji ardhi na Cheti (*Certificate*) katika fani za umiliki ardhi, uthamini na uchapaji ramani. Fani zinazofundishwa katika vyuo hivi zinakidhi mahitaji ya soko la wataalam wa sekta ya ardhi. Katika mwaka 2011/2012, walihitimu wanafunzi 153. Kati ya hao, 92 walitoka Chuo cha Ardhi Morogoro na 61 walitoka Chuo cha Ardhi Tabora. Kati ya wahitimu hao, wanawake ni 31 na wanaume ni 122. Naomba nisisitize kuwa Halmashauri ziajiri wataalam hawa ili kuziba pengo la ajira lililopo katika maeneo yao. Wataalam wanaohitimu katika vyuo hivi ndio wanaofanya kazi uwandani (*field work*). Sioni sababu ya baadhi ya Halmashauri kutokuwa na watumishi wakati vyuo vyetu vinatoa wataalam kila mwaka. Kwa hiyo, natoa kauli kabisa kwamba kada hii ya utendaji naomba iajiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara imekamilisha ujenzi wa bweni la wavulana katika Chuo cha Ardhi Tabora ikiwa ni hatua muhimu katika kuongeza udahili na kuboresha huduma ya malazi kwa wanafunzi. Kutokana na kukamilika kwa ujenzi wa bweni hili, mwaka 2012/2013, Wizara itaongeza idadi ya wanafunzi watakaodahiliwa katika Chuo cha Ardhi Tabora. Pia, vyuo hivi vitaandaa na kutekeleza mpango wa mafunzo ya muda mfupi kwa

wataalam wa sekta ya ardhi katika Halmashauri zote nchini kwa lengo la kuboresha utaalam wao. Mafunzo hayo yatatolewa kwa wataalam walioko katika taasisi za umma na sekta binafsi kwa kuwasilisha maombi. Natoa wito kwa taasisi za umma hasa Halmashauri kutumia fursa hii kuwapeleka wataalam wao kujifunza ili waende sanjari na mabadiliko ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani; Wizara yangu ina majukumu mengi na yanayogusa moja kwa moja Watanzania wote. Ni mategemeo yangu kwamba, Bunge litaendelea kuwa na mtizamo chanya na kuipa kipaumbele sekta ya ardhi kwa ujumla ili kuiwezesha kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyofikiwa na Wizara yangu ni kutokana na kuwepo kwa ushirikiano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo zikiwemo taasisi za fedha za kimataifa, nchi wahisani, taasisi zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini. Wadau hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (*UN-HABITAT),* Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*) na Serikali za Denmark, Sweden, Uholanzi na Uingereza kupitia Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara *(Business Environment Strengthening for Tanzania)* na Serikali za Finland na Norway. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine, napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mbunge, kwa kunisaidia katika

kutekeleza majukumu yangu. Pia napenda kumshukuru Katibu Mkuu, Bwana Patrick Rutabanzibwa na Naibu Katibu Mkuu, Bibi Maria Bilia kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Makamishna Wasaidizi na Wasajili Wasaidizi wa Kanda, viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na wataalamu wote wa sekta ya ardhi kwa kunisaidia katika kutimiza majukumu yangu kwa ufanisi. Naomba waendelee kutekeleza majukumu yetu kwa kujielekeza katika kuiwezesha ardhi kuwaondolea wananchi umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa Wizara yangu haina nyenzo na rasilimali za kutosha kutimiza matarajio ya Watanzania, lakini hata kwa kutumia rasilimali chache zilizopo kwa uangalifu tutatoa mchango mkubwa kwa Taifa. Mwisho, namshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa uchapisha Hotuba hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu imeazimia kutekeleza mipango ya kuendeleza ardhi, nyumba na makazi ili kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye kaulimbiu ya Kilimo Kwanza na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016). Aidha, mbali na kuunda Wakala wa Kuendeleza Mji Mpya wa Kigamboni (KDA), Serikali itakamilisha uanzishaji wa chombo kitakachosimamia utoaji wa ardhi kwa wawekezaji kwa utaratibu mpya wa wananchi kutumia ardhi kama mtaji *(land for equity*). Vilevile, itahakikisha kuwa migogoro ya ardhi inayoendelea kujitokeza

inatafutiwa ufumbuzi na kuzuia migogoro mingine isitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, Wizara yangu imejipanga kutayarisha mipango ya kuendeleza miji na vijiji na kuisimamia, kupanga matumizi ya ardhi, kupima ardhi, kuhakiki milki, kusajili na kutoa hati ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa milki. Natoa rai kwa mamlaka na asasi mbalimbali kutoa ushirikiano unaotakiwa kuhakikisha kuwa ardhi inaziwezesha sekta zote ili kufikia malengo ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2012/2013; Wizara yangu imejipanga kutekeleza majukumu yake iliyojiwekea ili kufikia malengo ya MKUKUTA II, Dira ya Taifa ya 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 na Malengo ya Milenia. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi kama ifuatavyo:-

(i) Mapato

Mapato ya Serikali Sh.99,816,438,480

(ii) Matumizi ya Kawaida

Matumizi ya Mishahara Sh.10,422,891,000

Matumizi Mengineyo (OC)
Sh.20,308,831,000
Jumla
Sh.30,731,722,000

(iii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

Fedha za Ndani
Sh.61,000,000,000
Fedha za Nje
Sh.10,000,000,000
Jumla
Sh.71,000,000,000

Jumla ya Matumizi ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni Shilingi 101,731,722,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara *www.ardhi.go.tz*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, hoja imeungwa mkono. Sasa naomba kumwita Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuweza kunipa fursa hii leo kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kusoma taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kama tulivyowasilisha asubuhi hapa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kumpa pole Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Lembeli kwa kufiwa na kaka yake, Bwana Victor Mlindwa ambaye leo anaelekea mazikoni na Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, naomba kuliaribu Bunge lako kwamba Mafia sasa hivi meli ya *LCT Sahara Two,* inaungua na hakuna vifaa vya kuzimia, meli inatetekea. Kwa hiyo, naomba sana mliangalie, watu tuliopo Visiwani tunapata athari kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114(11) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na maoni ya Kamati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 6/6/2012, Kamati ilikutana Jijini Dar es salaam, kwa lengo la kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka huu wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao hicho, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Profesa Anna K. Tibaijuka, Mbunge, aliongozana na Katibu Mkuu, Ndugu Patrick Rutabanzibwa na Watendaji Wakuu wa Wizara. Pamoja na majukumu ya Wizara, Mheshimiwa Waziri alieleza Dira na Dhima ya Wizara na masuala yaliyotekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 20 11/2012 na maombi ya fedha kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao hicho, Kamati ilipitia mambo yafuatayo:-

(i) Taarifa ya utekelezaji wa Kazi za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013;

(ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Shirika la Nyumba la Taifa katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Mpango wa Kazi za Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013;

(iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Mpango wa Kazi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013; na

(iv) Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Mpango wa Kazi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa majadiliano ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya Ushauri ulizingatiwa na kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na:-

(i) Serikali iipatie Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi *retention* ya asilimia 100 badala ya asilimia 71, Serikali iliridhia agizo hili la Kamati na lilianza kutekelezwa mwezi Januari 2012. Tunaishukuru sana Serikali.

(ii) Kitengo cha mawasiliano ya Serikali kipatiwe fedha za kutosha ili kuweza kutekeleza majukumu yake, Kitengo hiki kimewezeshwa kwa kuongezewa mtumishi na kupatiwa kifungu (*subvote*) na kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kimetengewa jumla ya shilingi milioni 200.

(iii) Malipo ya fidia yatakayotokana na uthamini wa mpango wa uendelezaji wa Mji wa Kigamboni yaendane na viwango vya soko vya thamani ya ardhi, nyumba na mazao, ukusanyaji wa takwimu kwa lengo la kuhuisha viwango vya fidia ya ardhi na mali ili viendane na thamani ya soko Kigamboni umefanyika na majadiliano yapo katika hatua za mwisho.

(iv) Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya upembuzi yakinifu wa kubaini uwezo wa wawekezaji kabla ya kumpatia ardhi mwekezaji, Wizara hizi mbili kwa kushirikiana na wadau wengine wako katika hatua za kuanzisha Mamlaka itakayosimamia maendeleo ya ardhi ikiwa ni pamoja na kubaini uwezo wa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo pamoja na utekelezaji wa maagizo hayo ya Kamati, Kamati imesikitishwa na Wizara kushindwa kutoa gawio la asilimia 30 kwenye Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya kulingana na kiasi cha pesa kilichokusanywa. Hii inatokana na Serikali kutokutoa *retention* ya asilimia 100 kwa wakati kama ilivyoridhia. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, hadi kufikia mwezi Mei, 2012 Wizara ilikusanya shilingi bilioni 16 na hadi Mei 2012, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 9.4 tu kutoka Hazina sawa na asilimia 59 ya kiasi kilichokusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012 - mafanikio na changamoto. Mafanikio. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya

Makazi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 47,895,198,000/= kati ya fedha hizo shilingi 25,884,761,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 22,010,437,000/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha hizo zimeweza kuisaidia Wizara kutekeleza majukumu mbalimbali ya mafanikio kama vile andiko la kuomba nyongeza nje ya Ukanda wa kiuchumi Baharini kuwasilishwa Umoja wa Mataifa na kupokelewa, mipango ya matumizi ya ardhi iliandaliwa katika vijiji 76 katika Wilaya mbalimbali nchini, kupima mipaka ya vijiji 150 katika Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo zinazoikabili sekta ya ardhi:-

(i) Kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya watu kuliko uwezo wa Serikali wa kupanga, kupima na kugawa ardhi na kusimamia uendelezaji wake;

(ii) Asilimia 90 ya ardhi nchini haijapimwa na kumilikishwa rasmi hivyo kuchangia kuongezeka kwa migogoro mingi ya ardhi na kuchelewa kutolewa ardhi kwa ajili ya uwekezaji;

(iii) Kukosekana kwa mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi nchini kwani asilimia 90 ya ardhi nchini haijaandaliwa mipango hiyo;

(iv) Upungufu mkubwa wa wataalamu wa masuala ya ardhi hasa katika Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya;

(v) Uhaba wa vitendea kazi hususan vifaa vya upimaji wa ardhi na ukosefu wa Ofisi katika Halmashauri;

(vi) Halmashauri kutengewa fedha kidogo kwa ajili ya shughuli za sekta ya ardhi;

(vii) Uelewa mdogo wa Sheria, Kanuni na Sera za Ardhi kwa wananchi na watumishi hasa katika ngazi ya Halmashauri;

(viii) Kuongezeka kwa migogoro ya ardhi; na

(ix) Ufinyu wa bajeti unaokwamisha Wizara kutekeleza mikakati iliyojipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na jitihada za Wizara katika kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuanzisha Mfuko wa Kulipa Fidia utakaowezesha utwaaji na upimaji wa ardhi kwa ufanisi;

(ii) Kukamilisha usimikaji wa alama za rejea kwa ajili ya upimaji na kununua vifaaa vya upimaji kwa ajili ya Halmashauri zote nchini;

(iii) Kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa lengo la kuziwesha

Halmashauri kuajiri watumishi wa sekta ya ardhi wenye sifa moja kwa moja kutoka vyuoni;

(iv) Kuendelea kutoa elimu kwa umma na kwa watumishi kuhusu Sera na Sheria za Sekta ya Ardhi;

(v) Kuimarisha utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi katika ngazi za Vijiji na Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika ngazi za Wilaya; na

(vi) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Wizara kusimamia mikakati yote iliyojiwekea ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta maendeleo kwa Taifa kwani ardhi ndio msingi wa maendeleo kwa watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2012/2013 pamoja na kazi zilizopangwa kutekelezwa. Ili Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2012/2013, inaomba Bunge lako liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kiasi cha Sh.101, 731,722,000/=. Katika fedha hizo, Wizara inakusudia kukusanya kiasi cha Sh.99,816,438,480/= kama Mapato ya Serikali; Sh.10,422,891,000/= kwa ajili ya matumizi ya mishahara; na Sh.20,308,831,000/= kwa matumizi mengineyo. Kwa Miradi ya Maendeleo, Wizara imepanga kutumia jumla ya Sh.71,000,000,000/= kati ya hizo, fedha za ndani ya

nchi ni Sh.61,000,000,000/= na fedha za nje ni Sh.10,000,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, fedha inayoombwa pamoja na kazi nyingine itatumika kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Wizara ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kutambua upitishaji wa miundombinu eneo la mpango wa kuendeleza upya eneo la Kigamboni kwa Kujenga Mji Mpya (Kigamboni *New City*);

(ii) Kuboresha maabara na karakana za utafiti wa vifaa vya ujenzi;

(iii) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi kwa kutayarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa ushirikishwaji katika vijiji 100 vya mfano;

(iv) Kuvijengea uwezo vyuo vya ardhi vya Tabora na Morogoro;

(v) Kuanzisha na kusimika mfumo wa pamoja wa kutunza kumbukumbu; na

(vi) Kutambua na kupima mipaka kati ya Wilaya na Wilaya yenye mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya Kamati kupitia makadirio ya bajeti Fungu 48, kifungu kwa kifungu na mwelekeo wa kazi za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kamati ina mapendekezo, maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia Serikali ya Tanzania kuandaa Andiko la Kuomba Eneo la Nyongeza Nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini na kuliwasilisha Umoja wa Mataifa, Kamati inapenda kuishauri Serikali kufuatilia kwa karibu Umoja wa Mataifa kwa hatua za mwisho za andiko. Pamoja na hayo, Kamati inapenda kuitambua Kamati ya Wataalamu iliyoandaa andiko hilo kwa kuwataja wajumbe kwa majina ambao ni:-

i. Profesa Evelyne I. Mbede- Mwenyekiti;
ii. Ndugu Pandu S. Makame- Mwenyekiti Mwenza;
iii. Ndugu Justo N. Lyamuya- Katibu;
iv. Ndugu Abdon D. Makishe- Naibu Katibu;
v. Ndugu John A. Msemwa- Mjumbe;
vi. Ndugu Kelvin R. Komba- Mjumbe;
vii. Ndugu Omary S. Mtunguja- Mjumbe;
viii. Profesa Desiderius C.P. Masalu- Mjumbe;
ix. Ndugu Adam I. Zuberi- Mjumbe;
x. Ndugu Issa A. Hemed- Mjumbe;
xi. Ndugu Donald L. Chidowu- Mjumbe; na
xii. Ndugu Richard A. Maridadi- Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 26, Mei 2012, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wataalamu hawa na kujulishwa faida za kuongeza eneo nje ya ukanda wa kiuchumi baharini. Faida hizo ni pamoja na eneo la nchi kuongezeka kwa takriban kilometa za mraba 61,000; haki ya kuvuna rasilimali zinazopatikana katika eneo la nyongeza; kudhibiti uchafu wa mazingira na maliasili ndani ya bahari; kujikinga na maharamia; na kuongeza pato la nchi kutokana na

shughuli za kiuchumi zitakazofanyika ndani ya eneo linalodaiwa. Kwa hiyo, naomba mfahamu kwamba suala hili lina faida kubwa sana kwa nchi. Naishukuru sana na kuwapongeza watalaam hao kwa niaba ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na umuhimu wa eneo la ziada linaloombwa, Serikali haikutenga bajeti kwa ajili ya kuendesha mradi huu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 wala 2012/2013 na hivyo Kamati ya wataalamu kutegemea fedha za wahisani tu. Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa, kwa kuzingatia umuhimu wa suala hili, ni vema Serikali ikatenga fedha za ndani kwa ajili ya mradi huu kwani faida zake zinaonekana wazi kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2012/2013, Serikali imeonesha juhudi za wazi za kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Wizara hii. Kati ya fedha za ndani zilizotengwa, Sh.60,600,000,000/= ni kwa ajili ya kufanikisha hatua za awali za matayarisho ya ujenzi wa Mji Mpya wa Kigamboni (Kigamboni *New City).* Kamati inaishauri Serikali kuanza utekelezaji wa hatua za awali za mradi huu mara moja, hongereni sana Serikali na wananchi wa Kigamboni pamoja na Mbunge wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka utaratibu kwa Wizara kupeleka makusanyo yake ya maduhuli Hazina na kisha fedha hizo kurudishwa Wizarani kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Wakati Kamati inapitia bajeti ya Wizara hii iligundua kwamba

Serikali kupitia Hazina imekuwa haitoi fedha hizo kama ilivyokubaliwa. Hivyo Kamati inashauri ni vyema utaratibu wa makusanyo ya maduhuli *(retention scheme)* ukaangaliwa upya na ikiwezekana ubadilishwe ili Wizara ibaki na makusanyo yake *(retention at source)* na fedha za ziada ndio zipelekwa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kwa kufanya hivyo, shughuli za msingi za Wizara zitatekelezeka ikiwa ni pamoja na Halmashauri kupata gawio la asilimia 30 kwa wakati na hivyo kuweza kutekeleza majukumu yao ya msingi ikiwa ni pamoja na kuziwezesha kukusanya tozo za ada mbalimbali kwa niaba ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa makazi nchini unaongozwa na Sera ya Makazi ya Taifa pamoja na Sheria ya Mipango Miji, Sheria Na. 8 ya Mwaka 2007. Kwa miongozo hiyo, shughuli zote za uendelezaji wa makazi zinasimamiwa na Halmashauri husika za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji kwa niaba ya Waziri mwenye dhamana ya Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ujenzi holela wa majengo mbalimbali unaondelea hasa katika maeneo ya mijini na hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na Halmashauri za Wilaya kushindwa kudhibiti tatizo la ujenzi holela. Kamati inazitaka Halmashauri zote kufuata Sheria ya Mipango Miji ili kupunguza matatizo yanayosababishwa na ujenzi holela ikiwa ni pamoja na mafuriko, milipuko ya magonjwa na kadhalika na watumishi wote

wanaoruhusu ujenzi huu na wenye majengo hayo kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uvamizi wa maeneo ya wazi katika maeneo mbalimbali nchini ambapo maeneo hayo ni kwa ajili ya michezo ya watoto, masoko na shughuli nyingine za maendeleo. Kamati inaitaka Serikali pamoja na Halmashauri zote kuhakikisha maeneo ya wazi yote yaliyovamiwa yanaachwa wazi kwa mfano eneo la wazi la Kitalu D, *Registered Plan Number* 8750, mtaa wa Mikumi na Makongoro iliyopo Magomeni Lango la Jiji; tunaomba sana Serikali ilisimamie eneo hili na hawa watu waondoke mara moja bila ya kujali wao ni nani au ni nani anayekaa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa limekuwa likiidai Serikali na Taasisi zake kodi za pango kwa muda mrefu sasa. Hadi kufikia Juni 2012, Serikali imekuwa ikidaiwa na Shirika kiasi cha shilingi bilioni 2.4. Kamati inaendelea kuitaka Serikali kulipa madeni yake yote kwani yanalinyima Shirika uwezo wa kujenga nyumba nyingine na kujiendeleza kwa ujumla. Wizara zinazoongoza kwa madeni ni pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (Sh.752,525,714) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Sh.471,817, 739) na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na utaratibu wa Serikali kuhamisha miliki ya nyumba za Shirika la Nyumba kwenda Idara nyingine za Serikali kama Wakala wa Majengo *(TBA)* pamoja na Serikali za Mitaa

na uzoefu umeonyesha kuwa baada ya nyumba hizo kuhamishiwa katika Idara hizo, nyumba hizo zimekuwa zikiuzwa. Jambo hili limekuwa likilipunguzia kipato Shirika ambalo linatakiwa kujiendesha lenyewe kibiashara. Aidha, utaratibu huu unaifanya Serikali ionekane machoni mwa Watanzania kuwa si wa kiuungwana na wa kumnyang'anya mtoto kile ambacho Serikali yenyewe ilimmilikisha. Kamati inasisitiza kuwa majengo yote yanayotumiwa na Serikali na Taasisi zake ambayo ni mali ya Shirika la Nyumba yaendelee kuwa chini ya Shirika ili kuliwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi. Majengo yaliyokodishwa na Serikali yanaliingizia Shirika jumla ya Sh. 208,047,274/= kwa mwezi na kwa mwaka Sh.2,496,597,288/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipowasilisha Bungeni taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kamati kwa mwaka 2011/ 2012, iliongelea suala la kuwepo kwa madai ya baadhi ya wapangaji wa Shirika la Nyumba kutaka kuuziwa baadhi ya nyumba za Shirika. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa haitakubaliana na utaratibu wa kuuza nyumba za Shirika zilizoko sasa kwa kuwa nyumba hizo ni mali ya Watanzania wote, hakuna nyumba itakayouzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inalishauri Shirika la Nyumba kuendeleza juhudi zake katika ujenzi wa nyumba mpya 15,000 ambazo asilimia 70 zitauzwa kwa wananchi na asilimia 30 zitapangishwa. Hivyo, Kamati inawashauri wapangaji wa Shirika kujipanga kununua nyumba mpya zinazojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kuwa sehemu kubwa ya nyumba za Shirika zipo katika maeneo mazuri ambayo thamani ya ardhi ni kubwa kuliko thamani ya nyumba pale ilipo, Kamati inashauri kuwa nyumba zote za Shirika zilizochakaa na ambazo uendeshaji wake ni mkubwa kuliko faida inayopatikana zibomolewe na maeneo hayo yaendelezwe kwa kujenga majengo ya kisasa yatakayoendana na thamani ya ardhi ya eneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa angalizo kwa Shirika litakapokuwa likijenga nyumba zake kuhakikisha wanatenga maeneo ya wazi kwa ajili ya michezo ya watoto na maeneo ya kuegesha magari na wale waliokuwepo basi watapata kipaumbele katika kukodishwa maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT)* kwenye nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa kwa ajili ya kuuzwa, unazifanya nyumba hizi ziwe ghali na kutompa unafuu mnunuzi anayetaka kumiliki nyumba hasa mwananchi wa kipato cha chini. Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa miradi ya Nyumba za Shirika la Nyumba kwa mwaka ujao wa Fedha kwani mfumo mzima wa ujenzi wa nyumba unahusishwa na ulipaji wa kodi ikiwa ni pamoja na vifaa vya ujenzi na makandarasi. Kwa kufanya hivyo, gharama ya nyumba hizo itapungua na hivyo kumwezesha mwananchi wa kawaida kuweza kukopa na kununua nyumba hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ilipoamua kuuza nyumba zake kwa watumishi kupitia Wakala wa Majengo *(TBA)* haikutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwa mauzo hayo, Kamati inashauri Serikali itumie utaratibu huu pia hasa kwa nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba na kuuzwa kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi katika Serikali za Mitaa bado halijapewa kipaumbele japokuwa mipango yote ya maendeleo duniani kote hutegemea ardhi. Halmashauri zimekuwa zikitengewa bajeti ndogo kwa ajili ya shughuli za sekta ya ardhi hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya msingi yanayohusu ardhi. Kamati inaitaka Serikali kulipa kipaumbele suala la ardhi katika Halmshauri kwani bila mipango mizuri ya matumizi ya ardhi, nchi haiwezi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa za Wizara hii ni kuongezeka kwa migogoro ya mipaka ya ardhi hapa nchini inayochangiwa na matatizo makubwa ya upimaji wa maeneo ya wananchi na upatikanaji wa hati miliki za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hii, bado Wizara imetenga bajeti ndogo kwa ajili ya mradi wa maendeleo wa Upimaji na Ramani (Kifungu kidogo cha 2002) kwa ajili ya mipaka ya kimataifa na mipaka ya ndani. Serikali imetenga kiasi cha Sh.300,000,000/= tu ukilinganisha na kiwango kilichotolewa mwaka wa fedha uliopita cha Sh.1,579,705,000/= Kamati inapendekeza kuwa ili

kupunguza migogoro ya mipaka, ni vyema kwa mwaka ujao wa fedha, kifungu hiki kikapewa kipaumbele na kupangiwa fedha ya kutosha kutekeleza majukumu yake na hivyo kusaidia kutekeleza mipango ya maendeleo ya ardhi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na mpango wake wa kupima na kutoa hati za kimila katika maeneo ambayo bado hayapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi, (*NHBRA*), una mchango mkubwa hasa katika kufanya utafiti na ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu ili kuinua na kuboresha viwango vya nyumba na kuongeza ubora wa maisha ya wananchi vijijini na mijini. Pamoja na umuhimu wa Wakala huu kwa Taifa, bado imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha hasa fedha za maendeleo ambazo zinahitajika kwa ajili ya utafiti. Kuanzia mwaka 1984 mpaka sasa utafiti haujawahi kutengewa fedha yoyote ya maendelo hivyo kukwamisha jitihada za Wakala katika kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wakala iliomba fedha za matumizi mengine kiasi cha shilingi bilioni 1.8 na Serikali ikaitenga shilingi milioni 754. Mpaka kufikia mwezi Mei 2012 Wakala alikuwa amepokea shilingi milioni 369 tu. Kamati inasikitishwa sana na bajeti ndogo zinazotengwa ukilinganisha na umuhimu wa kazi ya Wakala na hivyo naishauri Serikali, kutambua umuhimu wa Wakala huu na kutenga fedha za kutosha ili Wakala ieze kujitangaza, kusambaza teknolojia ya ujenzi wa

gharama nafuu, kuongeza watumishi wa Wakala na kununulia vifaa vya maabara kwa ajili ya tafiti zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na wadau wengine kwa kuwa katika hatua ya kuanzisha Mamlaka itakayosimamia maendeleo ya ardhi. Mamlaka hiyo pamoja na majukumu mengine itafanya kazi ya kutambua uwezo wa mwekezaji kabla ya kummilikisha ardhi na vilevile itatambua ardhi inayofaa kwa uwekezaji na kuingiza kwenye hazina ya ardhi kwa maana ya *land bank.* Kamati inaamini Mamlaka hii ikianzishwa itapunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya ardhi inayoendelea nchini. Aidha, Kamati inatoa angalizo kwa Wizara kuzingatia Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999, wakati wa kuingiza ardhi husika kwenye hazina ya ardhi kwani migogoro mingi hutokea ardhi ya kijiji inapomilikishwa kwa mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia majukumu makubwa ya Wizara hii na ufinyu wa Bajeti inayotolewa kwa ajili ya Wizara kutekeleza majukumu yake, Kamati inashauri ni vyema Wizara ikaanzisha utaratibu wa kukusanya kodi za majengo *(property tax)* hasa majengo makubwa yaliyopo mijini kwa ajili ya kuongezea mapato ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Mwisho lakini si kwa umuhimu, nakushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wenzako wote wa Bunge, kwa kazi kubwa

mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 hadi kukamilika kwa taarifa hii ambayo kwa niaba yao naiwasilisha leo katika Bunge lako Tukufu. Kwa heshima, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge, ambaye ni Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdulkarim E.H. Shah, ambaye ni Makamu Mwenyekiti ambaye ndiye ninayesoma hotuba hii, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Benardetha K. Mushashu, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Ali khamis Seif, Mheshimiwa Suzan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Michael Lekule laizer, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mheshimiwa Dkt.

Mary Machuche Mwanjelwa, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Al- Shymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga na Mheshimiwa Abdallah Haji Ali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, Makatibu wa Kamati, Ndugu Rachel Nyambuli Nyega na Ndugu Grace Bidya kwa kusaidiwa na Ndugu Lukindo Choholo, kwa kuihudumia Kamati ipasavyo na kufanikisha maandalizi ya taarifa hii. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru tena wewe na pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Bungeni, naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, utangulizi. Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikushukuru wewe kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii kwa mujibu wa Kanuni ya 99 kanuni ndogo ya (7), ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wa Jimbo la Kawe (wapiga kura wangu), kwa imani yao kwangu, makamanda wote (vijana, wazee na akina mama wa vyama vyote) kwa kuendelea kuniunga mkono katika kuhakikisha Jimbo letu linapata huduma zote za msingi katika viwango stahili. Ahadi yangu kwenu ni kuwatumikia kwa uwezo wangu wote kwa kadiri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa CHADEMA kikiwa chini ya Mtendaji wake Mkuu (Katibu Mkuu-Taifa), Mheshimiwa Willbroad Peter Slaa. Hakika kila Mtanzania anaona kazi unayoifanya ya kuhakikisha chama chetu kina kuwa juu na Watanzania wote wanatuunga mkono. Mungu akupe uhai, naamini ipo siku tutaifikia Nchi ya Ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, kwa kuniamini na kuniteua tena kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii. Shukrani pia ziende kwa wasaidizi wa Kiongozi wa Kambi, Mheshimiwa Kabwe Zitto (Naibu Kiongozi wa Kambi) na Mheshimiwa Tundu Lissu (Mnadhimu wa Kambi), kwa kutuongoza vyema katika shughuli hii ngumu ya kuwatetea wanyonge. Shukrani pia ziwafikie Wabunge wenzangu wote wa Kambi kwa ushirikiano wao kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, niishukuru sana familia yangu yote, wazazi wangu Profesa James Salehe Mdee na Theresia Kisenga Ngowi, kwa upendo wao na kwa upekee nimshukuru kaka yangu Joseph James Mdee, kwa msaada na ushauri mkubwa katika kuhakikisha natimiza majukumu yangu ya Kibunge ndani na nje ya Bunge. Ahsanteni sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za Kambi ya Upinzani 2011/2012, kufuatia Hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni ya mwaka 2011/2012, Kambi ya Upinzani inatambua hatua zilizochukuliwa na Serikali

katika hoja kadhaa ambazo ziliwasilishwa kwake hususan suala la ada ya ukodishwaji wa mashamba na vitalu ambapo Serikali ilikuwa inatoza shilingi 220 tu kwa eka. Kauli ya Serikali kupitia Naibu Waziri wa Ardhi wakati akichangia hotuba ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka 2012/2013 imeonyesha nia ya Serikali kuongeza ada husika ili kuiongezea Serikali mapato. Kambi ya Upinzani inatambua pia hatua ambazo Serikali imeahidi kuzichukua katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 kwa kutenga fedha za fidia kwa wananchi wa Kurasini Mabwawani. Serikali imeeleza kwamba fidia zitalipwa kwa viwango vipya kuendana na thamani ya soko. Kwa umuhimu zaidi nitambue kauli iliyotolewa na Waziri wa Ardhi asubuhi hii akisisitiza kwamba linapokuja suala la uwekezaji sheria za nchi lazima zizingatiwe na kufuatwa. Hoja ambayo tuliizungumza kwa kina sana katika Hotuba yetu ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, Kambi ya Upinzani inatambua hatua zitakazochukuliwa na Serikali kuhusiana na mwekezaji Agrisol, ili kuiepusha nchi kuingia kwenye mkataba mbovu usiozingatia maslahi na sheria za nchi. Kambi ya Upinzani imefarijika na Kauli ya Waziri Mkuu wakati akihitimisha hotuba yake ya bajeti ambapo, pamoja na mambo mengine alitamka kwamba mchakato wa Agrisol haujaanza, hawajaingia makubaliano/mkataba wowote na kwamba mchakato ukianza ndipo wataingia kwenye mambo ya msingi waone wanapangiana vipi, uwiano utakuwaje na kwamba Halmashauri imiliki kiasi gani cha hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai ya Kambi ya Upinzani ni kwa Serikali kusitisha mpango wake wa kuligawa eneo la Mishamo na Katumba lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 325,000 au ekari 760,728 kwa Agrisol. Kuna taarifa kwamba tayari Serikali ilishaligawa eneo la Lugufu lenye ukubwa wa hekta 10,000 kwa Agrisol (kwa kuwa mikataba inaendeshwa kwa usiri mkubwa.) Ni imani yangu Serikali itatupa jibu juu ya mustakabali wa Lugufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ikitafakari, ni muhimu Bunge hili Tukufu likaelewa kwamba aliyekuwa mshirika muhimu wa *Agrisol IOWA State University College of Agriculture,* aliyekuwa mhimili muhimu wa mwekezaji huyu hasa katika kuwasaidia wakulima wadogowadogo kama ilivyoainishwa katika kipengele cha 4.7 cha MoU baina Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda na *Agrisol Energy Tanzania Limited* alijitoa baada ya kugundua kwamba mwekezaji huyu hana dhamira ya kuisaidia nchi na wakulima wadogo zaidi ya kujinufaisha kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya *IOWA State University College of Agriculture,* ilijitoa baada ya kugundua ilitumiwa na mmiliki wa Agrisol, bwana Bruce Rastetter ili aweze kupata uhalali wa kukubalika kirahisi kama mwekezaji mahiri. Ukweli ni kwamba nia ya mwekezaji huyu haikuwa kuisaidia nchi bali kuendeleza mashamba makubwa ya zao mojamoja, yenye matumizi ya viwango vikubwa vya kemikali na pia kuomba mabadiliko katika kanuni za kitaifa za usalama

wa kibiolojia ili mazao yenye viinitete (*GMO*) yaweze kupandwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara ya *GMO* ni makubwa sana, moja kubwa ni kufifisha kabisa matumizi ya mbegu za asili. Mwekezaji akizitumia kwenye eneo lake, madhara yanasambaa pia kwa mashamba ya jirani, inajenga utegemezi wa wakulima kununua mbegu kutoka kwa wakulima wakubwa. Mbali na utegemezi wa mbegu, *GMO* zina madhara makubwa sana kiafya. Tafiti zimeonyesha kwamba nchi zilizoendelea ziko katika vita kali sana za kuzuia matumizi ya *GMO* lakini sisi tunayapokea makampuni makubwa kwa misamaha lukuki ya kodi, tukiamini tunaalika wawekezaji waje kuijenga nchi, kumbe wanakuja kutengeneza Taifa la utegemezi na lenye maradhi lukuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu ikaeleweka kwamba katika Wilaya ya Mpanda, ardhi ambayo iko wazi kwa matumizi ya binadamu (*arable land*) ni 19% tu ya eneo lote. Nyingine iliyobaki ni hifadhi za taifa ambapo 18% hifadhi ya wanyama, 59% hifadhi ya misitu na 4% hifadhi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kila kitu kuwategemea mabeberu, inawezekana kabisa Serikali ikawekeza katika eneo husika. Taarifa zinaonyesha kwamba Agrisol walitarajia kuwekeza $100 milioni (shilingi bilioni 150) katika kipindi cha miaka 10, kwa matarajio ya kupata faida ya $272 milioni (shilingi bilioni 408) ndani ya mwaka mmoja baada ya uwekezaji huo

kwa kulima hekta 200,000 tu za mahindi, kiasi ambacho kinalingana kama sio kuzidi bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Agrisol wangepata/watapata hadhi ya mwekezaji wa kimkakati *(strategic investor).* Wangepata/watapata pia msamaha wa kodi ya shirika (*corporate tax*) ambayo ni 30% ya shilingi bilioni 408 (ambayo ni bilioni 122). Hivi kweli Serikali makini, mbali ya kuwa na vivutio vya utalii vilivyosheheni na hivyo kuwa nchi ya nne ya uzalishaji wa dhahabu Afrika, nchi pekee yenye madini tofautitofauti zaidi ya 15 na kwa upekee ni madini ya Tanzanite, tuna urani ya kutosha, hivi karibuni tumegundua gesi yenye thamani ya Tsh. trilioni 626.7, tuna tani milioni 86 za makaa ya mawe, tuna kila dalili ya kupata mafuta na kadhalika, inashindwa kuwekeza kwa faida ya nchi na wananchi wake? Tunawezaje kuokoa kizazi cha vijana waliogeuka wazururaji kwa sababu Serikali yao haijawapa fursa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2011/2012, Kambi ya Upinzani ilielezea kwa kina matatizo sugu ya migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini ambayo imekithiri kufikia hatua ya uvunjifu wa amani kunakopelekea umwagaji damu na wakati mwingine vifo kutokea. Mwaka mmoja umepita bado hakuna hatua dhahiri zilizochukuliwa na Serikali hususan kuhusu:-

(i) Mgogoro wa ardhi unaowahusisha wakulima wa kijiji cha Nzasa, ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii wanataka kuwaondoa wananchi katika ardhi yao

halali kwa madai kwamba wanaishi ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi.

(ii) Mustakabali wa maeneo ya yaliyokuwa mashamba ya Ngano, Hanang (*Hanang Wheat Complex (HWC)* na *Dakawa Ranch*.

(iii) Tatizo la ukodishwaji wa mashamba unaofanywa na wawekezaji dhidi ya wananchi wenyeji. Hususan shamba la mpunga la Mbarali na Kapunga, yote yakiwa Wilaya ya Mbarali na mwekezaji *RAI Group* anayemiliki mashamba ya *Setchet*, *Murjala* na *Gidagamowd* ambaye alikuwa anawakodisha wananchi $10 kwa ekari.

Kambi ya Upinzani ina taarifa za kuendelea kwa ukodishaji wa mashamba unaofanywa na wawekezaji. Shamba la hekta moja hukodishwa kwa shilingi laki moja mpaka laki moja na nusu katika mashamba ya Kapunga na Mbarali.

Hoja ya Kambi ya Upinzani imethibitishwa pia na timu ya wataalam wa *Consolidated Holding Corporation (CHC)* katika taarifa yao ya ufuatiliaji wa mashamba na viwanda vilivyobinafsishwa, kwa mujibu wa *Consolidated Holding Corporation, United Republic of Tanzania,* Taarifa ya Ufuatiliaji wa Mashamba na viwanda vya bidhaa za kilimo, Januari 2012, *pg x*, inabainisha kwamba katika shamba la Mbarali *Rice Farm* mwekezaji analima sehemu ya shamba na sehemu nyingine ya shamba anakodisha kwa wananchi kwa utaratibu maalum.

(iv) Kambi ya Upinzani inataka kujua mustakabali wa kijiji cha Kapunga, kilichopo Wilaya ya Mbarali ambacho kiliuzwa kwa mwekezaji. Mkataba wa mauzo na Hati Miliki ya shamba (*Certificate of Title*) zinaonyesha kuwa shamba lina ukubwa wa hekta 7,370. Wanakijiji wanadai kuwa shamba linatakiwa kuwa na ukubwa wa hekta 5,500 kulingana na barua ya maombi ya ardhi kutoka kwa *NAFCO* na muhtasari wa mkutano wa kijiji ulioidhinisha utoaji wa eneo husika.

(v) Mashamba ya *Gawal* na *Warret* yaliyopo Hanang yalitakiwa kurejeshwa kwa wananchi lakini hayajarejeshwa.

(vi) Mgogoro wa ardhi baina ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) na wananchi wa Bukanga na Buhare (Mgaranjab) Musoma Mjini.

(vii) Mgogoro unaohusu shamba namba 299 (iliyokuwa *NARCO Ranches*) lenye ukubwa wa hekta 49,981. Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero. Mgogoro huu uliwahusisha vigogo wakubwa wastaafu wa Chama cha Siasa na Serikali.

(viii) Mgogoro baina ya Simba *Motors* na wanakijiji wa Mapinga, kitongoji cha Undindivu, Wilaya ya Bagamoyo.

(ix) Mgogoro baina ya wakulima na wafugaji wa jamii ya Wamasai katika eneo la vijiji vya Izava (Chamwino) na Chitengo (Kongwa).

(x) Uvamizi wa maeneo ya wazi Mkoa wa Dar es Salaam; viwanja vingapi vimerejeshwa kwa matumizi ya umma na viwanja vingapi bado vipo mikononi mwa wavamizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya tathmini na malipo ya fidia. Imekuwa ni jambo la kawaida sana kwa zoezi la fidia kuendeshwa kienyeji na pasipo kuzingatia Sheria na taratibu tulizojiwekea na hata wananchi wakilalamika, Serikali inaendelea na miradi. Kambi ya Upinzani inataka majibu ya hoja zifuatazo ambazo licha ya kuzungumzwa katika bajeti ya mwaka 2011/2012 bado Serikali haijazipatia majibu:-

(i) Hatma ya wanakijiji wa kijiji cha Mabwepande ambao miaka mitano iliyopita Serikali ilifanya tathmini na kuwaagiza wasifanye maendeleo yoyote ili kupisha ujenzi wa Chuo cha *IFM*. Pia baada ya mafuriko makubwa yaliyolikumbwa Jiji la Dar es Salaam maeneo yao yalichukuliwa na Serikali kwa ajili ya kugawa viwanja kwa waathirika. Mpaka sasa hakuna fidia yoyote iliyolipwa.

(ii) Hatma ya wananchi wa Kigamboni.

(iii) Hatma ya wananchi 1600 wa Wilaya ya Mbarali waliotakiwa kuondoka kupisha upanuzi wa mbuga ya Taifa ya Ruaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012. Mpango wa Taifa, kwa mujibu wa *The Tanzania Long Term Perspective Plan (LTPP) 2011/2012-25/26. The Road Map to a Middle Income*

Country, April, 2012, pg 28, umeainisha wazi kwamba, pamoja na mambo mengine kufanikiwa kwake kunategemeana sana na mipango bora ya matumizi ya ardhi na chombo pekee cha kuweza kufanikisha hili ni Wizara ya Ardhi kupitia taasisi yake ya Tume ya Taifa ya Mipango. Kati ya majukumu ya Tume ni:-

(i) Kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji.

(ii) Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi kwa kutekeleza programu za kilimo, mifugo na maji kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo, Maji na Kilimo.

(iii) Kusaidia kupatikana kwa ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa Kilimo Kwanza.

(iv) Kufanya utafiti katika masuala yanayohusiana na ardhi hasa katika maeneo yenye migogoro, uhamiaji mijini kutoka vijijini, ushirikishwaji wananchi katika kuendeleza ardhi mijini, viwango vya matumizi ardhi mijini na vijijini.

(v) Kufuatilia na kutathmini mipango ya matumizi ya ardhi iliyokwishaandaliwa na katika maeneo yenye migogoro sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba majukumu yao yangekuwa yanachukuliwa kwa uzito unaostahili, leo tungekuwa hatuzungumzii hoja za migogoro ya ardhi ambayo kwa sasa ni tishio la amani ya nchi, bali

mafanikio ya matumizi endelevu ya rasilimali kubwa ya ardhi tuliyobarikiwa na mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupuuzwa kwa miradi ya maendeleo. Licha ya umuhimu na ukubwa wa majukumu yake, Wizara ya Ardhi ni kati ya Wizara ambazo zinapewa fedha ndogo sana za kutekeleza miradi ya maendeleo na mbaya zaidi, licha ya ufinyu wa fedha, fedha zimekuwa hazipelekwi zote. Mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 22,265,078,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi mwaka unaisha, Wizara ilipokea jumla ya shilingi 4,673,383,000/- tu ambapo fedha zilizotumika kutekeleza miradi ya maendeleo ni shilingi 3,931,581,086/- Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2010/2011 na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, tarehe 1 Juni, 2011. Hali kadhalika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 22,010,437,000/ kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Mei 2012, Wizara ilipokea shilingi 3,663,685,463.96/- tu kwa jili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzembe wa aina hii hauwezi kuvumilika. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu, ni kwa nini kwa miaka miwili mfululizo fedha za maendeleo zimekuwa hazitolewi kama zilivyopangwa? Sambamba na hilo, ni miradi mingapi imekwama kutokana na upungufu huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupuuzwa kwa maelekezo ya Waziri Mkuu. Kwa kuzingatia changamoto za kimapato zinazoikabili Wizara ya Ardhi, Serikali kupitia Kauli ya Waziri Mkuu iliridhia kuipatia Wizara kibali cha kubakia na makusanyo yao asilimia 100. Naomba kumnukuu:

"Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasema hivi, jana tukiwa kwenye Cabinet tumemuidhinishia huyu mama kwamba wewe mama ile fedha yote ambayo utakuwa unakusanya kutokana na shughuli zako za ardhi baki nayo yote, chukua yote ili ikusaidie wewe katika uendeshaji wa Wizara hiyo. Kwa hiyo, tunatambua changamoto alizonazo na naamini tutamsaidia vizuri sana na najua ataweza". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 hadi Mei 2012, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 16. Kinyume na maelekezo ya Waziri Mkuu, Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 9.4 tu, sawa na asilimia 59 ya kilichokusanywa. Kutokana na upungufu huo, Wizara ilishindwa kuongeza gawio la fedha za *retention* kwa Halmashauri mpaka kufikia 30% badala ya gawio la sasa la 20%. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo juu ya mustakabali wa kiasi cha *retention* ambacho bado hakijapelekwa Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yanayohitaji maelezo. Mishahara. Imekuwa ni utaratibu wa Bunge lako Tukufu kupitisha mafungu mbalimbali kama yalivyoombwa na Wizara na Idara mbalimbali za Serikali. Tafsiri ikiwa kila Wizara au Idara ya Serikali ina

ufahamu wa makadirio ya fedha ambazo inatarajia kutumia katika fungu husika. Kwa miaka miwili mfululizo, Wizara ya Ardhi imekuwa ikitumia fungu la mshahara kuliko kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 6,423,295,000/- kwa ajili ya mishahara. Lakini katika kipindi cha Julai 2010 hadi Mei 2011 kiasi cha shilingi 8,499,539,334/- zilitumika kulipa mishahara. Hali kadhalika katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara iliidhinishiwa shilingi 7,531,409,000/- kwa ajili ya matumizi ya mishahara. Hadi Mei 2012, kiasi cha shilingi 9,765,774,300/- zilitumika kulipa mishahara. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo, hiyo tofauti (ya zaidi ya shilingi bilioni mbili) ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge na kiasi kilichotumiwa na Wizara kwa miaka miwili mfululizo imetokana na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya Kimataifa. Serikali ilikuwa katika mchakato wa kuandaa andiko la kuomba eneo la nyongeza nje ya ukanda wa kiuchumi baharini . Andiko hili liliwasilishwa Umoja wa Mataifa tarehe 18 Januari 2012. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na 2011/2012, kiasi cha shilingi 431,572,872/- na 171,920,854.59/- zilitumika kuandaa andiko husika. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kutoa mchanganuo wa matumizi husika na kuainisha ni kwa namna gani Andiko limeweza kuigharimu Serikali zaidi ya shilingi milioni mia sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba yaliyobinafsishwa ambayo hayajaendelezwa. Wakati

akihitimisha bajeti ya ardhi mwaka jana, Waziri wa Ardhi aliliahidi Bunge lako Tukufu kwamba baada ya Bunge la bajeti, Wizara ingekwenda kufanya ukaguzi huru wa nani ametelekeza mashamba. Alisisitiza kwamba wawekezaji wote waliotelekeza mashamba *the honeymoon is over*. Hii ni kwa mujibu wa Majadiliano ya Bunge, Taarifa Rasmi *(Hansard),* Mkutano wa Nne, Kikao cha Arobaini na Nane, Tarehe 16 Agosti, 2011. Kambi ya Upinzani inataka kupata idadi ya mashamba yaliyokaguliwa na Wizara na mahali yalipo toka ahadi husika ilipotolewa na ni hatua gani ambazo zimeshachukuliwa na Serikali dhidi ya wawekezaji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kambi ya Upinzani ikisubiri taarifa toka kwa Waziri wa Ardhi juu ya ukaguzi huru iliyofanywa na Wizara kuweza kuwabaini waliotelekeza mashamba, Kambi ya Upinzani, inataka Serikali itoe msimamo juu ya taarifa ya ufuatiliaji wa mashamba na viwanda vya bidhaa na kilimo iliyofanyiwa kazi na *CHC* kufuatia maelekezo waliyopewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma *(POAC).* Taarifa husika imebainisha kwamba mashamba 13 yenye ukubwa wa hekta 71,184 yalikuwa yameendelezwa kwa kiasi, wakati mashamba 14 yenye ukubwa wa hekta 44,764 yalikuwa hayajaendelezwa kabisa/yametelekezwa. Mengi ya mashamba yakiwa ni mashamba ya Mkonge. Mashamba hayo ni:-

(i) *Ndungu Sisal Estate*, shamba hili lenye ukubwa wa hekta 1,230. 9 liliuzwa kwa *L.M Investiment* ya Tanga mwaka 1997 kwa bei ya shilingi milioni 278.

Mpaka sasa mwaka 2012, miaka 15 baada ya kukabidhiwa shamba, mwekezaji ameendeleza 52% tu ya shamba lote.

(ii) *Mkumbara Sisal Estate*, shamba hili lenye ukubwa wa hekta 1,734 liliuzwa mwaka 1997 kwa *M/S D.D Ruhinda & Company Limited* kwa bei ya shilingi 100 milioni. Mpaka sasa (miaka 15 baada ya kukabidhiwa shamba) mwekezaji ameendeleza 52% tu ya shamba lote.

(iii) *Toronto Sisal Estate*, shamba lenye ukubwa wa hekta 6,023 lililobinafsishwa kwa *Highland Estate Limited* kwa bei ya shilingi milioni 265.4 mwaka 1998. Mpaka Septemba 2011, ni 50% tu ya shamba lilikuwa limeendelezwa. Taarifa zilizopo ni kwamba mwekezaji husika hana hati miliki ya shamba kutokana na kudaiwa riba hivyo kushindwa kupata mkopo wa kuliendeleza shamba.

(iv) *Magunga Sisal Estate*, shamba lipo Wilaya ya Korogwe, lina ukubwa wa hekta 6,520. Katika shamba hili ambalo linamilikiwa kwa ubia na kuendeshwa kwa kilimo cha mkataba kati ya wakulima wadogo wa mkonge na Katani *Limited* limeendelezwa kwa 19% tu.

(v) *Mgombezi Sisal Estate*, shamba liko Wilaya ya Korogwe na lina ukubwa wa hekta 6,480 ambapo hekta 3881 zimegawiwa kwa wakulima. Shamba linaendeshwa kwa kilimo cha mkataba kati ya wakulima wakubwa na wa kati. Eneo lililopandwa mkonge ni hekta 1301.6 tu.

(vi) *Hale Mruazi Sisal Estate*, shamba lina ukubwa wa hekta 4,180, ambapo hekta 1,136 tu ndizo zilizopandwa mkonge.

(vii) *Manzabay Sisal Estate*, shamba liliuzwa kwa *Chavda Group* mwaka 1998. Mwekezaji alitumia hati miliki kupata mkopo ambapo hakutumia mkopo husika kuendeleza shamba, shamba husika lilishikiliwa na *CRDB* mpaka mwaka 2001 alipoiuzia *Mbegu Technologies* ambaye naye amelikodisha kwa Omari Mduduma. Shamba halijaendelezwa.

(viii) *Kwashemshi Sisal Estate*, shamba lina ukubwa wa hetka 1498.5, shamba liliuzwa kwa *Chavda Group* mwaka 1998, mwekezaji alitumia hati miliki ya shamba kupata mkopo, ambao hakuutumia kuendeleza shamba. Shamba hilo lilishikiliwa na *NBC* mpaka 2003 lilipouzwa kwa Mathew Upanga Mnkande. Shamba limeendelezwa kwa 35% tu.

(ix) *Ubena Sisal Estate,* shamba lenye ukubwa wa hekta 4,227 ambalo lipo Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani liliuzwa kwa *Highlands Estates Limited* mwaka 2007 kwa kiasi cha shilingi 278 milioni. Jumla ya hekta 499 ambayo ni sawa na 12% tu imepandwa mkonge.

(x) *Kingolwila/Pangawe Sisal Estate*, shamba lenye ukubwa wa hekta 3703 liko Wilaya ya Morogoro, Mkoani Morogoro, liliuzwa kwa *Highland Estates limited* kwa bei ya shilingi milioni 210.2 kupitia *PSRC* mwaka 2007. Jumla ya hekta 800 kati ya hekta 3703 ambazo ni sawa na 22% ya eneo lote ndio zimepandwa mkonge.

(xi) *Msowero Sisal Estate*, Shamba lenye ukubwa wa hekta 5200 lipo Wilaya ya Kilosa Morogogo, shamba liliuzwa na Mamlaka ya Mkonge Tanzania kwa kampuni ya *Noble Azania* Agricultural *Enterprises* mwaka 1993. Shamba limepandwa mkonge hekta 900 tu ambazo ni 17% ya shamba lote na alizeti na mtama zimepandwa hekta 200 tu. Hekta 4100 hazijaendelezwa toka mwaka 1993.

(xii) *Rudewa Sisal Estate*, shamba lina ukubwa wa hekta 6351, liliuzwa kwa kampuni ya *Farm Land* mwaka 1992. Kampuni husika iliuza shamba kwa kampuni ya *China State Farms Agribusiness* (*Group*) *Corporation Tanzania Limited* (*CSFACOT*) kwa kiasi cha dola za kimarekani milioni 1.2 mwaka 2000. Mwekezaji ameweza kuendeleza 32% tu kwa kupanda mkonge hekta 2018.

(xiii) *Kimamba Fibre Estate*, shamba lenye ukubwa wa hekta 5743 liliuzwa kwa kampuni ya *ANCO Limited* mwaka 1998. Mwaka 2009 Kampuni ya *ANCO Limited* iliuza hekta 3,043 kwa kampuni ya Sino na kubakiwa na hekta 2700. Mustakabali wa shamba walilouziwa Sino haujulikani, ila shamba lililobaki *ANCO Limited* limeendelezwa kwa 46.3% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba ambayo hayajaendelezwa kabisa ni:-

(i) *Kikulu Sisal Estate*, lenye ukubwa wa hekta 5900 lililouzwa kwa *Chavda Group,* mwekezaji aliweka

dhamana shamba, kama kawaida yake akachukua mkopo hakuendeleza shamba.

(ii) *Kibaranga Sisal Estate* lenye ukubwa wa hekta 6,900, liliuzwa kwa kampuni ya *Katani Limited*, iliposhindwa kuendeleza Serikali ililiweka chini ya *PSRC* na Bodi ya Mkonge.

(iii) *Kwamngwe Sisal Estate*, lenye ukubwa wa hekta 3700, liliuzwa kwa *Chavda Group* mwaka 1998, alichukua mkopo, hakuendeleza shamba.

(iv) *Kwafungo Sisal Estate*, lenye ukubwa wa hekta 2310, liliuzwa kwa *Chavda Group* mwaka 1998, mwekezaji alitumia hatimiliki ya shamba kuchukua mkopo, ambapo hakutumia kwa kusudi la kuendeleza shamba. Shamba hilo bado linashikiliwa na *CRDB*.

(v) *Bombuera Sisal Estate*, lenye ukubwa wa hekta 2370, lipo Korogwe, liliuzwa kwa *Chavda Group* mwaka 1998. Mwekezaji alitumia hatimiliki ya shamba kupata mkopo. Hakuliendeleza shamba. Mwaka 2002 *CRDB* iliuza shamba kwa *AMC Arusha Limited.*

(vi) *Hale Mwakiyumbi Sisal Estate*, lenye ukubwa wa hekta 4,309. Shamba liliuzwa kwa *Chavda Group,* 1998. Alitumia hatimiliki kupata mkopo ambao hakuutumia kwa kusudi la kuendeleza shamba na kulitekeleza. Shamba linashikiliwa na *CRDB*.

(vii) *Allidina Sisal Estate*, lenye ukubwa wa hekta 2300, liliuzwa kwa *Noble Azania Agriculture Enterprises* mwaka 1993. Hakuna uwekezaji wowote uliofanyika.

(viii) *Msowero (Godes) Farm*, lenye ukubwa wa hekta 5,000. Lilikuwa linasimamiwa na Wizara ya Kilimo chini ya *Tanzania Livestock research Organization* (*TALIRO*). Mwaka 1993, Serikali ya CCM ilipanga kujenga Chuo cha Mifugo. Mpango ambao haukukamilika, shamba likabaki bila usimamizi wowote.

(ix) *Rutindi Sisal Estate*, lina ukubwa wa hekta 1,087. Shamba liko Morogoro, linamilikiwa na kampuni ya *Noble Azania Agricultural Enterprises*. Shamba halijaendelezwa na mwekezaji toka amelinunua.

(x) *Magole Sisal Estate*, lina ukubwa wa hekta 1,149. Lipo Dumila, kilometa 65 toka Kilosa. Lilikuwa la Serikali chini ya Mamlaka ya Mkonge Tanzania. Japo halijabinafsishwa liko katika hali mbaya.

(xi) *Mauze Sisal Estate*, lina ukubwa wa hekta 2,842.5. Shamba lilikuwa na deni la shilingi milioni 1.36 kutoka benki ya *NBC*. Benki ilishikilia Hatimiliki na kuliweka chini ya ufilisi wa *LART* kutokana na kuongezeka kwa deni mpaka milioni 10. Kwa sasa kuna vijiji vya Kilangali na Mabwembele vilivyoanzishwa na vimesajiliwa ndani ya shamba. Halmashauri za vijiji hivyo zinakodisha maeneo katika shamba hilo kwa wanavijiji na watu kutoka nje ya vijiji kwa gharama ya shilingi 3,000 kwa ekari moja.

(xii) *Myombo* na *Kilosa Sisal Estate*. Mashamba haya yana ukubwa wa hekta 2,024 (Kilosa) na 1843 (Miyombo). Mashamba yalibinafsishwa na Mamlaka ya Mkonge kwa Kampuni ya Katani mwaka 1998.

Baada ya kampuni ya *Katani Limited* kushindwa kuyaendesha, iliyakodisha kwa kampuni ya *Agro-Focus.* Mwaka 2005, Baraza la Mawaziri liliagiza kuwa mashamba haya yatafutiwe mwekezaji mwenye uwezo kwani kampuni ya *Agro- Focus Limited* imeshindwa kuyaendeleza. Hata hivyo, kinyume na maagizo, mwaka 2009, Bodi ya Mkonge iliyauza mashamba haya kwa *Agro-Focus.* Matokeo yake mpaka sasa hakuna uwekezaji wowote uliofanywa. Sehemu kubwa ya shamba ni pori na sehemu iliyobaki imekodishwa kwa wananchi kwa ajili ya kulima mahindi.

(xiii) *Madoto Sisal Estate*, shamba lina ukubwa wa hekta 3,200. Shamba lilinunuliwa na kampuni ya *SUMAGRO Limited* ambayo nayo ililiuza kwa *East African Breweries* mnamo mwaka 2009. Hakuna uwekezaji wowote uliofanyika.

(xiv) *Kivungu Sisal Estate*, shamba lina ukubwa wa hekta 2,200. Shamba lilinunuliwa na kampuni ya *SUMAGRO Limited*. Ililiuza kwa *East African Brewaries* mwaka 2009. Hakuna uwekezaji wowote uliofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuyarejesha mashamba yote ambayo wawekezaji wameshindwa kuyaendeleza kama ambavyo taarifa hii imeainisha. Hali kadhalika, kwa wale wawekezaji ambao wameweza kuendeleza sehemu ndogo na hawana uwezo wa kuendeleleza shamba zima, warejeshe sehemu ya mashamba waliyoshindwa kuendeleza ili wapewe wananchi wenye uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza Serikali iangalie hatua za kuchukua dhidi ya wawekezaji katika mashamba 13 ambao wameshindwa kuendeleza mashamba kwa 100%. Pamoja na wawekezaji katika mashamba 14 ambao wameshindwa kabisa kuendeleza mashamba waliyonunua, kama ambavyo yameorodheshwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tathmini hii fupi iliyofanywa na *CHC,* utaona ni kwa namna gani zoezi la ubinafsishwaji mashamba lilifanywa kiholela na kwa hujuma, pasipo kuzingatia maslahi ya umma. Katika hali ya kawaida, watu wote walioshiriki katika zoezi hilo wana kila sababu ya kuchukuliwa hatua, hakika hawana tofauti na wahujumu uchumi. Kwa mfano huyu mwekezaji anayejiita *Chavda Group*, aliuziwa shamba kwa bei ya kutupa, mashamba saba, yenye ukubwa wa hekta 25,000, katika maeneo tofauti ya nchi hii. Kikubwa alichokifanya ni kutumia hati za shamba kuchukulia mikopo, kisha kutelekeza mashamba. Hivi kweli unahitaji kuwa na akili nyingi kuyaona haya? Nyuma ya *Chavda Group* wako akina nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe ni familia hiihii ya Chavda (V*.G Chavda na kaka yake P.G Chavda),* waliojitwalia mkopo wa $3.5m mwaka 1993 chini ya *DCP* (*Debt Conversion Program)* wakiahidi kufufua mashamba ya mkonge Tanga ndani ya miaka 10 na kupata $42 milioni. Taarifa hii ni kwa mujibu wa *Corruption, Politics and Societal Values in Tanzania. An*

Evaluation of the Mkapa Administration's Anti-Corruption Efforts, Dr. Bruce Heilman and Dr. Lauren ndumbaro, Vol.7 (2002). Walipopata hayo mapesa, hawakufanya lolote na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi yao. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu, lazima tuwachukulie wawekezaji wa aina hii kama ni waporaji na hawana tofauti na majambazi yanayoiba benki kwa kutumia nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi yenye jukumu pana la kusimamia sekta ya ardhi kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo hayajaendelezwa na wawekezaji yanarejeshwa Serikalini bure bila fidia kwa ajili ya kutafuta wawekezaji wengine wenye mtaji wa kutosha watakaoyaendeleza mashamba hayo. Hali kadhalika, kwa yale mashamba ambayo tayari yana wakulima wadogowadogo wanaoendesha shughuli zao za kilimo, Serikali ipange utaratibu wa kuwamilikisha wananchi maeneo husika ili kuondokana na ile dhana ya uvamizi au kukodishwa ardhi kwa ajili ya kilimo. Zoezi hili lazima lifanywe kwa uwazi ili kuepuka udanganyifu uliotokea katika maeneo mengine ya nchi ambapo vigogo na watu wenye nafasi zao walijitwalia ardhi wakijifanya na wao ni sehemu ya wanakijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba yaliyopendekezwa kurudishwa kwa wananchi Mkoa wa Arusha. Tarehe 17/6/1997 na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Ndugu D. Ole-Njoolay, aliitisha kikao kilichohudhuriwa na Ndugu Kileo – Katibu Tawala Mkoa, Ndugu P.H. Muhale - Afisa Maendeleo ya Ardhi

(M), Ndugu E. K. E. Makere – Afisa Ardhi na Ndugu Z.M.S Meirish – Afisa Ardhi. Kikao husika kilichofanyika saa 4.35 asubuhi kilikuwa mahsusi kwa kuchambua mapendekezo yaliyoletwa kutoka Wilayani kuhusu taarifa za mashamba makubwa Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba yaliyojadiliwa na kufikia maamuuzi mbalimbali yalihusisha Wilaya sita kama ifuatavyo:-

(i) Wilaya ya Arumeru- Mashamba 18;
(ii) Wilaya ya Ngorongoro- Mashamba 10;
(iii) Wilaya ya Babati – Mashamba 11;
(iv) Wilaya ya Simanjiro – Mashamba 2;
(v) Wilaya ya Karatu –Mashamba 6; na
(vi) Wilaya ya Monduli – Mashamba 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakala ya majina ya mashamba pamoja na hatua zilizopendekezwa, nimeziambatanisha kama sehemu ya hotuba hii. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili Tukufu nini mustakabali wa mashamba 83 na hatua zilizochukuliwa kufuatia kikao husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1999, ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, kupitia barua yenye kumb. Na. RC/AR/ CL 2/3 Vol IV/19 ilimwandikia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Arumeru ikimtaarifu juu ya mashamba 11 ambayo yamepata kibali cha Rais kufuta miliki. Taarifa ambayo ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilipata toka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi kwa barua yenye Kumb. Na. CL/46/VOL III ya tarehe 1 Juni 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba hayo:-

(1) Shamba namba 78 na 79 - *NAIC , Usa River.*
(2) Shamba namba 90 na 91- *Madiira Coffee Limited.*
(3) Shamba namba 98/2/1 – *Duluti New – Duluti Lodge.*
(4) Shamba namba 218/2- *Maua Limited.*
(5) Shamba la Oljoro – *Salama Estate.*
(6) Shamba la Unit 15 *Oljoro – Iman Estate.*
(7) Karangai Sugar Estate *(Tanzania Plantation).*
(8) Shamba Namba 3 – *Milimani Farm.*
(9) Shamba la Nduruma- *Lucy Estate.*
(10) Shamba la Nduruma – *Umoja Sisal Estate.*
(11) Shamba la *Dolly – Dolly Estate - Flycatchers* (ambalo limegeuzwa uwanja wa Gofu na shamba la wanyama kinyume na maagizo ya Rais).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itupe maelezo ya kina kuhusu mashamba haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi. Kama ambavyo tulifanya katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kambi ya Upinzani itakuwa na utaratibu wa kila mwaka wa fedha kuianishia Serikali migogoro mbalimbali ya ardhi inayolikumba Taifa letu. Ni jukumu la Serikali kupitia vyombo vyake kuhakikisha kwamba inafuatilia migogoro hii kwa kina na hatimaye kuitafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bagamoyo - Mkoa wa Pwani. Wananchi wa kijiji cha Milo chenye vitongoji

vitano; Milo, Relini, Kengeni, Kisiwani na Migude, kilichoandikishwa chini ya Sheria ya Kijiji (chenye shule ya msingi na zahanati na kijiji) wanailalamikia Kampuni ya *Noble-Azania Agricultural Enterprises Limited* ambayo inadai ni wamiliki halali wa eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 3000. Eneo ambalo limekimeza kitongoji cha Migude na sehemu ya kijiji cha Milo. Kwa upande mwingine, Kampuni ya Azania, inadai wanakijiji hao ni wavamizi kwa kuwa wao wanaumiliki halali wa eneo husika kupitia umiliki namba 36911.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mpanda – Katavi. Mkoa mpya wa Katavi, anakotoka Waziri Mkuu, ni kati ya maeneo yenye migogoro mingi sana ya ardhi, mingi ikiwa ni migogoro sugu, ambayo imeshindwa kutafutiwa ufumbuzi licha ya malalamiko kufika ngazi za juu Serikalini pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Migogoro inazihusu Kata za Kabwe, Korogwe na kijiji cha Nkungwi. Katika kijiji hiki cha Nkungwi wanakijiji waliporwa ardhi (heka 3000) na kikundi kinachojiita Mpairo. Ni mgogoro ambao unaendelea kutokota chini kwa chini lakini kwa mujibu wa wananchi unaweza kuzua mauaji kwa sababu unashabihiana na mgogoro uliosababisha mauaji ya kutisha ya tarehe 21/5/2012 kati ya kikundi cha nguvu kazi kinachoendeshwa na Galas Kasonso chini ya kivuli cha baadhi ya wakubwa Wilaya ya Mpanda. Vijiji vingine ni kijiji cha Kabange, Kijiji cha Mbuguni, mgogoro baina ya hifadhi ya Ubende na vijiji kumi na nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawasilisha mezani kwako nyaraka mbali mbali za migogoro hii, kama Serikali itaona inafaaa, iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, nitaelezea mgogoro mmoja sugu, ambao unahusisha watendaji Serikalini. Mgogoro ambao unaambatana na vitisho kwa wananchi, mpaka kufikia hatua wananchi kufunguliwa kesi za jinai ili kuwatisha. Mfano kesi namba CC.204/2011, CC.207/2011 na Pl. 16/2011. Rejea pia barua toka ofisi ya Mkurugenzi wa mashtaka yenye Kumb.Na. J/C.110/9/322 kwenda kwa wakulima wa kijiji cha Sibwesa, Kitongoji cha Kabange, unaohusu wananchi kubambikiwa kesi ya mauaji. Wananchi wa Kata ya Sibwesa, Wilaya ya Mpanda, wanalalamikia mtandao ambao umeundwa na watumishi wa Serikali, ambao ni waajiriwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, wanaofahamika kama Cletus Siwezi, Andrea Malando (Kitengo cha Ardhi) na Bwana Galus Kasonso (Meneja wa Mradi wa Maji katika Halmashauri ya Mpanda). Watumishi hawa wanalalamikiwa na wananchi, wakituhumiwa kuwanyang'anya mashamba yao kwa kutumia nafasi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi huyu wa Serikali (kupitia kwa bwana Ramadhani), alishindwa kuthibitisha umiliki wake katika Baraza la Ardhi la Kata, walikimbilia Baraza la Ardhi na Nyumba la Sumbawanga ambapo ilitolewa hukumu ya upande mmoja. Baada ya hukumu hiyo ya upande mmoja, kumekuwa na hujuma dhidi ya wananchi na kuna malalamiko kwamba kuna mbinu ya kuandikwa hati ya kukamata heka mia tatu na sitini (360) kutoka mbuga

ya Mwamapuli, kijiji cha Kabage na mbinu yake ya kuendelea kufanya mipango ya kukamata watu bila ya kuwa na kosa kwa kutambua kuwa hawana uwezo wa kukabiliana na kesi za jinai. Jeshi la Polisi linahusishwa pia katika mazingira mawili, la kwanza kufungua kesi za kubambikiza, hali kadhalika kumlinda mhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yanayotokea Mpanda, yanafanyika pia kwenye maeneo mengi ya nchi hii, kwa watu ambao wamepewa dhamana kutoa huduma hii muhimu kwa wananchi, kutumia fursa hiyo kujilimbikizia ardhi na pale ambapo wananchi wa kawaida wenye uhitaji wa huduma hiyo wanapojitokeza hukumbana na urasimu mkubwa uliotawaliwa na rushwa. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ijipime kwa kuangalia ni hatua gani stahili itawachukuliwa watumishi hao wa Halmashauri kama ushahidi ulivyotolewa na pengine inaweza pia kubaini mambo mengi mazito yaliyojificha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara - Babati. Mgogoro huu unahusu hifadhi ya Taifa Tarangire na Vijiji vya Gijedabung, Ayamango ambacho kilisajiliwa tarehe 1/4/1976 kwa usajili namba AR.KJ 26 na Gedamar ambacho kilisajiliwa tarehe 1/4/1976 kwa usajili namba AR.KJ43. Vijiji hivi vilikaliwa na wananchi toka miaka ya 1960. Hifadhi ya Tarangire ilianzishwa mwaka 1970 kwa kuzingatia Tangazo la Serikali (GN) Na. 160. Mipaka yake ilitambulishwa kwa barabara iliyozunguka hifadhi nzima na kuipatia umbo linaloonekana katikati yake kupitia Sheria ya mwaka

1974 ya Vijiji na Vijiji vya Ujamaa, mpaka ambao wananchi wote waliutambua na kuuheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro ulianza baada ya uongozi wa Hifadhi ya Tarangire ulipotekeleza zoezi lake la kuhakiki mipaka yake kwa nia ya kufanya tafsiri yakinifu kwa kutumia vifaa vya kisasa. Wataalam walibaini kwamba ule mpaka wa miaka yote wa barabara, ulioliwekwa na Mamlaka ya Hifadhi yenyewe haukuzingatia vipimo halisi na hivyo kusababisha eneo lenye ukubwa wa ekari 16,249.10325 kuingizwa kwenye mamlaka ya vijiji kimakosa. Kwa mantiki hiyo, hifadhi iliamuru wananchi waliokuwa wakiishi kwenye ardhi hiyo kuhama mara moja na kusitisha matumizi yote juu ya ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na amri hiyo, wananchi wengi wa maeneo haya wako katika hali mbaya sana kiuchumi kutokana na ardhi waliyokuwa wanaitegemea kuchukuliwa na Serikali. Wananchi wamezuiwa kufanya kitendo chochote cha kufanyia matengenezo makazi yao walioishi kwa zaidi ya miaka 50. Ikumbukwe kwamba wananchi hawa hawakuvamia eneo hili bali waliwekwa na mamlaka ya Wilaya kwa makosa pasipo kukusudia. Pamoja na Serikali kutaka kuwahamisha wananchi hao haijafanikiwa kuwapatia makazi mapya na mashamba ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usumbufu wa Askari wa Hifadhi ya Tarangire wanaofanya vitendo vya unyanyasaji, ni kero kubwa kwa usalama, utulivu na ustawi wa wananchi wa maeneo husika. Kambi ya

Upinzani haidhani kwamba hifadhi ni muhimu zaidi kuliko Watanzania walioiweka CCM madarakani. Ni rai yangu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, awatazame wananchi wa maeneo haya kwa jicho la huruma. Awatazame wananchi wa maeneo haya kwa jicho la huruma kutokana na kwamba hawana maeneo mbadala ya kuishi ili kuendeleza maisha yao. Rais wa Jamhuri ya Muungano ana mamlaka ya kuhawilisha ardhi ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire inayokaliwa na wananchi wa vijiji tajwa ili iwe ardhi ya kijiji, ombi ambalo lilishawasilishwa Wizara ya Ardhi Nyumba na Makazi, lakini mpaka leo hakuna majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa Wa Kagera - Wilaya ya Karagwe. Muda sasa Kambi ya Upinzani, pamoja na Wabunge wengi, wamekuwa wakizungumzia juu ya mgogoro baina ya wakulima na wafugaji, kutokana na Serikali kutokuwa na mpango endelevu wa kutenga maeneo ya wakulima na wafugaji. Mwaka jana katika hotuba ya Kambi, tulielezea juu ya mgogoro wa wakulima na wafugaji wa jamii ya Wamasai katika eneo la vijiji vya Izava (Chamwino) na Chitego (Kongwa). Mgogoro huu mpaka leo hujapatiwa ufumbuzi. Kimsingi mgogoro ulisababishwa na ubabe na maamuzi mabovu ya Mkuu wa Wilaya. Katika hotuba hii, Kambi ya Upinzani inafikisha mbele ya Bunge lako Tukufu kilio cha wanavitongoji vya Karugwebe, kijiji cha Iteera na kitongoji cha Mtakuja kijiji cha Chanya, Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanalalamikia kufukuzwa kwenye maeneo yao ya kilimo na kupewa wafugaji matajiri bila wao kuhusishwa. Baada ya

kufukuzwa, hawakupewa hifadhi, kitu ambacho kimewafanya wawe wahamiaji wasio rasmi ndani ya nchi yao. Ikumbukwe wananchi hawa walikuwa wanafanya shughuli za kilimo kwa kipindi cha zaidi ya miaka 20. Madiwani walipohoji katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 31/2/2012, walipata vitisho kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Misenyi aliyekuwa anakaimu ukuu wa Wilaya ya Karagwe. Kambi ya Upinzani inataka kauli ya Serikali kuhusiana na matukio haya mawili; hali kadhalika Serikali ilitaarifu Bunge lako Tukufu, ni lini Serikali itaandaa mpango rasmi wa matumizi ya ardhi kwa wakulima na wafugaji ili kuepuka migogoro isiyokwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar- Es-Salaam. Maeneo ya pembezoni. Miaka ya hivi karibuni, Serikali imekuwa na mikakati, inayoitafsiri kama mikakati kabambe ya kuendeleza maeneo yaliyomo pembezoni mwa jiji la Dar es Salaam. Mipango hiyo imeleta msiba mkubwa sana kwa wananchi wa maeneo hayo. Kwa sababu ya muda, tutazungumzia miradi ya Luguruni na Kwembe Kati, Kinondoni Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo haya, wananchi wameporwa ardhi yao yote kwa fidia ndogo sana, wamebomolewa makazi yao na kutimuliwa kutoka kwenye ardhi yao kwa nguvu ya dola, wakiwa wamemaskinishwa kupindukia baada ya kuporwa rasilimali ardhi yao na wakiwa na fidia duni mkononi, wakihamia kwingineko kuanzisha makazi yasiyopimwa na ya kimasikini kupindukia. Miradi hiyo imegubikwa na utendaji wenye kupindisha sheria, ubabe, usio na

utawala bora, uliototeresha viwango vya ramani na upimaji uliochakachua fidia, uliofanya ofa na hatimiliki kuwa uyoga, uliojaa dhuluma na hujuma dhidi ya hakiardhi ya wananchi. Hapo Luguruni tarehe 22/5/2007, Mkurugenzi wa Makazi na Ardhi, alitangaza utwaaji wa ardhi wa 5% ya ardhi kwa ajili ya miundombinu. Hali hii ilibadilika kufikia 100% na waliofanya hivyo ni watendaji wa mradi baada ya Mkurugenzi husika kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kinachofanyika Kwembe Kati, kwa maeneo ya miundombinu, biashara na makazi yalitwaliwa na Mradi na kutangazwa kuwa mali ya Serikali, licha ya tamko la Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Chiligati Bungeni la tarehe 18/06/2009 na tamko la Naibu Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye Bungeni tarehe 12/11/2011 kusisitiza ya kwamba baada ya Rais kutwaa ardhi na miundombinu albaki ya ardhi kwa ajili ya makazi na biashara ibakie mikononi mwa wananchi wamiliki wa ardhi, waiendeleze wao wenyewe ili waweze kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo yote hayo, baada ya ardhi yote ya wananchi kutwaliwa kwa fidia duni chini ya 20% ya bei ya soko kinyume hata na matakwa ya Sheria ya Ardhi, Namba 4 ya mwaka 1999, sehemu ya II, kifungu cha 3 kinachoelezea misingi mikuu ya sera ya ardhi ya Taifa, wananchi walitimuliwa kimabavu baada ya makazi yao kubomolewa kwa tingatinga. Mfano dhahiri ni wa eneo la Luguruni; fidia iliyolipwa kwa mita moja ya mraba ilikuwa ni shilingi 1,977, ardhi hiyohiyo iliuzwa

kwa Tsh.30,000 mita moja ya mraba bila maendelezo yoyote. Hivyo kuzalisha faida ya 1500% ...Huu ni wizi na unyonyaji mkubwa. Inasikitisha sana pale watendaji wa Wizara ya Ardhi, wanapotumia mgongo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutengua toleo la hatimiliki halali za wananchi wamiliki wa ardhi, kupora ardhi yao kwa mtindo huu, kupima viwanja vipya juu ya viwanja vya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka Serikali hii ya CCM, kuacha kufanya mambo kibabe na kusitisha kile kinachoendelea katika maeneo ya Luguruni na Kwembe Kati. Ulipaji fidia unakuwa na mianya lukuki ya ubadhirifu wa fedha, hivyo kuhitaji ukaguzi na udhibiti wa makini sana wa masuala yote ya malipo na matumizi ya fedha kwenye miradi ya Luguruni na Kwembe Kati. Viwango vya fedha vinavyohusika hapa ni vikubwa sana kutokana na wingi wa watu wanaohitaji kufidiwa na kutokana na mauzo ya viwanja vilivyopatikana katika mchakato mzima wa kutwaa na kuuza ardhi, kuna uhitaji mkubwa wa ukaguzi na udhibiti mahsusi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Suala la ukaguzi ni muhimu kutokana na tuhuma kwamba malipo ya fidia yamefanywa bila kutumia nyaraka halali za matayarisho na ulipaji fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uvamizi wa maeneo ya watu. Kuna tabia iliyozuka kwa kasi sana, katika Manispaa ya Kinondoni, hususan maeneo ya pembezoni na katika Jimbo la Kawe; ninaloliwakilisha, tabia hii imekithiri sana Kata za Bunju, Mabwepande na

Wazo. Kumekuwa na genge la watu wenye silaha wanaovamia maeneo ya watu, kuharibu mali, kugawa viwanja na kuwauzia watu (wapya) viwanja kwa bei ya kutupa. Hilo genge, baada kufanya uharibifu eneo moja, huhamia eneo lingine. Hali hii imesababisha uvunjifu wa amani na katika mazingira mengine kusababisha vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu ya wananchi inaongezeka kutokana na kutokupata ushirikiano kutoka kwa mamlaka zenye jukumu la kuhakikisha wananchi na mali zao wako katika hali ya usalama. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Mkoa wa Dar es Salaam, zote zina taarifa ya genge hili la majambazi wa ardhi, vyombo mbalimbali vya habari vimetoa taarifa kuhusu genge hili la majambazi, hakuna hatua zilizochukuliwa na wala hakuna dalili kama kuna dhamira ya dhati ya kuweza kutafuta suluhu. Ni dhahiri kwamba Serikali ingejipanga katika matumizi bora ya ardhi na kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata ardhi kwa gharama nafuu bila urasimu wala rushwa, hili genge la majambazi wa ardhi lisingepata wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze Bunge ina mipango gani ya muda mfupi na mrefu kuweza kukomesha kabisa suala la uvamizi wa maeneo ya wazi. Nikiwa Mbunge wa Kawe, napenda kuwasisitizia wamiliki wote wa ardhi Jimbo la Kawe, Serikali ya Wilaya kupitia Kamati yake ya Ulinzi na Usalama imeshindwa kuwapa ulinzi wenu na mali zetu. Niendelee kuwashawishi kila mmoja kwa nafasi yake mmoja mmoja au kwa vikundi kuweka

walinzi binafsi kwa ajili ya kulinda mali zao na chochote kikitokea Mbunge wenu nitawalinda kwa sababu nilishatoa taarifa kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa mpaka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majiji ya Viungani *(Setelite Towns).* Mwaka 2006/2007, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikishirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake tatu ilianzisha mkakati wa kuanzisha miji midogo sita itakayokuwa na vituo vya huduma za kijamii na za kibiashara. Kutokana na ukubwa wa mpango huo, iliamuliwa kuwa utekelezaji uanze katika eneo la Kibamba Luguruni ambalo lilipaswa kuwa eneo la mfano ambapo uzoefu katika uendelezaji ungetumika kwa maeneo mengine ya Jiji na nchi nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Mji wa Kibamba uligawanywa katika maeneo makubwa matatu; eneo Kitovu cha Mji cha Luguruni, eneo la makazi mbadala la Kwembe Kati na uendelezaji wa eneo linalozunguka kituo. Hata hivyo, miaka zaidi ya mitano imepita bila uendelezaji huo kukamilika na hivyo sehemu kubwa ya maeneo tajwa kurejea kuwa mapori na kuanza kurejea kwa migogoro ya ardhi katika maeneo tajwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa mpango huo na kueleza bayana kasoro na matatizo yaliyojitokeza sambamba na kuharakisha ujenzi wa mji husika ili kuwa mfano kwa mipango ya ujenzi wa miji mingine ambayo maandalizi yake

yanaelezwa kutaka kufanyika katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati zoezi la wa Luguruni, Kwembe Kati na Kigamboni yakitawaliwa na malalamiko makubwa sana kutoka kwa wananchi, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi imeandaa mpango mpya wa Makongo. Mradi huu utasimamiwa na mtendaji aliyeendesha zoezi la kihuni la ujenzi mpya wa mji wa Kigamboni. Kambi ya Upinzani inaona mradi huo umeanza vibaya kwani msimamizi wake mkuu haaminiki kutokana na miradi aliyoisimamia huko nyuma. Hivyo basi, inaitaka Serikali ikutane na wananchi na majirani zake wa Makongo tulijadili hili kwa kina. Kutumia mabavu hakutasaidia. Wananchi wa Makongo wanataka maendeleo, lakini yasiwe maendeleo yenye lengo la kuwapa mzigo, ufukara na kuwahamisha wale ambao hawatakuwa na uwezo wa kukidhi matakwa ya mradi. Nasisitiza mimi ni Mbunge wako, njoo tuzungumze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwindaji, ufisadi na ukiukwaji wa Sheria za Matumizi ya Ardhi. Kwa muda mrefu sasa, ardhi ya Tanzania imegeuzwa shamba la bibi na kikundi cha mafisadi. Kambi ya Upinzani imeshuhudia mkataba ulioingiwa baina ya kampuni za U*ranium Resourses PLC, Western Metals Limited* na *Game Frontiers of Tanzania Limited.* Mkataba ambao umetengenezwa na Kampuni ya Kitanzania ya *Rex Attorneys* na ulisainiwa tarehe 23.3.2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba husika ambao vipengele vyake vinaainisha kwamba unatakiwa uwe

wa SIRI, unaihusu kampuni ya uwindaji inayofahamika kwa jina la G*ame Frontiers of Tanzania Limited* inayomilikiwa na Bwana Mohsin M. Abdallah na Ndugu Nargis M. Abdallah. Kampuni hii ya uwindaji, imeingia mkataba na kampuni mbili za kigeni, za kufanya utafiti wa uchimbaji wa madini ya *Uranium* katika kijiji cha Mbarang'andu kwa malipo yafuatayo:-

(a) Malipo ya $6,000,000/- za Kimarekani ambazo zitalipwa kwa awamu mbili ya malipo ya $3,000,000. Malipo ya kwanza yatafanyika pale uzalishaji wa urani utakapoanza.

(b) Malipo ya $250,000/- baada ya kampuni za madini kukamilisha utafiti wa madini ya urani na kupata kibali cha uchimbaji wa madini.

(c) Malipo ya $55,000 kila mwaka kama fidia ya kushindwa kufanya biashara na usumbufu unaotokana na shughuli za machimbo kwenye kitalu. Malipo hayo yatafanyika kila tarehe 31 Machi.

(d) Malipo ya $10,000 kwa vijiji vitakavyoathiriwa na utafiti huo wa urani. Malipo ambayo yametokana na makubaliano baina ya kampuni ya uwindaji na kampuni za madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Sheria za Uhifadhi wa Wanyamapori, *The wildlife Conservation Act, 1974* (Sheria ya zamani) na Sheria mpya *The wildlife Conservation Act, Act no 5 of 2009*. Sheria hizi zinamruhusu mtu aliye na leseni ya uwindaji, kuwinda wanyama tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, Sheria Na.4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sheria Na.5 ya mwaka 1999 inatamka bayana kwamba ardhi inajumuisha vitu vyote vilivyo juu ya ardhi na chini ya ardhi isipokuwa madini au mafuta... na kwa mujibu wa sheria za Tanzania linapokuja suala la madini, umiliki unatoka kwa mtu binafsi na kurudi Serikalini na ni Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ndiyo pekee yenye mamlaka ya kutoa leseni ya kutafuta madini kwa kampuni za madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu uhalali wa mkataba kati ya *Game Frontiers* na *Uranium Resourses PLC* na *Western Metals*. Ni sheria ipi inayoipa kampuni ya uwindaji haki ya kualika kampuni ya nje kwenye eneo ambalo haina umiliki kufanya utafiti na hatimaye kuchimba madini hatari kama urani? Nini mustakabali wa Watanzania wanaoishi kwenye vijiji vinavyozunguka mbuga hiyo ambao wanaishi maisha yao ya kila siku pasipo kujua kama kuna utafiti wa madini hatari ya urani unaoendeshwa kwa siri kubwa? Ni Serikali ya aina gani, yenye uwakilishi mpaka ngazi ya kitongoji na usalama wa taifa mpaka ngazi za chini kabisa za utawala inashindwa kuyaona haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kutoa ardhi kwa wawekezaji. Uchunguzi uliofanywa na Haki Ardhi umebaini kuwa katika Wilaya ya Kilwa, mwekezaji alikuwa na kampuni iitwayo Bioshape kutoka nchini Uholanzi. Kampuni hii ilipewa ardhi yenye ukubwa wa

hekta 80,000 kwa lengo la kulima zao la mbono kaburi, ardhi hiyo ilihusisha vijiji vinne ambavyo ni Mivuji, Migelegele, Liwili na Inokwe. Mwekezaji hakutumia eneo lote na kulima hekta 800 tu katika kijiji cha Mavija ambazo ziligeuka kuwa pori baada ya mwekezaji kutelekeza shamba, vifaa na wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kisarawe, mwekezaji alikuwa ni kampuni inayoitwa *SunBiofuels* kutoka nchini Uingereza. Kampuni ilipewa ardhi ya ukubwa wa ekari zipatazo 9000 iliyojumuisha ardhi za vijiji 11 ambavyo ni Marumbo, Muhaga, Mtamba, Mzenga A, Kurui, Chakenge, Mitengwe, Paraka, Kidugalo, Vilabwa na Chakaye. Mwekezaji huyu hakulima shamba lote bali alilima shamba la mfano katika eneo la ekari zipatazo 3000 lililopo kijiji cha Mtamba ambalo lilikuwa na mazao ambayo mengi yameanza kuzaa matunda huku yakiwa tayari kwa kuvunwa, pia Bagamoyo kampuni iliyohusika inaitwa *Sekab Bioenergy Tanzania Limited*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke kuwa katika maeneo yote ardhi zilikuwa za aina mbili; zilizomilikiwa na wanakijiji na zile za vijiji ambazo zilipaswa kuhawilishwa kwanza na kisha kutolewa kwa mwekezaji. Kwa jumla, wananchi katika vijiji, watendaji wa vijiji, wajumbe wa Kamati za Vijiji kwa pamoja walisema hawakuridhika na mchakato uliotumika kutoa ardhi kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasikitika mchakato kujaa mizengwe, hadaa, utapeli kwa wananchi na hata harufu ya rushwa kwa baadhi

ya watendaji wa vijiji, maofisa ardhi katika Wilaya na vigogo wa juu katika Wilaya na Halmashauri. Hata pale ambapo wananchi walirubuniwa kutoa ardhi zao kwa kuelezwa kuwa mwekezaji ataleta neema katika maeneo yao, bado fidia hazikuwafikia, zilichelewa au fidia iliyotolewa ilikuwa ndogo, huku zoezi la kutathmini mali zilizopo katika ardhi zao likiwa siyo la wazi na shirikishi. Hata vigezo vya tathmini kwa ardhi na mazao havikuwekwa bayana kwa pande husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani kwa niaba ya wananchi inaitaka Serikali kuzingatia sheria na kusimamia utekelezaji wake kwa ngazi mbalimbali kwa kuwatendea haki wananchi kuwapa huduma zenye uhalali kisheria ikizingatiwa fidia zilizotolewa hazikurandana na hali halisi ya soko kwa wakati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika hotuba yake hapa Bungeni kupitia Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi mwaka wa fedha 2011/2012 ilikiri kuwa na changamoto ya kutokuwa na mfumo thabiti na utunzaji wa kumbukumbu za sekta ya ardhi na kutoa ahadi ya kujenga mfumo mmoja wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi kwa njia ya kielekroniki *(Integrated Land Management System)* utakaounganisha mifumo yote ya utunzaji wa kumbukumbu za sekta ya ardhi. Kambi ya Upinzani inaitaka serikali kueleza wananchi mfumo huu umefikia wapi na utekelezaji wake uko je?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tatizo la ardhi kwa maana ya uwekezaji na matumizi mbalimbali ya Serikali kutopatikana kwa urahisi mijini na

vijijini, Serikali kupitia Wizara iliahidi hapa Bungeni kuanzisha chombo kitakachosimamia Hazina Ardhi *(Land Bank)* ili kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya miradi ya uwekezaji na kuunda Mfuko wa Kulipa Fidia *(Land Compensation Fund)* kwa mujibu wa Sheria za Ardhi ili kuiwezesha Serikali kulipa fidia timilifu na kwa wakati inapotwaa ardhi kwa maslahi ya umma. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu kutoka kwa Serikali ni hatua gani ziliendelea kuchukuliwa ikizingatiwa kuwa tatizo la fidia limeendelea kuwepo na kuwa kero kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya nyumba. Sekta hii ni sekta pekee inayoweza kuleta na kutekelezwa kwa dhana nzima ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Nchi yetu na Watanzania kwa ujumla bado tuna matatizo makubwa ya nyumba bora na za bei nafuu kutokana na bei kubwa ya simenti na bati - bidhaa muhimu katika kutimiza azma ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema na tunasema kuwa bei ya simenti na bati inaweza kuwa chini ya shilingi elfu saba, kama Serikali itakuwa na utashi wa kuwahudumia wananchi kwa dhati. Bei ya simenti Uturuki na Paksitani ukinunua tani 600,000 bei ya tani moja ni dola za Marekani 70 hadi bandarini. Guangzhou – China tani moja ni dola za Marekani 26. Kwa hesabu za kawaida kwa mfuko mmoja ni dola 3.5 sawa na shilingi 5250/- kama ukinunua Pakstani au Uturuki. Ukinunua China bei itakuwa dola 1.3. sawa na shilingi 1950/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani bado inasisitiza kuwa kama Serikali ina dhamira ya kweli mfuko wa simenti hauwezi kuuzwa zaidi ya shilingi 7,500. Hivyo basi tunaitaka Serikali itueleze kwa nini bei ya simenti inauzwa zaidi ya shilingi 14000 Dar es salaam na nje ya Dar es Salaam bei ni zaidi ya hapo, wakati malighafi zinapatikana hapa hapa nchini na kiwanda kikubwa cha simenti kinatumia gesi asili ili kupunguza gharama za umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza gharama hizi na ni faida kiasi katika kodi tunayopata kwa kuwalangua Watanzania. Serikali haioni kwamba ina wajibu wa kuondoa hizi kero wananchi wajenge nyumba bora na kwa bei nafuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa. Shirika la Nyumba la Taifa, lilipoanzishwa mwaka 1962, moja kati malengo yake ilikuwa ni kujenga nyumba za bei nafuu kwa ajili ya Watanzania wafanyao kazi mijini. Hata hivyo, kwa kadiri siku zilivyosonga mbele, Shirika hili liligeuka kutoka kuwahudumia maskini na watu wenye kipato cha kati na badala yake linawahudumia watu wa kipato cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa linahudumia asilimia 0.5 tu ya Watanzania wote wa nchi hii. Swali la msingi ni je Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha kuwa Shirika hili linahudumia Watanzania wengi zaidi kwa kuwapatia nyumba za bei nafuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kambi Rasmi ya Upinzani imepata taarifa kuhusu ujenzi inaoendelewa kufanywa na Shirika la Nyumba katika maeneo mbalimbali nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Wizara kutoa maelezo kwa umma kuhusu migogoro iliyojitokeza kati ya Shirika na wapangaji na hatua ambazo zimechukuliwa kushughulikia malalamiko yaliyotolewa hususan katika maeneo ya Chang'ombe, Ubungo na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* na Ongezeko la Mtaji *(Capital Gain Tax) k*wenye Mauzo ya Nyumba Zinazojengwa na Shirika. Changamoto kubwa inayowakabili Watanzania wengi ni kuweza kupata nyumba za bei nafuu. Suala hili tulilizungumza mwaka jana na tutaendelea kulizungumza. Kwa Sheria zetu za Kodi, nyumba mpya iliyojengwa kwa ajili ya kuuzwa inapaswa kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* pale inapouzwa na anayelipa kodi hiyo ni mnunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi ni kuwa nyumba hiyo wakati inajengwa vifaa vyote vya ujenzi vililipiwa kodi hiyo, hivyo kitendo cha mnunuzi kulipa kodi ya *VAT* wakati wa kununua nyumba hiyo ni kulipia kodi mara mbili *(Double Taxation)*. Je, Serikali haioni kama haimsaidii mwananchi kuweza kuishi kwenye nyumba nzuri na kwa gharama iliyo nafuu? Mfano dhahiri ni kwamba kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Shirika lilitarajia kujenga nyumba 49, zenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 4.08. Kwa gharama iliyotumika, wastani wa nyumba moja ililigharimu Shirika shilingi milioni 83.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa Kazi za Shirika la Nyumba la Taifa kuanzia Julai 2010 hadi Mei 2011 walitarajia kupata shilingi bilioni 6.3 kutokana na mauzo ya nyumba hizo, yaani faida ya shilingi bilioni 1.9 Kwa tafsiri nyingine nyumba moja itauzwa na Shirika la Nyumba kwa shilingi milioni 129.2, wakati gharama halisi za ujenzi ni shilingi milioni 83. Kwa kila nyumba iliyouzwa Shirika limepata faida ya shilingi milioni 46.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mikopo yaani *"Government Loans, Guarantees and Grants Act 1974 and amendments 2003"* inalifanya Shirika la Nyumba la Taifa kulazimika kupata kibali kutoka Wizara ya Fedha hata pale ambapo halihitaji kupata dhamana ya Serikali na pia hata kwa mikopo ya ndani ya nchi. Wote tunafahamu rasilimali ambazo Shirika hili linazo. Pamoja na kufahamu yote, bado tumeamua kuliweka Shirika hili katika urasimu mkubwa wa Kiserikali wa kupata vibali kutoka Wizara ya Fedha bila ya sababu za lazima. Je, Serikali imedhamiria kutekeleza ahadi zake katika ujenzi wa nyumba na kuliwezesha Shirika kujiendesha kibiashara kama sheria yake inavyolitaka? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe ufafanuzi ni lini inatarajia kuanzisha mchakato wa kurekebisha sheria hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka/Wakala wa Kuratibu Bei za Pango la Nyumba. Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2011/2012, tuliitaka Serikali kuanzisha chombo kitakachoweka utaratibu utakaotambulika kisheria ili kiwe kinatoa

miongozo ya kudhibiti gharama za kodi za nyumba kwa ujumla wake. Kwa maana nyingine ni kuanzisha mamlaka ya udhibiti itakayoitwa *"Real Estate Regulatory Authority"*. Tunarudia tena kusisitiza ushauri wetu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ambayo imejaa changamoto ambazo kama zikifanyiwa kazi ni dhahiri pato la taifa litaongezeka na pia tatizo la ajira linaloikabili nchi yetu linaweza kupungua kwa kiasi kikubwa kama si kuondoka kabisa. Swali muhimu la kuuliza ni kwa vipi Serikali itabadilidha changamoto kuwa fursa? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia kwa makini kuwa mamlaka ya udhibiti ndiyo inayoweza kubadilisha changamoto zilizopo katika sekta hiyo kuwa fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa kwa Taarifa yako nzuri. Kwa vile muda wetu umebaki kidogo sana, naomba nimwite mchangiaji mmoja tu kwa asubuhi hii, tukirejea tutaendelea. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Dokta Augustine Lyatonga Mrema, Mheshimiwa Mrema!

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa heshima hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi matatizo nitakayoyazungumzia kuhusiana na Wizara hii, ni kuhusu migogoro ya ardhi iliyo katika Jimbo langu. Mwaka jana, Mheshimiwa Waziri, utakumbuka kuna vijana wa Kimasai walikuja Ofisini kwako wakilalamika wamekuwa wanawindwa na Polisi, wanabambikiziwa kesi na hao ni vijana wa Kahe, Kijiji cha Mawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lao ni kwamba, wameamua kulinda rasilimali ardhi yao. Serikali mlifanya vizuri pale Mawala, Kahe, mkatenga eneo la wafugaji na eneo hili limetengwa tangu mwaka 1973 na liko kwenye ramani lakini matajiri wamevamia, wamechimba visima; wale vijana wa Kimasai wakijaribu kulinda lile eneo lao, sasa ndio kesi ambayo inawahangaisha, inawatesa. Serikali yote inajua eneo lile, mliwapa nyie, mnalifahamu, lakini hakuna mtu anayewasimamia, hakuna mtu anayewatetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwamba, Serikali, ilitenga eneo la kilimo na kuleta maji kwa ajili ya wanavijiji lakini naomba nikufahamishe, Wanasiasa Mashuhuri wa Mkoa ule, yaani badala ya kutuletea Viongozi wenye uchungu na watu, mnatuletea watu wanaotafuta mashamba. Mkuu wa Wilaya aliyeondoka, amekwenda pale amechukua heka zake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri amechukua heka zake, yaani wamegawana heka 100, watu wenye nguvu, wenye pesa. Sasa wale Wamasai pale wanahangaika, hawajui ni nani atawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mkuu wa Mkoa, tumekwenda pale na yeye, walipohojiwa

wakasema hakuna Mkutano Mkuu wa Kijiji ulioidhinisha Mkuu wa Wilaya kupewa shamba wala Mkurugenzi kupewa shamba, wala madereva wake, hizo heka 100; katika kijiji kile, tuna vijana 100 hawana ajira, hawana shamba. Ndio mambo yanayofanyika Mheshimiwa Waziri; kilio cha watu wa Mawala, Kahe, utawasaidiaje? Tangu wewe umewaandikia barua waende kwa *DC,* nikakwambia huyu *DC* ni sehemu ya mgogoro na Mkurugenzi ni sehemu ya Mgogoro. Nashukuru Rais, kwa kumteuwa Mkuu wa Mkoa Mpya, Mkuu wa Wilaya Mpya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri yetu angalau sasa tuna amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tatizo la Mawala, Mheshimiwa Waziri na wale vijana bado wanahangaika, ardhi ni yao, watu wenye fedha wanawavamia, Serikali mpo, hamuwatetei. Wamebambikiziwa kesi, kesi imebidi tukawachangishe wale Wamasai, kesi iko Mahakamani, wanahangaika, lakini wenye kesi ni wale waliovamia shamba la kuchunga mifugo. Sasa hawa Wamasai waende wapi? Kwa hiyo, nakuambia Mheshimiwa Waziri, ile barua uliyoniandikia haijatekelezwa. Wale Wamasai hawajapata haki zao, bado wanahangaika, hawajui waende kwa nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimshukuru Naibu Waziri, Goodluck Ole-Medeye. Kuna tatizo la Mji wa Himo, naomba uniambie leo kama ule ni Mji au ni Kijiji na ni nani anayepima Mji? Ni Mahakama au ni Wizara yako? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wajanja wameenda Mahakamani tangu mwaka 2002, wakaweka *Court Injunction. Court Injunction* imekaa Mahakamani miaka 12, hakuna mtu anayejua *injunction* ile inaondolewa lini. Namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, juzi kaniandikia barua, kasema ipeleke Mahakamani ili wafute hiyo *Injunction.* Sasa mimi nashangaa, nyie wenye Wizara, mko wapi? Inakuwaje? Ile ardhi ya Himo, haipimwi, Mji haukui, Mji haupimwi. Ninao vijana karibu 337, wengine wako Canada, Uingereza, wanasema Mrema, tunataka tupime viwanja tujenge, tuna hela, tukope hela Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Ole-Medeye, Waziri, tumeendanaye pale, wananchi wamekubali kwamba, ardhi ile ipimwe. Tumeendanaye Wizarani kwake, Katibu Mkuu ameandika barua eneo lile lipimwe kwa sababu ni kama tumesimama. Hatuwezi kuwa na maendeleo pale, wakati tunasema tuna soko la Kimataifa tunataka watu wa Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi waje kufanya biashara kwetu, sasa kama hakuna viwanja vilivyopimwa, kama Mji haujengwi, utakuwa ni Mji gani jamani? Nyie mmekaa, tangu 2002 mpaka leo? Naweza kusema hakuna Wizara, kama ipo ni hewa; hamna uwezo wa kuweza kuzuia haya mambo, kwa nini? Mbona mimi wakati wangu niliweza kuzuia kwa siku saba (7), nyie mnashindwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitaomba Mheshimiwa Waziri, uniambie ule Mji wa Himo, ni Mji au ni Kijiji? Unajengwa, haujengeki? Tatizo ni nini? Ni kwa nini kesi inakaa Mahakamani tangu mwaka 2002

mpaka leo 2012? Ni kesi gani hizi? Kwa sababu, hizi kesi zinaanzishwa ili kuwafanya mateka nyie Wizara mshindwe kufanya kazi zenu. Hivi hamna uwezo wa kuzungumza na hao Majaji? Sio kwamba, muwafundishe namna ya kuhukumu, lakini muwaambie itakuwaje kesi ya 2002 mpaka leo? Ni nchi gani hii, tunaielekeza kwenda wapi? Watu wanalalamika, Mbunge analalamika, *everybody is crying.* Ni vitu gani hivi mnafanya? Hilo la pili. Naomba maelezo, naomba mipango yenu ya kuendeleza Mji wa Himo na kusaidia hawa watu wanaotaka kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu. Nina Masista walikuja kwako na barua; nasikitika hata hiyo barua haujanijibu, haujawajibu, wale Masista wa *Holy Spirit Sisters* wa Rauya, naomba tusiwakatishe tamaa hawa watu wa Mungu. Hawa watu, wana shamba walilolinunua lenye Hati, Hati ni ya kwako. Sasa tatizo ni kwamba, tunafanyaje? Juzi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amenisaidia sana, ameandika barua, turudi Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikwambie kilichotokea; wamekwenda kuwahamasisha wale Masista kwamba, ninyi mkitaka amani muwaachie hao wavamizi eneo hilo na hao wavamizi walipandikizwa huko nyuma, sio wenyeji wa pale wala sio Wakristu wa lile Kanisa, ni watu walioletwa kwa makusudi kusumbua Kanisa, kusumbua hao Masista. Kuna Wenyeviti wa Vijiji wanauza lile shamba na wapo na watu waliouziwa. Hata hao kuwakamata hamtaki, mnawahangaisha, sasa mnasema utawala bora, utawala wa sheria, ni upi huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Masista waende wapi? Wamekuja mpaka hapa, hakuna mtu anayewasaidia. Wamekuona wewe Waziri, Waziri wa Mambo ya Ndani, sasa mimi nikamuona na Mwanasheria; hii nchi ni kilio kitupu kila mahali, mbona hamna Mamlaka? Mbona hamna mwngozo wa kuweza kuisaidia nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, pale Himo tena kuna shamba la mkonge mlinunua, heka 1,650, mkagawa kwa wananchi waliokuwa kwenye maporomoko, *well and fine,* hiyo hatuna mgogoro, mlifanya vizuri. Mkabakiza eneo kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Kijiji cha Himo. Mkasema Sekondari ya Ashira, *Marangu TTC,* Marangu Mangaka, wakapewa eneo walitunze, walilinde kwa ajili ya maendeleo ya vitu vingine. Mwisho wake, sijui ni nani, mimi sijui ni nani ana madaraka katika nchi hii, maana kila mtu ana sharubu, baba ana sharubu, mama ana sharubu, mtoto naye ana sharubu; wamekwenda kuwanyang'anya wale hilo eneo wakalipunguza, Ashira kidogo, *Marangu TTC* kidogo, *Mangaka TTC,* eti wakaweka wawekezaji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Fula, Meresini, tunataka kupanua pale. Tuna Hospitali ya Wilaya, ina heka tano (5) tu, inahitaji heka 10 na heka 10 zilikuwa pale. Tunataka Benki, yaani kuna mambo mengi yanayohitajika pale katika Mji wa Himo kwa ajili ya maendeleo. Wamekwenda kumpa Mbunge wa zamani, nasikitika kumsema hapa, heka 11; ndio

sababu hii nchi imekuwa ya madalali, tangu Viongozi wa Serikali mpaka hata na sisi wanasiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eti amepewa ni mwekezaji, anaweka Kituo cha Redio, yaani karibu na Shule ya Meresini. Kwa hiyo, ukitaka kupanua ile shule, kuna mtu mmoja amesema kwamba, anataka kunijengea *Form VI* pale, atajenga wapi, wakati kuna Kituo cha Redio? Kituo cha Redio, nani anahitaji hicho Kituo cha Redio? Kituo cha Redio heka 11? Haiwezekani! Wala watu wa Himo, watu wa Vunjo, hawahitaji hicho Kituo cha Redio, cha kazi gani? Tunataka lile eneo litumike kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, matajiri walioko pale, kuna shule ya binafsi ya *Scholastica,* tajiri mkubwa sana, ambaye amenunua Himo yote, leo mnaenda tena katika eneo lile, mnamgawia. Mimi nashindwa kuelewa. Sasa sisi tukataka kufanya maandamano siku ile, hawa watu wenye pesa, wakazuia yale maandamano yangu; karibu na mimi nipigwe. Mbunge halali, anazuiwa asifanye maandamano ya amani ya kutetea watu wake, tena mara mbili! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hapo tumefika? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, sikuonei wivu kazi yako, ni ngumu sana, lakini uwezo wa kuifanya kazi hiyo unao. Siwezi kuunga mkono hoja hii *at this stage,* mpaka uniambie haya mambo yangu, yataishia wapi, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Dokta Mrema, muda wetu umekwisha.

Kabla sijasitisha shughuli hizi, niliulizwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, kuhusu kesho Maswali kwa Waziri Mkuu, jibu ni kwamba hayatakuwepo kwa sababu Waziri Mkuu, kama tulivyoambiwa atarejea tarehe 15 na kwa mujibu wa Kanuni ya 38(5), anapokuwa hayupo basi hatuwezi kuendelea na kipindi kile.

Pia napenda kumtaarifu Mheshimiwa Yahya Kassim, Meza imepokea. Tutajitahidi sana kuona wote wanaokaa mabenchi ya nyuma ili kuwatendea haki. Ni bahati mbaya, sio kwa makusudi. *(Makofi)*

Kabla sijasitisha, naomba niwataje ambao tutaendelea nao saa 11.00. Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Abuu Jumaa na Mheshimiwa Zarina Madabida na Mheshimiwa Dokta Faustine Ndugulile, wajiandae.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.57 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Tunaendelea na majadiliano kama tulivyoanza vizuri. Tutaanza na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, atafuatiwa na Mheshimiwa Abuu

Hamoud Jumaa na Mheshimiwa Zarina Madabida ajiandae.

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache kuhusu hoja ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Awali ya yote, naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walio chini ya Wizara, kwa jitihada kubwa wanayoifanya katika kuendeleza na kusimamia vizuri Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali ambazo zinahusu Wizara hii. Ninaomba jitahada hizo waziendeleze kwa nguvu zao zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya jukumu la Wizara hii kama Waziri alivyoeleza katika ukurasa wa 34 wa Hotuba yake ni pamoja na kusimamia mipaka ya nchi yetu na majirani zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kisichopungua miaka kumi, ndani ya Bunge hili tumekuwa tukizungumza sana juu ya kero ya mpaka wa kati ya nchi yetu na nchi ya Malawi kupitia Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa kidogo nilipokuwa napitia taarifa ya Waziri juu ya utekelezaji ambayo amejitahidi kushughulikia masuala ya mpaka wetu hasa katika Bahari ya Hindi; lakini sikuona mahali popote ambapo amezungumzia suala la mpaka wa Tanzania na Malawi kupitia Ziwa Nyasa. Nimeshangaa kwa sababu kila mwaka hapa Bungeni walau kwa sentensi moja, mbili au tatu au *paragraph* moja, huwa

tunaelezwa ni hatua gani ambazo zinaendelea za mazungumzo ya uhusiano na kutafuta suluhu ya mpaka wa kati ya nchi ya Malawi na Tanzania, lakini hapa limeachwa kabisa! Waziri anatuambia pia kwamba, wao wana jukumu hili la kusimamia na kuweka mipaka. Nchi jirani ya Malawi sote tunafahamu kwamba, wamekuwa wakidai kwamba mpaka wa Ziwa uko kandokando ya Ziwa katika nchi ya Tanzania. Jambo hili linatia wasiwasi mkubwa kwa sababu sioni sababu kwa nini Wizara isiende kuwaelimisha wenzetu. *(Makofi)*

Kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukishuhudia mambo mbalimbali yakiendelea kutokana na hoja hiyo na sisi tumekaa kimya, wananchi wa kule kila wakati wanapiga simu na hawa ni wananchi wanaoishi kandokando ya Ziwa nikianzia Mkoani kwangu Mbeya, Wilaya ya Kyela, watu wanaishi kwa hofu, Wananchi wa Wilaya ya Ludewa wanaishi kwa hofu, Mbinga wanaishi kwa hofu na Wilaya Mpya ya Nyasa wanaishi kwa hofu. Je, tunataka kuridhika na jambo hilo na litaendelea kuzungumzwa au kutolewa maneno ya ahadi mpaka lini? Tatizo ni kitu gani? Hakuna asiyefahamu kwamba, nchi yoyote ambayo inapakana na nchi nyingine katika Ziwa, lazima mpaka upite katikati. Leo hakuna linalozungumzwa, wenzetu tunawaacha wanazungumza hilo la kwamba mpaka ni kandokando ya Ziwa upande wa Tanzania na sisi tunasikikiliza tumekaa kimya, hiyo ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku wananchi wanaona meli zinakuja mpaka nchini kwetu, kweli ni haki hiyo, wanaona ndege zikiruka kandokando ya

Ziwa upande wa Tanzania. Wanaona watu wanaleta meli ndogo ndogo na kufanya utalii utalii huku kwetu. Wanafanya utalii kuona milima yetu bila gharama. Naomba jambo hili liishe na ninaomba wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatoa majumuisho yake, Watanzania hasa wale wanaoishi kandokando ya Ziwa Nyasa, wasikie ni juhudi gani zinazoendelea hivi sasa za Wizara hii kuona kwamba suala mpaka linakwisha. *(Makofi)*

Kama ambavyo wanafanya wananchi katika maeneo ya bahari kwa kuanzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi hasa uvuvi, basi na Wananchi wa Ziwa Nyasa nao wawe na haki ya kufanya shughuli za kiuchumi, ambazo ni uvuvi, kwa amani na utulivu, bila wasiwasi wowote, hatuwatendei haki hata kidogo. Ninaomba sana jambo hili sasa lifikie mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ninalotaka kulizungumzia ni Shirika la Nyumba la Taifa. Juzi, Jumamosi ya wiki iliyopita kulikuwa na semina hapa ya Wabunge, baadhi yetu tulihudhuria tukaelezwa na wenzetu wa *National Housing* mipango yao mizuri sana ambayo wanataka nchi hii iweze kuona mabadiliko hasa katika upande wa wananchi kuishi katika nyumba ambazo ni za kisasa. *(Makofi)*

Mimi niliupongeza sana mpango ule na nilichangia lakini kwa *record* ya *Hansard* naomba niliweke nilizungumze leo tena. Lazima tuwapongeze vijana hawa wa *National Housing* kwa sababu wameleta mambo mapya, wana mtazamo wa mbali na ni yale ambayo tunaposafiri kwenye nchi za

wenzetu tunaona. Tunaona jinsi ambavyo wananchi wa nchi nyingine wanaishi katika makazi mazuri. Azma ya hili kama *concept* nzima ya *National Housing*, ni kujenga nyumba zenye bei nafuu. *(Makofi)*

Ili wananchi wengi waweze ku-*afford* kuzinunua na waishi humo na katika hali ya sasa kwa sababu bado tunang'ang'ania kuweka *VAT* katika nyumba za kuuza au kutoza ushuru katika vifaa vya kujengea hizi nyumba za hawa tunaosema wakae kwenye nyumba za bei nafuu tumeng'ang'ani hapo. Naomba Wizara isaidie hilo, izungumze na Hazina mara moja wafute ushuru ili wote tununue nyumba. *(Makofi)*

Hata nyumba ya bei nafuu anayosema Mkurugenzi Mkuu, ambayo inajengwa na kuuzwa kwa hivi sasa, mimi hapa ni Mbunge siwezi kuinunua gharama yake ni kubwa; je, mtu wa kawaida? Ninaomba sana Wizara ijitahidi kuzungumza na Hazina na ninamwona Waziri wa Fedha hapa Bungeni, alisikie hili jambo alichukulie hatua haraka iwezekanavyo watu tupate nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ardhi. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. ABUU H. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nachukua fursa hii kumshukuru ama kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada kubwa anazozifanya kuhakikisha kwamba, nchi yetu

inapiga hatua katika suala zima la maendeleo. *(Makofi)*

Vilevile ninawashukuru Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini, kwa imani yao kubwa wanayoonesha kwa Serikali yao na Mbunge wao; nawaambia tuko pamoja sitawaangusha. Nawapongeza pia Madiwani wangu, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika Jimbo langu, pamoja na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi ya Mwaka 2012/2013, inayolenga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inayosisitiza uchumi endelevu katika matumizi bora ya ardhi. Kuendelea na mpango huu wa kurasimisha ardhi kwa wananchi, itawapa heshima Wananchi wa Tanzania katika kumiliki ardhi yao na kuwa na makazi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango mizuri ya Wizara hii, lakini bado kuna matatizo mengi yakiwemo umilikishwaji wa ardhi na urasimu wa zoezi zima la utoaji wa hati miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mheshimiwa Rais anasisitiza Mpango wa Kilimo Kwanza, lakini kwa bahati mbaya mpaka leo hii Hati Miliki za Vijiji hazijapatikana. Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini wanahitaji wapate Hati Miliki ili waweze kuchukua mikopo kwa ajili ya kununua matrekta na kupata

pembejeo waondokane na kilimo cha jembe la mikono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili limekuwa kubwa, tunaomba Serikali kupitia Wizara hii, iharakishe suala hili ili wananchi waweze kupata hati hizo. Lipo tatizo lingine kubwa la mashamba pori katika Jimbo langu, kuna maeneo mengi tu baadhi ya wawekezaji wanachukua mashamba ama maeneo makubwa na badala yake wanachukulia mikopo lakini wanashindwa kuyaendeleza. Wananchi wanahitaji wapate maeneo hayo kwa ajili ya kulima, lakini pia na sisi katika Jimbo letu la Kibaha tumekuja na mpango wa upimaji wa viwanja. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ichukue hatua za haraka ili tuweze kupata maeneo yale. Kuna migogoro mingi ya ardhi katika maeneo yetu; kwa mfano, kuna Kata moja ya Soga, pale kuna shamba moja liko Alave, naambiwa la tajiri mmoja limekuwa na mizozo mikubwa na wananchi. Ninaamini Wizara inafahamu kwa sababu Mkuu wa Mkoa aliainisha maeneo yote yenye matatizo na amepeleka Wizarani. Ipo migogoro mingine ya wafugaji na wakulima ya kugombea mipaka, tatizo hili limekuwa kubwa; kwa nini Serikali isitenge pesa kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi waelewe suala zima la mipaka?

Kwa sababu yako maeneo ambayo yametengwa na Serikali imetenga maeneo haya lakini kwa bahati mbaya wananchi hawa wanashindwa kupata elimu hii ili waweze kuelewa suala zima la mipaka yao na maeneo ambayo wanaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango hii ya Wizara, lakini kuna ujenzi ambao unaendelea. Dar es Salaam pale kuna wafanyabiashara ambao wamejitokeza sasa hivi wanauza magari katika nyumba za makazi; kwa nini Wizara isitenge eneo katika Mji wa Kibaha Vijijini tukajenga maegesho makubwa kwa ajili ya kuuza magari hayo? *(Makofi)*

Ukienda Dubai, Shadiya pale kuna eneo kubwa sana wametenga kwa ajili ya kuuza magari na Dar es Salaam sasa hivi kila nyumba ambayo unaingia kumekuwa na mchezo wa kuuza magari. Tatizo likitokea, kwa mfano, inawezekana gari moja likapata athari ya kuungua, madhara yake yanaweza yakawa makubwa sana. Bado naendelea kuishauri Serikali ijipange waje kujenga *yard* kubwa au kutenga eneo kwa ajili ya wauzaji wa magari, wote wahame Dar es Salaam waje katika Mji wa Kibaha Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini wapo tayari kabisa Serikali ijenge nyumba za mfano katika Mji Mdogo wa Mlandizi, ioneshe mipaka, ionesha njia, iweke barabara, umeme na maji ili iwe mfano katika maeneo mengine. Kumekuwa na ujenzi holela; kwa mfano, nasikitika kutoa mfano katika Jiji la Dar es Salaam, kuna maeneo mengi yamejengwa kiholela sana mfano ukiangalia Manzese, Tandale na maeneo mengine. Sasa ni lazima tuondokane na tatizo hili na mimi kwa bahati mbaya huwa nasikitika sana nikiona Halmashauri inatoa vibali vya kujenga maghorofa pale Manzese; ni jambo la kusikitisha kweli. Hivi tutaendelea na mpango wa kujenga nyumba za kawaida tu pale, kwa sababu

naamini ipo siku tutakuja kubadilisha matumizi katika maeneo yale tutaingia gharama kubwa kulipa fidia. Sasa ni vizuri tungeanza kuzuia kutoa vibali katika maeneo ambayo hayajapimwa ili kupunguza gharama kwa Serikali baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* kwa juhudi kubwa wanazozifanya za kujenga nyumba na kuwauzia wananchi. Pamoja na juhudi hizi, lakini ni kweli kuna matatizo mengi ya nyumba, nyumba zinazojengwa ni chache, wananchi wengi wanazihitaji. Vilevile kodi zimekuwa kubwa sana za nyumba hizi. Sasa hivi naambiwa juzi tu hapa ukilinganisha mwaka 2001 mpaka 2012, zaidi ya mara kumi kodi zimepanda na zinapanda zaidi ya asilimia 50; tatizo hili limekuwa kubwa sana. Kuna mtu mmoja ameniambia walikuwa wanalipa shilingi laki tatu, lakini sasa hivi wanalipa shilingi laki sita, naishauri Serikali iwe makini katika suala hili; kuna wananchi wetu kule na kwa bahati mbaya nyumba ambazo wanalipia shilingi laki sita unakuta wananchi wanazihudumia wenyewe nyumba, wanapiga rangi wenyewe, *National Housing* wakija kupiga rangi nje lakini ndani vyoo vibovu, mabomba ya maji, umeme na kadhalika, vyote wanahudumia wananchi wenyewe. Naomba Serikali iliangalie suala hili, tuna wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru

Mwenyezi Mungu, kwa kutuweka hapa salama leo. Vilevile naomba nichukue fursa hii kuwatakia Waislamu wote na Watanzania wote kwa ujumla, mfungo mwema, nasema *Ramadhani Kareem. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa Bajeti nzuri. Naomba vile vile niipongeze Kamati na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mwana-Dar es Salaam mwenzangu, kwa sababu kuna maneno ambayo ameyasema mimi nakubaliana na yeye hasa katika masuala ya msingi ikiwemo kuchukua sheria mkononi na watu ambao wanakwenda kuvunja kwa mabavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii, kumpongeza Waziri wa Ardhi, Waziri wa Elimu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kulimaliza suala la Mlogazila. Mimi nasema ahsante sana na nina imani hata nitakayoyasema leo kupitia kwako, Mheshimiwa Waziri atayachukua na atayafanyia kazi kama alivyolifanyia kazi suala la Mlogazila. Hiyo mimi naita ni India ya Watanzania, tunaisubiri kwa hamu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina masuala madogo mawili ambayo ningependa kuchangia. Mojawapo, nimesikiliza hotuba nzuri sana ya Mheshimiwa Waziri na nilikuwa nafurahi alipokuwa anazungumza, lakini ninajiuliza hivi nimesikia sawasawa au kidogo sijasikia vizuri? Ninamwomba Waziri anifafanulie atakaposimama kusema, hawa Wananchi

wa Kigamboni yaani Mji Mpya unaojengwa wanaingia ubia au ni kwamba wao wanatafutiwa mahali pengine waende ili kupisha ujenzi? Mimi nitakubaliana naye moja kwa moja kama wanawapeleka mahali pengine ni *temporary* wakakae lakini wakimaliza hapo warudi na siyo kwamba wampe *flat* moja akae, hapana, waangalie yule mwekezaji atapata nini na huyu mwananchi anapata asilimia ngapi ya uwekezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni mali ambayo siku zote inaongezeka thamani, kwa hiyo, natarajia mwananchi huyu kuchukua ardhi yake kusimtumbukize katika dimbwi la umaskini bali limuweke na yeye mahali ambapo anaweza kufurahia maisha kama mwananchi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa nikakisoma Kitabu cha Hotuba, katika ukurasa wa 50 na 51 pale kidogo nimepata wasiwasi, ninaomba ufafanuzi. Kwenye ukurasa wa 50, Mheshimiwa Waziri ameorodhesha vitu ambavyo wanatarajia kuvifanya mwaka huu na pale wameandika na zile Kata ambazo ndizo zinachukuliwa lakini *page* ya 51 ndiyo iliyonitia mashaka zaidi. Inasema kwamba, watatumia shilingi bilioni 60 kwa ajili ya shughuli za mwaka huu. Hizi shilingi bilioni 60 ni asilimia kumi ya mahitaji ya mwaka mzima. Sasa najiuliza kama hizi ni asilimia kumi; je, hizo asilimia tisini wanazitoa wapi kwa mwaka huu? Hilo ninaomba nipate jawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mradi umeanza toka mwaka 2008, wananchi walikatazwa kujenga, yaani ni miaka minne, hata kama mtu alikuwa na kijiakiba

chake cha uzeeni anataka kujenga pale, ameshakila kimekwisha. Sasa mimi nauliza; watapataje fidia ya hii miaka ambayo wamepoteza; yaani hii miaka minne? Itaingizwa katika huu Mradi ili na huyu mwananchi apate?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa bado nina tatizo lingine, naomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie. Hii habari ya kutengeneza *Kigamboni Development Authority,* hii inakuja kuwa wanafanya kazi pamoja au zinazofanana na Manispaa ya Temeke na sisi tuliokuwa zamani tunajua kulivyokuwa na mgongano kati ya *CDA* na Manispaa ya Dodoma. Sasa hili sijui wanalitatua vipi?

Kitu kingine ambacho kilikuwa kinanipa matatizo hapa katika Kitabu cha Mheshimiwa Waziri imetajwa Kata ya Mjimwema, Kigamboni, Vijibweni, Kibada na Somangila. Katika Kata hizo hizo kuna Mradi mkubwa wa *NSSF;* upo humo? Kuna Mradi mkubwa wa Shirika la Nyumba haupo humo? Vilevile Manispaa ya Kinondoni inapima na kugawa viwanja humo humo. Mimi naona kama kuna vuruguvurugu! Sasa sijui Mheshimiwa Waziri atanifafanulia akija kujibu kwamba hii itakuwaje wakati tutakapouleta, maana hapa sasa hivi bado ninaona giza, sijaona mwanga mbele yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu Shirika la Nyumba. Kusema kweli mimi naungana na Mheshimiwa Waziri na wenzangu kuwapongeza sana Mkurugenzi Mkuu na Watendaji wote; ni vijana *energetic,* wanaonekana ni wazalendo, wanajua wanachokifanya. Ninasema wazalendo kwa

sababu sisi Wabunge wa Dar es Salaam walitutembeza katika Miradi yao na walitupitisha kuangalia sehemu zote ambazo wanajenga, vilevile walitupa maelezo na wakatuambia jinsi walivyookoa nyumba nyingine ambazo wajanja tayari walishazifanya zao kwa kuzipata bure. Kwa hiyo, nawaomba waendelee, tuwatie moyo na kusema kweli Serikali iwasaidie waweze ku-*perform*.

Pamoja na hilo na mimi naungana na wenzangu, wamesema hivi, hizi nyumba ambazo wanajenga ni za *middle income;* lakini tukimchukua huyu *middle income* ni nani? Huyu kijana ambaye ametoka Chuo Kikuu leo, Injinia au Daktari, Mwalimu au Mfamasia na wengine wote ndiyo hii *middle income;* mshahara wao sisi sote tunaujua ni kati ya shilingi 450,000 mpaka 500,000. Akilipia nyumba shilingi 250,000 atakula nini? Sasa hii *middle income* ni akina nani; ni wafanyabiashara? Kwa hiyo, naomba tafadhali sana hawa watu wa *National Housing* waliangalie hilo. Mimi sina tatizo la wao kujenga nyumba ambazo watafanyia biashara, lakini ni lazima wasiondoke katika *objective* yao ya kwanza ya ku-*provide* nyumba kwa watu wa *low income* kwa bei nafuu. Hilo naomba liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashauri; mimi nawaambia kwa sababu wengine watundu watundu ni wafanyabiashara kidogo, hebu waende Ethiopia wakaangalie, kuna viwanda kule wenzetu ile *technology* wameitoa China sasa hivi wana viwanda vitatu wanatengeneza *building material* ambayo haitumii chuma wala *cement;* kwa hiyo, wanapunguza

cost ya kujenga kwa zaidi ya asilimia 30. Nami nafikiri tukifikia hapo, tutateremsha bei sana halafu cha ziada ni kwamba hizi *raw materials* ambazo wanazitumia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ya pili hiyo? Naunga mkono hoja na ninaomba niwape ushauri hawa *National Housing (NHC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Ahsante sana na sasa namwita Mheshimiwa Faustine Ndugulile.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kabla kengele haijanililia na mimi niseme kwamba, siungi mkono hoja.

Mnamo tarehe 15 Agosti, 2011 wakati nachangia Hotuba ya Wizarara hii, nilitoa sababu sita kwa nini sikuunga mkono Hotuba ya Bajeti ya mwaka jana. Kuna maeneo sita ambayo niliyaainisha.

Moja, nilisema kwamba, kule Pemba Mnazi kuna mwekezaji ambaye ana ekari zaidi ya 5,000 ambazo umiliki wake una utata, wananchi wanakosa eneo la kulima na kuishi. Nikawaomba Wizara wanipatie maelezo kuhusu mkataba ambao walikuwa

wameingia naye lakini mpaka sasa hivi hawajatoa majibu.

Pili, niliongelea suala la viwanja 20 Kibada, Serikali imeuza viwanja pasipo kuchonga barabara na watu wengine mpaka sasa hivi pamoja na kukaa na Watendaji na Waziri mwenyewe na kumwandika barua, lakini mpaka sasa hivi sijapata majibu.

Dungu Farm kuna watu zaidi ya 105 pamoja na mama yangu mzazi, walikuwa na eneo pale wakawa wameendeleza lakini mpaka sasa hawajapata fidia na sijapata majibu ya msingi kutoka Serikalini.

Sababu ya nne, kuna viwanja 20,000 vya Kisota, Watendaji wa Wizara ya Ardhi walipima maeneo makubwa lakini viwanja vilivyotolewa ni vichache sana. Watendaji wa Wizara ya Ardhi wana zaidi ya viwanja 100 pale. Nilimwomba Waziri afanye *audit* ya viwanja vile, sasa sijui na yeye wamemuwezesha sasa hivi amekaa kimya na hilo hajalifanya mpaka leo.

Kuna suala la tano ambalo lilikuwa la uendelezaji wa bandari Vijibweni. Mradi huu umekaa umepinda kweli kweli, mara wanataka ekari 7,000, mara wanata ekari 700, mara ekari 400 na yote haya nilimwomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu na haya mambo mengine hayahitaji fedha. Kwa hiyo, nikifanya tathmini, *I had a very high expectation* ya Waziri huyu lakini *performance is being very dismal,* nampa sifuri katika utendaji katika suala hili. Mengine haya hayahitaji fedha ni udhaifu na utendaji mbovu ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujikita katika suala kubwa la msingi, yaani suala la Mji Mpya wa Kigamboni. Kuna maswali ya msingi ambayo mimi nataka tujiulize; hivi kwa nini Serikali inataka kuingia gharama kubwa kuingia katika maeneo ambayo tayari yameshaendelezwa na watu wanaishi? Hivi Tanzania tumeshapungukiwa maeneo kiasi hicho? Kwa nini tusiende Mkuranga, Kisarawe, Kibaha au Bagamoyo? Kama mnapenda Kigamboni, Kata ya Somangila, Pembamnazi na Kisarawe kuna maeneo; kwa nini mnataka kwenda kwa wananchi ambao tayari wameshakaa na wameendeleza? Kwa nini Serikali inataka kuingia gharama kubwa kulipa fidia na *compensation* kwa watu ambao tayari wameendeleza makazi yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni Sera ya Serikali kusumbua wananchi wake? Hivi kwa nini wananchi hawana haki kuishi katika maeneo mazuri?

Miaka ya 70 Serikali hii mliwaambia wananchi watoke kule wapelekwe katika Vijiji kama Gezaulole na Kibugumo, sasa hayo maeneo yamependeza na mkawaimbia na wimbo kabisa kwamba, nendeni Gezaulole, Kibugumo na Mwanagirati kwenye makao mapya, sasa hayo maeneo yamependeza Serikali inataka kuyachukua na kuwanyang'anya wananchi! Hivi mwananchi wa kawaida hana haki ya kuishi katika maeneo mazuri?

Suala lingine ambalo nahitaji kuuliza ni kwamba; miji mara nyingi inaendelezwa na Sekta Binafsi lakini

katika huu Mradi wa Kigamboni Serikali imeamua kung'ang'ania udalali, ichukue ardhi ya wananchi iuze kwa bei kubwa. Sasa hii inatupa mashaka sana, lakini nasema katika lugha zetu za mtaani, kama Serikali ilichukua fedha za mwekezaji rudisheni mwambieni kule Kigamboni kimenuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na Sheria ya Ardhi inatamka kwamba, ardhi ni mali ya mwananchi, anapaswa kunufaika na ardhi yake. Naomba Waziri anieleweshe hivi ni Sera ya Serikali kudhulumu ardhi ya maskini na kuwapa matajiri; nini dhana ya maisha bora kwa kila Mtanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu mzima una upungufu mkubwa sana wa kisheria. Mpango huu ulitangazwa kwa kupitia tangazo katika Gazeti la Serikali Na. 229 la tarehe 24 Oktoba, 2008 kupitia kifungu Na. 34 cha Sheria ya Utoaji Ardhi Na. 47 ya Mwaka 1967 na baada ya hapo yakatoka matangazo kwenye magazeti tarehe 26 Oktoba na mchakato mzima ulikuwa unatawaliwa na Sheria Na. 8 ya Mwaka 2007. Sheria ni nzuri tu na wala haina matatizo, lakini wakubwa walijisahau walipokuwa na haraka haraka na papara zao. Sheria hii kwa mujibu wa kifungu cha 83(a), kinataka kabla hamjaanza mchakato wa Mradi ni lazima mfanye mkutano wa hadhara katika eneo husika na wananchi watoe ridhaa. Mkutano huo haujawahi kufanyika. Mheshimiwa Waziri atuambie hapa ni lini Mkutano huo ulifanyika na Wananchi gani wa Kigamboni walioshiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuonesha kwamba mchakato huo hawa wakubwa waliuanza mapema, mchoro wa Mpango Miji walishauandaa tangu tarehe 9 Juni, mwaka huo huo na kuupa namba 1/38508. Wameanza mchakato kabla hata ya kuja kuutangaza na uhamasishaji kwa wananchi wamekuja kuuanza Desemba. Hiyo inaonesha kwamba, kifungu cha kwanza kimeshakuwa ni batili sheria imekiukwa.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mnachoambiwa hapa siyo kweli. Wanasema kwamba, mpango umekamilika sasa hivi imebakia hatua ya utekelezaji; hilo siyo kweli. Kuna vifungu vingi tu ambavyo havijakamilika na hata mkutano wa wananchi na wadau haujafanyika. Katika kitabu chake Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, ana asilimia kumi tu ya fedha ya uwezeshaji na ninyi mtakumbuka katika bajeti ya mwaka jana tuliwapa muda mpaka mwezi Juni, 30, wawe wametekeleza Mradi, mpaka hivi sasa wameshindwa na Mradi huo haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi; Mradi huu kwa mujibu wa Sheria umeshapitwa na wakati. Mradi huu kwa mujibu wa Sheria ni batili kwa sababu vifungu vingi vya Sheria vimekiukwa na Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu nitakupatia vifungu vya Sheria vilivyokiukwa. Kwa hiyo, Mradi huu ni batili na Wananchi wa Kigamboni wamenituma kauli moja tu kwamba, sasa hivi hawautaki tena Mradi wa Kigamboni. Naomba nirudie, Wananchi wa Kigamboni hawautaki tena Mradi huu wa Kigamboni, waliwapa muda wa kutosha, mmeshindwa kuanza hatutaki tena,

hatutatoa ushirikiano. Huu utaratibu ambao Wizara na Waziri ameuanzisha wa kuwahonga Waheshimiwa Madiwani kwa gharama ya Serikali kuwaleta Dodoma, nikwambie kabisa pasipo ushirikiano wa Mbunge hutoweza; wapeleke Malaysia, Hong Kong, Mradi wa Kigamboni hautofanyika. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Sema!

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUNGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee, rudini kwa Wananchi wa Kigamboni, mchakato huu uanze upya na mfuate Sheria kama inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, Wananchi wa Kigamboni naomba niongee, najua leo kama Wananchi laki moja wananisikiliza; naomba mwendelee kujenga, Mradi huu ni batili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, ahsante sana.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, napenda kuwashukuru vijana wenzangu wa Umoja wa Vijana wote hapa nchini, kwa kunipa ushirikiano mkubwa ninapotimiza wajibu wangu, kwa kunipa maoni mbalimbali ambayo wanataka niyawakilishe Bungeni bila kujali itikadi za vyama vyao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na tatizo la Kigamboni na changamoto zake, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri. Hotuba ya

mwaka huu mbali na matatizo ya Kigamboni ambayo na mimi nayaafiki, kuna vitu vya msingi ambavyo vimefanyiwa kazi. Hotuba ya mwaka huu imeonesha utofauti na Hotuba ya mwaka jana, hilo naomba niliseme na mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kutaka kurudisha heshima ya dola kwa watu wanaotumia nguvu ya fedha kuchukua maeneo ya wananchi bila kufuata taratibu. Alianza na hivi ninavyoongea utaratibu huo unaendelea katika Jiji la Dar es Salaam, lakini Mheshimiwa Waziri nakuomba kasi hiyo haitoshi, endelea nayo na ninajua bado kuna mabangaloo mengine mawili yanahitaji kuvunjwa na usikubali. Watu wanaotumia nguvu za fedha kutaka ku-lob Mahakama kupindisha sheria na amri halali ya Wizara iliyotolewa kuhakikisha nyumba zinavunjwa kwa watu ambao hawaheshimu dola, kwa watu ambao wanakiuka taratibu na kutaka kuwanyonya wanyonge wa Taifa hili. Mheshimiwa Waziri, hilo naomba uendelee nalo kwani litarudisha heshima ya Taifa letu na itaonesha kwamba pesa siyo kitu ndani ya Sheria.

Mheshimiwa Waziri, kabla sijaendelea na mambo mengine, naomba niongelee mambo yanayohusu Jimbo langu, maana mimi ni Mbunge wa Vijana.

Katika Bunge lililopita tulipitisha Azimio la Vijana na mambo ya msingi kwenye Azimio lile ambalo nchi wanachama wamekubaliana nalo ikiwemo Tanzania, kuhakikisha mnawawezesha vijana kumiliki ardhi ili

kuwaondolea umaskini. Mheshimiwa Waziri, naomba nikwambie kwamba, hatma ya Vijana wa Taifa hili ipo mikononi mwako, vijana wameshindwa kufaidika katika maeneo mengine sasa hivi tumaini lao kubwa ni ardhi. Naomba utakapokuwa unahitimisha Hotuba ya Wizara yako, unipe *strategic plan* katika utekelezaji wa Azimio la Vijana kuwawezesha vijana kumiliki ardhi yao na kujiondoa katika wimbi la umaskini na tatizo la ajira linalowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia changamoto kubwa ambayo inaikabili Wizara hii na nchi zilizonufaika na ardhi, kuna mambo ya msingi ambayo waliyafuata. Moja ni kuhakikisha ardhi inapimwa, lakini pili kuhakikisha wananchi wanamiliki ardhi yao kwa kupewa hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hekta milioni 88 za ardhi ya nchi hii, ni asilimia kumi tu ambayo imepimwa, asilimia 90 haijapimwa. Tatizo hili linachangia kuleta migogoro ya ardhi hapa nchini. Naamini kabisa ardhi ikipimwa, tutagawa matumizi ya ardhi kutokana na mahitaji husika ya sehemu husika na hivyo hakutakuwa na mwingiliano kati ya wakulima na wafugaji na tutaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya ardhi ambayo inalikabili Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Wizara ya Ardhi kupitia Vitengo vya Upimaji Ardhi, ina timu kila kanda, tatizo kubwa ambalo linaikabili Wizara hii ni fedha. Mwaka huu najua wametenga karibu shilingi bilioni 3.7, hazitoshi na naiomba Serikali mlichukulie suala hili kwa umuhimu wake. Katika kutafuta habari, nilipata

information kwamba, Kitengo hiki cha Upimaji Ardhi kinahitaji bilioni 20 ili kukamilisha upimaji wa ardhi hapa nchini. Rai yangu ni kwamba, mbali na kwamba katika Hotuba ya Waziri mmeonesha mna nia ya kufanya hivyo, naomba katika mwaka ujao wa fedha, mfikirie kutenga fedha nyingi kuhakikisha kwamba ardhi ya nchi yetu inapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbali na hilo, matatizo haya pia yanachangiwa na Halmashauri kutokuwa na watumishi wa kutosha kwenye Vitengo vyao vya Ardhi. Hii inawapa *advantage* wale wafanyakazi wachache kutengeneza *chain* na Wizara kutumia *weakness* iliyopo ya kutopimwa kwa ardhi kuhakikisha wanaendelea kuwadhulumu Watanzania wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kama ardhi itapimwa na Watanzania watapata hati, tutapunguza tatizo kubwa lililopo. Zaidi ya Watanzania milioni 40 waliopo ni asilimia moja tu ndiyo wana hati na tunajua watu wengi na hasa wananchi waliopo vijijini na ukizingatia hizi hati za kimila benki hazizitambui, wanashindwa kwenda kukopa benki kwa sababu hawana hati na hasa vijana wenzangu. Kama mnavyojua, benki hazina urafiki na maskini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hakikisha unatenga fedha za kutosha, ardhi inapimwa, wananchi wanapata hati, vijana wenzangu wanapata hati na wazitumie kupata mikopo kwa ajili ya kujikomboa na umaskini.

Kabla Mheshimiwa Waziri hajahitimisha hotuba yake, nitaomba azungumzie kwa kina utekelezaji wa

Wizara yake katika Azimio la Vijana ambalo tumelipitisha. Pili, nitaomba aelezee kwa kina maana hajaelezea kabisa, Mheshimiwa Januari Makamba, hapa alikuwa amewasilisha hoja binafsi kuhusiana na kupatikana kwa sheria ya wapangaji. Hilo hujaligusia na mimi nalizungumzia kwa sababu wanaoathirika ni vijana wenzangu ambao wanaanza maisha. Wao ndiyo ambao wanakutana na kero kubwa ya kodi kubwa ya pango na kama unavyojua, siku hizi dola ndiyo inatumika kupita kiasi, maana siku hizi mpaka kodi za nyumba ni kwa dola. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri alichukulie hili kwa umuhimu wake. Pia nasisitiza kwamba, kuna haja ya Mheshimiwa Waziri kukaa na Wananchi wa Kigamboni. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini kabisa kama Mheshimiwa Ndugulile hana dhamira ya dhati. Tunajua Sheria ya Mipango Miji inawapa mamlaka ya kuchukua maeneo ambayo wananchi wapo, lakini kuna *limit* tangu mwaka ambao mnataka kutangaza Mradi na kuhakikisha fidia ni miaka miwili kwa mujibu wa Sheria Na. 42, kifungu kidogo cha (2), lakini leo hii ni miaka minne sasa. Sasa wananchi wanapofanya makosa tunaona *action* inachukuliwa haraka, lakini katika hili Serikali kidogo mmeteleza; kuna haja ya kukaa upya na Wananchi wa Kigamboni kuona ni jinsi gani mta-*solve* tatizo hili. *(Makofi)*

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lugola, kwanza, umekiuka Kanuni; ulitakiwa usimame kimya halafu ndiyo useme mambo ya mwongozo. Kwa hiyo, kaa chini. Namwita Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa Anna Kilango Malecela atafuatia.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Wizara hii muhimu ya Ardhi. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema leo nisimame katika Bunge hili Tukufu, nizungumze masuala muhimu ambayo yanawasibu Watanzania wanyonge ambao ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu, ajibu hoja za Upinzani kwanza, kwa sababu sasa kumekuwa na tabia ya Mawaziri kuacha hoja za Upinzani, wanajibu hoja za Wabunge. Tumeshaliona hilo kwa Wizara mbili, tatu, zilizopita. Niseme kwamba, tunahitaji majibu ya kina katika haya ambayo yamesemwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na bahati nzuri ameongelea masuala ya msingi na muhimu sana. Kwa hiyo, tunahitaji majibu kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala zima la Bajeti ya Wizara hii. Inasikitisha sana, Wizara ambayo imehodhi kila kitu, majengo tunaweka juu ya adhi, utawala, sheria, maji na chochote, kila kitu kipo juu ya ardhi, inatengewa fedha za maendeleo kidogo lakini wanapelekewa chache zaidi ya kile ambacho Bunge hili limepitisha; ni aibu! Mwaka juzi walitengewa shilingi bilioni 22 zikapelekwa shilingi bilioni nne. Mwaka huu

unaoisha wa 2011/2012, Wizara ilitengewa shilingi bilioni 20 fedha za maendeleo lakini zikapelekwa shilingi bilioni tatu, yaani kama kilomita tatu tu za lami. Wizara hii ni kubwa, ina-*cut accross* nchi nzima, migogoro mingi, lakini hata zile shilingi bilioni 22 zinazotengwa zinapelekwa shilingi bilioni tatu. Hii ni aibu kwa Serikali! Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nafikiri sasa wakati mnawekeana *ceiling* kwenye Baraza la Mawaziri, inabidi mwongeze nguvu; vinginevyo, mtaendelea kutengewa fedha kidogo halafu hampelekewi na hivyo migogoro inaongezeka. Nimeishauri Wizara na Mheshimiwa Waziri, waangalie hizi fedha kwani hazitoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye yale ambayo Wananchi wa Mkoa wa Manyara wananituma kila siku na yale ambayo Wananchi wa Babati wananituma niyasemee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mashamba. Namshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ameorodhesha mashamba kwa Wilaya na Mikoa. Wilaya ya Babati ina mashamba 11 ambayo yalishauriwa na Serikali hii hii mwaka 1997, chini ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, kipindi hicho Mheshimiwa Ole Njoolay kwamba, mashamba hayo yarudishwe kwa Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha, mpaka leo mashamba hayo 11 likiwepo la Rivaku, *Brewaries, Sisal Estate, Latina Estates,* mashamba yote haya ambayo yanapatikana pale Babati Mjini hayajulikani.

Mpaka leo migogoro haiishi, wananchi wamekuwa wanahama hama wanakimbizwa, wamekuwa watumwa katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani na Waziri, Naibu Waziri, ninawaomba Wizara ya Ardhi haipo Dar es Salaam tu, waje Babati haya mashamba yahaulishwe, yafufuliwe yarudi kwa wananchi kwa sababu yamekaa tu. Vigogo ndiyo wanamiliki haya mashamba wakati wananchi wakiteseka. Hii nchi hatuwezi tukaongoza kwa kiasi hiki cha miaka 50 ya Uhuru, Watanzania ni Manamba katika nchi yao, watu wachache wanahodhi ardhi lakini wanyonge hawana maeneo hata ya kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la mashamba namhitaji Mheshimiwa Waziri anijibu wakati anahitimisha. Sasa niende haraka haraka kwenye migogoro ya ardhi. Naishukuru Wizara kupitia Waziri na Naibu Waziri, walimtuma *Chief Valuer* akaja Babati mwezi wa pili, akasikiliza migogoro ya ardhi ya Babati Mjini, Bagara Ziwani, lakini cha kusikitisha aliishia Jimbo la Babati Mjini tu, hakuenda tena Babati Vijijini. Pamoja na hayo, Wananchi wa Babati wanamwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ile ripoti imeishia wapi? Mpaka leo hawajalipwa fidia tangu mwaka 2004, mashamba yao yamechukuliwa, Mipango Mji wamepanga mji lakini wale wananchi mpaka leo Halmashauri haijawalipa fidia. Bahati nzuri *Chief Valuer* ameeleza vizuri na Ripoti ipo kwako. Tunahitaji kufahamu mlichoandika kwenye hiyo Ripoti kwa sababu wananchi wameshindwa kuendeleza mashamba yao, wanashindwa kujenga na

hawajalipwa fidia tangu mwaka 2004. Hii Serikali ni sikivu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kuhusiana na hiyo Ripoti; ni hatua gani zimechukuliwa? Ninasikitika kwamba, Halmashauri inadaiwa fedha nyingi sana na sidhani kama wataweza kulipa. Kwa hiyo, tunahitaji majibu ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la fidia, iletwe *amendment* ya Sheria ya Ardhi kuhusu suala la fidia kwa sababu Sheria ya sasa inataka kwamba, kama eneo lako limechukuliwa haujalipwa fidia basi unalipwa riba ya asilimia sita ya *fixed deposit* katika *Commercial Banks*. Hiyo asilimia sita tumeshuhudia imeongezeka Babati kwa miaka hiyo tangu mwaka 2004 ni kiasi cha shilingi 40,000, mwananchi *by then* ardhi yake imechukuliwa kwa shilingi 300,000, lakini kwa miaka hiyo yote Serikali imechelewesha fidia, ile asilimia sita imeongezeka kwa shilingi 40,000; *is shame*. *Value* ya ardhi imepanda, hiyo ardhi inauzwa shilingi milioni 10 mpaka 20, Mtanzania wa Babati unamlipa shilingi 340,000, hawawezi kuelewa, hawawezi kusikia kwamba Serikali hii ni sikivu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ije na *amendment* ya hiyo Sheria mapema sana katika hili Bunge Tukufu, tuone jinsi gani Watanzania wanatendewa haki. Kitu cha kusikitisha ni kwamba, kama huna nyumba kwenye shamba lako, haijalishi ni ekari ngapi, hawakupi kiwanja, wanakupa fedha. Fedha zenyewe una shamba la ekari 19 lakini haizidi shilingi milioni mbili. Shamba hilo linakuja kutoa viwanja

vingi wanauza kwa mamilioni ya fedha na yule Mtanzania mwenye *ownership* ya ile radhi tangu enzi za nchi hii inazaliwa, anaondolewa tu. Kibaya zaidi ni pale ambapo una familia ya watoto kumi na una nyumba moja lakini kinacholipwa ni kiwanja kimoja tu cha ile nyumba iliyokutwa pale. Haya ni mambo gani? Tunahitaji marekebisho ya hiyo Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kuhusiana na suala zima la Wananchi wa Babati Vijijini, Gijedabu, Ayamango na Gedamari; ni muda mrefu sana tumezungumza juu ya hawa wananchi ambao kwa miaka minne wanaishi kwa kupelekewa chakula cha njaa kutoka Serikalini. Wamekatazwa kulima kabisa kwa sababu wana mgogoro na Hifadhi ya Tarangire. Hawaruhusiwi kujenga choo, kufagia uwanja, kujenga nyumba, nyumba zao zimedondoka na wanapambana na askari kila siku. Wameambiwa watapewa Shamba Galapo, Kashi, lakini hilo Shamba la Kashi ambalo lipo katika Kata ya Kashi, wamechukua Vigogo wa Serikali. Wameenda kuangalia mahali pa kupeleka wale wananchi wawahamishe ili Hifadhi iendelee, lakini hatima yake wakachukua yale maeneo na wale wananchi wanahangaika, wanaambiwa watapelekwa Hanadeko, Galapo Estates, watapelekwa Kashi, wale wananchi mpaka leo wanalia. Hivi hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kama siyo ufisadi kwenye ardhi ni nini? Tangu mwaka 2008 sasa hivi ni 2012, Wananchi wanapelekwa huku kaya zaidi ya 200, vijiji vitatu! Wizara mbili za Maliasili na Ardhi kwa nini msikae mkazungumza kuhusu mgogoro wa Gedamari, Ayamango na Gidejabu; kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina sababu ya kuunga mkono hoja hii kwa namna yoyote ile. Watanzania wa Manyara watanishangaa, kwanza, fidia zao ndogo, maeneo yao yanachukuliwa hawathaminiwi, lakini hakuna popote wanaposikilizwa. Ninaomba Wabunge wenzangu, tukae chini tufikirie kwa nini tuunge mkono Wizara hii wakati hata Serikali inapopanga *ceiling* ya Bajeti ya Wizara hii wanatengewa fedha ndogo za maendeleo na hawapelekewi? Migogoro ya ardhi ipo mpaka Bagamoyo, ukiangalia taarifa za habari kila mahali ni migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inasikitisha, hata pale wananchi walipotoa migogoro yao kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, wale wananchi leo wapo Mahakamani. Mmoja ameshtakiwa na Diwani na nimemweleza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, Diwani huyu wa Chama cha Mapinduzi angekuwa CHADEMA angekuwa ameshafukuzwa; kwa nini mnamlea? Anashtaki wananchi wanaoeleza kero zao, anawadai fidia ya shilingi milioni 80; huu ni utawala bora? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakishangaa Chama cha Mapinduzi, naishangaa Serikali ya CCM, hata Viongozi tunawashtaki wananchi tunaowaongoza! Hii ni aibu, haifai. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Gekul, muda umekwisha.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa nimekuruhusu.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), ambayo inafahamika, nilikuwa naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Naomba uisome.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Hali kadhalika...

MWENYEKITI: Kanuni ya ngapi?

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Kanuni ya 68(7)

MWENYEKITI: Haya endelea.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa hapohapo au baadae kadiri atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ambacho sisi Wabunge tumepewa, katika ukurasa wa 31, yapo maelezo au mambo ambayo yametokea ambayo yanazungumzia kwamba, Wizara ya Ardhi imeamua kuingilia uhuru wa Mabaraza.

MWENYEKITI: Naomba uyasome.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Anasema: "Ili kupunguza kiwango cha mashauri yanayokatiwa rufaa kwenye Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na hivyo kuongeza ufanisi wao, nahimiza Halmashauri zote nchini kuwa ziandae mpango utakaowezesha kuyaimarisha Mabaraza ya Vijiji na Kata ili yaweze kushughulikia migogoro ya ardhi kwa ufanisi katika ngazi hizo. Pia nichukue nafasi hii, kuhimiza Wenyeviti wa Mabaraza haya, kutambua kwamba, Wananchi wamekuwa wakilalamikia Wizara kuhusu uadilifu na utendaji usioridhisha wa baadhi yao. Bila kupenda kuingilia uhuru wa Mabaraza, nimelazimika kuunda Tume ya kuchunguza baadhi ya malalamiko. Wale watakaobainika wana makosa watachukuliwa hatua stahiki."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Bungeni tumekuwa tukizungumzia dhana ya mashauri ambayo yako Mahakamani, lakini yalipokuwa yanatakiwa yazungumzwe hapa ndani tulikuwa tunaambiwa tusiingilie uhuru wa Mahakama na Mihimili mingine na hasa kwenye hilo suala la Madaktari. Sasa hapa Serikali hiyo hiyo ambayo imekuwa ikija na dhana hiyo ya kutoingilia, naona kwenye ukurasa huu inasema, bila kupenda lakini ameamua aingilie uhuru wa Mabaraza

haya katika mashauri ambayo yanahusu migogoro ya ardhi. Sasa nilikuwa naomba Mwongozo wako, kama inaruhusiwa Serikali kutamka bayana hapa Bungeni kwamba, sasa itaingilia uhuru wa Mabaraza haya japo ilikuwa haipendi. Nilikuwa naomba Mwongozo wako kama inaruhusiwa.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Lugola. Nimepokea, nitatoa maelekezo baadae. Tuendelee na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Mustapha Akunaay ajiandae.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi. Naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kutoa Hotuba yao vizuri sana, maana kila mtu anaangalia jambo kivyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, naomba nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka; anajitahidi sana, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Wizara hii ina changamoto nyingi sana, lakini mama mwenzetu anajitahidi, japo naomba nimwambie neno moja kupitia kwako; watamwita mkali sana, lakini ni vyema uitwe mkali kuliko uitwe mpole, ukiitwa mkali ina maana huburuzwi. Naomba uongeze huo ukali kidogo katika kutenda kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia kwamba, tuna kawaida kuona magazeti yanaandika vitu ambavyo labda havipo. Kuna *article* nimeisoma juzi, Siku ya Jumapili, ambayo imenitia wasiwasi

mkubwa. Gazeti la Nipashe la Jumapili, tarehe 8 Julai, 2012, ukurasa wa kwanza linasema: "Tanzania Kinara Kuuza Ardhi kwa Wageni."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili gazeti nitaomba lipitie kwako limwendee Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mambo yaliyozungumzwa hapa ni makubwa kidogo, kwa sababu kidogo tu inasema kwamba; inasemekana kuna dili la Serikali yetu kuimilikisha ardhi yenye ukubwa wa ekari zaidi ya laki tatu kwenye Bonde la Mto Rufiji, Mkoani Pwani, kwa Kampuni ya Muasia wa *bungalow* anayejulikana kama *Karutaki Global.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mwenyezi Mungu angeweza kulalamika tukamsikia, angeilalamikia sana Tanzania. Tanzania tumepewa maliasili nyingi sana tena kwa kupendelewa. Tanzania tumepewa ardhi yenye rutuba kuliko nchi zingine zote za Afrika Mashariki. Nitaomba Mheshimiwa Waziri asome hii *article* atuambie ni kweli haya mambo yanafanyika. Kama tutafikia au tumefikia mahali pa kuwapa wawekezaji ardhi zaidi ya ekari milioni moja imeandikwa hapa. Sasa Mheshimiwa Waziri ataikanusha au atatueleza, kwa sababu inaonesha kuna vielelezo vyote viko kwenye gazeti hili. Ni vyema Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, ikathamini ardhi ya nchi yetu, ikawa kwa faida ya Watanzania. Hatukatai wawekezaji wakitumia ardhi yetu, lakini wasifaidi wao kuliko sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba hiki kielelezo kifike kwa Mheshimiwa Waziri kupitia kwako, baada ya

mimi kumaliza hotuba hii kwa sababu nina vielelezo vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie jambo la pili; sisi viongozi tuliopo hapa ndani wa jinsia yangu nikiwa nina maana wanawake, pamoja na majukumu ya Kibunge ambayo tunayafanya, wengine ni Viti Maalum, wengine ni Wabunge wa Majimbo na wengine ni wa kuteuliwa, lakini ni lazima tuelewe kwamba, tunapaswa tuwe sauti ya Wanawake wote wa Tanzania ambao wanaonewa. Mimi nakuja mbele yako na lalamiko ambalo linaniuma sana. Kuna mama mmoja ambaye amekuja kwangu anaitwa Hellen Mrutu, ambaye ni mjane amefiwa na mume wake, aliyekuwa anaitwa Emmanuel Mrutu, aliyefariki tarehe 3 Aprili, 2010. Akina mama wenzangu, mnajua hakuna kitu kigumu kama kuwa mjane. Mume anafariki ghafla anakuachia watoto, lakini anakuachia na ardhi ikusaidie wewe na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke huyu alipokuja kwangu akanieleza nikasema mimi ni Kiongozi Mwanamke lazima niwe sauti ya wanawake wote bila ya kujali itikadi zao. Ameniletea vielelezo vyote na ni jinsi gani Watendaji wa Wizara wa Ardhi wamechukua ardhi aliyoiacha mume wake, ambaye ni urithi wake yule mama na watoto wake. Watendaji wa Wizara ya Ardhi wamefanya utapeli mkubwa, wameuza ardhi yote ya yule mama na kumwacha mjane na watoto wake wakihangaika na kila kielelezo kipo hapa ndani. Ninakusihi Mheshimiwa Waziri, nitaunga mkono hoja kama utamtendea haki huyu mama mjane, ambaye ameporwa ardhi yake na

Maafisa wa Wizara yako ya Ardhi. Nitaunga mkono hapo tu utakapomtendea haki mwanamke mwenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka nilikuwepo ndani ya Bunge wakati Mheshimiwa January Makamba akitoa hoja yake binafsi na sasa tunaomba tuletewe Muswada hapa wa Sheria ya Kudhibiti Upangaji wa Nyumba ambayo Serikali ilimuahidi kwamba, italifanyia kazi jambo hili. Sheria hii itamsaidia sana mnyonge yeyote wa Tanzania. Hivi Serikali kwa nini inapofikia wakati wa kwamba tuwasaidie wanyonge mnapata kigugumizi cha kutuletea huu Muswada? Wengi wanaoishi kwenye nyumba za kupanga jamani ni wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Muswada uje na kama hauji, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha atueleze kwa nini huu Muswada hauji. Yangu yalikuwa hayo matatu, pamoja na kusisitiza nitaunga mkono tu pale Mheshimiwa Waziri atakapomtendea haki huyu mwanamke mjane na nina uhakika anajua maana ya kuwa mwanamke mjane. Naomba nikwambie kwamba, nitaunga mkono hoja baada ya haya yote niliyoyazungumza kupata majibu sahihi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha nisimame hapa na muda ukiniruhusu nitazungumza mambo manne. Kwanza, nitaanza na Sera ya Taifa kuhusu Ardhi ya Mwaka 1995. Pili, matumizi ya ardhi. Tatu, bei za

nyumba nchini na fidia ya ardhi na mwisho Uwanja wa Azimio wa huko Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitu 15 ambavyo Sera ya Ardhi imevizungumzia, Sheria ya Mwaka 1995 inatamka mambo mawili. Ya kwanza ni kuhakikisha kwamba, Raia wa Tanzania anakuwa na umiliki wa hakika wa ardhi wa muda mrefu na wa kudumu. Katika hilo Serikali inatakiwa ihakikishe kwamba, ardhi ya nchi hii inapimwa na kila mmoja anayemiliki anapewa hati miliki. Mara nyingi Serikali imezungumzia na kupanga bajeti ya kupima mashamba ya wananchi katika nchi hii, lakini mpaka leo wananchi wengi wanaishi kwenye ardhi, kwa lugha ya kisheria wanaitwa *squatters,* ambapo saa yoyote anaondolewa na hana hati. Hiyo inaleta tatizo wakati wa kufidiwa kama barabara ikipita au eneo hili linachukuliwa kwa ajili ya matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limeleta tatizo kama Waheshimiwa Wabunge wengine walivyozungumzia juu ya fidia kwamba, mtu analipwa asilimia sita baada ya muda mrefu. Pia analipwa asilimia sita bila kujali thamani ya ardhi hiyo ni kiasi gani. Inatakiwa mtu alipwe fidia ya *market value* kama ardhi yake wakati ikinyang'anywa ilikuwa ni shilingi milioni mbili na leo ni shilingi milioni 300, basi alipe thamani ya shilingi milioni 300. Hiyo fedha ambayo analipwa *rate* ya miaka iliyopita ni dhuluma na kinyume cha Katiba ya Nchi yetu, Ibara ya 24 kwamba, kwa ruhusa yako naomba nisome kwa sababu hii ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba inasema: “Kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya kuhifadhi mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria”. Sehemu ya pili: “Bila kuathiri masharti ya ibara ndogo ya kwanza ni marufuku kwa mtu yeyote kunyang’anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au kwa madhumuni mengineyo, bila ya idhini ya sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili, yaani ndiyo ile *market value*.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa leo asubuhi kwamba, vijiji vichache ndiyo vimepimwa. Naishauri Serikali kwamba, Wananchi wa Tanzania kwa kupitia MKURABITA wapewe hatimiliki ya ardhi iwasaidie katika kukuza uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili ambacho nilitaka kukizungumzia ni juu ya Mabaraza ambayo imeelezwa katika ukurasa wa 31 kama mzungumzaji mmojawapo alivyoitaja. Mabaraza ya Ardhi imekuwa neno juu ya kero, yaani bughudha kwa sababu Wenyeviti hawa wa Mkoa na Wilaya wamekuwa wajeuri kiasi kwamba, kwa sababu hakuna anayewasimamia, hawamjui Jaji na Waziri wa Ardhi ambaye ndiyo mwenye dhamana ya kuangalia. Faili likiitwa mahali juu ya wakubwa wake hawaitikii, wanawatoza watu ada wanazotaka na kwa lugha nyingine wao ndiyo Wafalme wa eneo hilo. Kwa hiyo, tunashauri kwamba, haya Mabaraza yavunjwe yasiboreshwe, mashauri yao yarejeshwe katika Mahakama za Mwanzo ambazo zipo katika kila Kata badala ya kuwa na Mabaraza katika sehemu 42 sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba, anataka kuunda Tume, hana sababu ya kuunda Tume kwa sababu hata Mheshimiwa Jaji Mkuu ana taarifa zote za nchi nzima juu ya malalamiko ya hawa Waheshimiwa Wenyeviti. Jambo la tatu ambalo nataka kulizungumzia ni juu ya maendeleo ya makazi na nyumba. Nchi hii imekuwa ni tabu kubwa sana, kwa sababu ya bei ya vifaa vya ujenzi ambayo imekuwa ghali sana kutokana na kodi tunazotozwa kwenye vifaa vya ujenzi ikiwa ni saruji, bati, nondo na misumari. Hiyo ushahidi wake tumepewa juzi tulipopata semina ya nyumba za *National Housing;* nyumba ya shilingi milioni 21 inakuja kuuzwa kwa shilingi milioni 48. Sasa Serikali hii kama shughuli yake ingekuwa ku-*coordinate,* fedha hizi zingeondolewa. Hawa ni *National Housing* ambayo ni *corporate,* sasa mwananchi wa kijijini ambaye hana mkopo anayetaka kujenga nyumba ya vyumba vitatu inamchukua zaidi ya miaka 15 kuweka akiba ya kujenga hiyo nyumba mpaka ahamie anakuwa hana hamu nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wetu hapa ni kwamba, Wizara ya Ardhi iwasiliane na Wizara ili makazi ya watu yaendelezwe, iwasiliane na Wizara ya Fedha na *TRA* wakae chini maana hii *VAT* iliyoko katika hizi nyumba au kwenye hizi biashara mwisho wake anayetozwa ni huyu anayetaka kujenga nyumba ya bati anayetoka kwenye nyumba ya tembe. Sasa kama unatafuta kodi kwenye nyumba ya tembe; hii kodi itaendesha Serikali ipi maana hawa watu

watakwisha kwa maradhi, watashikwa na TB wanakaa chini ya udongo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifurahishwa na ile semina, tulimsikiliza Mwakilishi wa *National Housing* ametuonesha na picha za nyumba, nyumba ni nzuri na wamesema na zile za bei ya chini kwa ajili ya Wafanyakazi wa Serikali au Mashirika ya Umma wanaopata kipato cha chini kwamba, vyumba viwili tu ni shilingi milioni 21, ukiongeza kodi inakuwa shilingi milioni 48. Hakuna mfanyakazi mwenye shilingi 170,000 atakayeweza kukopeshwa na Benki kuweka *collateral* hiyo, kwa sababu mpaka amalize hata kazi yake hiyo fedha hataweza kuilipa. Ushauri wetu ni kwamba, Sera ya Kodi itazamwe upya, *fiscal policy* iende na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu matumizi ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji. Mgongano mkubwa unatokana na kutokuwa na ardhi iliyopimwa, mipaka inakuwa ni tabu baina ya mtu anayelima na yule anayefuga ng'ombe. Kwa hiyo, kama vitafanywa vipimo hivyo itajulikana kwamba, eneo hili limepimwa kwa ajili ya kufuga na hili kwa ajili ya kuchunga mifugo, basi matatizo hayo yatakuwa yamepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni kuhusu Uwanja mmoja kule Arusha, sehemu inayoitwa Sakina kuna uwanja mkubwa sana unaitwa Uwanja wa Azimio. Kule Arusha kuna vijana wengi sana wanaitwa Wamachinga, wanatembea hawana soko maalum, sasa Mamlaka

ya Mji wa Arusha *(Arusha City Council)* ingepewa mamlaka ya ule mji ili eneo hili lipewe iweze kuanzisha *Machinga Complex.* Mji ule watalii watapita kwa usalama. Kwa hivi sasa wanasababisha foleni mjini wakiwafuata watalii wawauzie mali zao, lakini wakipewa eneo maalum watalii watapelekewa pale kama eneo la maonesho na kivutio cha kufanyia nao biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu kudhibiti nyumba za upangaji kwa maana mbili; ya kwanza, wenye nyumba wanawanyanyasa wapangaji kama Mheshimiwa Anne Kilango alivyosema, lakini zaidi ni kwamba, hawa wamekuwa wanapokea fedha nyingi sana, ambayo hata Serikali haijui na kodi hawalipi. Tukianzisha Sheria ya *Estate Levy,* Serikali itapata fedha za kutosha badala ya kutegemea fedha ndogo ndogo kama tulivyozungumza kwenye Wizara ya Fedha, bodaboda, lakini hapa ndiyo kuna *rear tax.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika moja au mbili iliyobaki, nashauri katika Wizara ya Ardhi wale wanaopima viwanja nao ni wachache na wananchi wengi ambao wanataka kupimiwa ardhi zao wanashindwa kupima kwa sababu kiwanja kimoja mjini kinatozwa mpaka shilingi 1,300,000. Hiyo ni ghali sana na tunaomba hii taaluma iongezwe kwenye Wizara ya Ardhi ili tuweze kupima viwanja vyetu, tuwe na milki tuweze kufanya *collateral* kwenye mikopo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ahsante sana.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na uzima na kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008, Bunge la Tisa lilitunga Sheria Na. 17, inayohusiana na *Mortgage Financing.* Lengo la Sheria hii ni kuwawezesha Watanzania kupata mikopo ya muda mrefu ili wajenge nyumba za kuishi. Katika hili niseme tu kuwa, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* ndiyo Shirika la mwanzo ambalo limejitolea katika kuitekeleza Sheria hii ambayo nimeitaja na ushahidi ni kuwa, hivi karibuni Shirika hili limepata mkopo kutokana na Mabenki tisa, wenye jumla ya shilingi bilioni 165.4. Hivyo, ni dhahiri kuwa, Shirika la Nyumba limeaminiwa na mabenki kama tunavyoelewa maumbile ya mabenki mahali ambapo hawana uhakika wa kurudisha fedha zao basi hawatoi mikopo. Bila shaka inaonekana Shirika walijieleza vizuri, walitoa ushahidi kuonesha ufanisi ambao wanaufanya katika shughuli nzima za ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukichukua utendaji wa Shirika katika suala zima la ukusanyaji wa kodi ya pango, mwaka 2009/2010 Shirika lilikusanya jumla ya shilingi bilioni 35.82, mwaka 2010/2011 shilingi bilioni 44.44, mwaka 2011/2012 walikisia shilingi bilioni 43.14 na wamekusanya bilioni 53.17 na wanakadiria kuwa mwaka huu wa 2012/13 watakusanya shilingi bilioni 52.97.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonyesha ni kiasi gani Shirika la Nyumba liliaminiwa na mabenki kukopeshwa. Vilevile hatuna uzoefu mashirika ya umma kuchangia fedha kwa Serikali. Kwa kawaida, mashirika yetu kama *ATCL* na mengineyo ni kupata fedha kutoka kwa Serikali, lakini hili kwa ufanisi wake, mwaka 2009/2010 mchango wake kwa Serikali ilikuwa ni Shilingi bilioni 3.73; mwaka 2010/2011 ilikuwa Shilingi bilioni 8.89; mwaka 2011/2012 ilikuwa Shilingi bilioni 14.6 na wanategemea mwaka huu 2012/2013 kuchangia Shilingi bilioni 24.18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba linaonekana dhahiri kwamba limejipanga katika kuhakikisha wananchi wanapata nyumba zilizo bora ingawa niseme tu kwamba nyumba bado ni ghali. Lakini kujipanga kwa Shirika kutasaidia kiasi fulani, lakini ipo haja Serikali nayo kujipanga ili kupokea haya mabadiliko mapya. Wachangiaji wengi, Kamati ya Ardhi na Kambi ya Upinzani wamesema *VAT* ambayo ni ongezeko la thamani, iondolewe. Mimi naungana mkono nao, lakini sasa Serikali wakati wanafikiria kuiondoa hiyo, nashauri waangalie mambo matatu.

La kwanza, nini mchango wa Serikali moja kwa moja kwenye Shirika juu ya unafuu wa bei za nyumba? Dunia ya leo, zipo Serikali ambazo zinawajengea nyumba wananchi na kuwapa bure. Zipo nchi ambazo ushuru wa vifaa vya ujenzi Serikali zimesamehe. Sasa leo nitashangaa sana Serikali kushindwa kusamehe *VAT* katika Shirika la Nyumba. Hii itakuwa ni mtihani mkubwa. Kwa hiyo, naomba katika kulifikia hili ombi la kuondoa *VAT* katika nyumba mpya ambazo zinauzwa

na Shirika la Nyumba, basi waone kuwa Serikali walikuwa na wajibu, wawajengee wananchi. Kwa hiyo, Shirika limewasaidia mzigo.

La pili, ni njia ya kuwezesha Shirika kuweza kushiriki katika biashara hii ya nyumba ikilinganishwa na sekta binafsi. Inaweza ikazuka hoja kuwa hii *VAT* iko katika mauzo ya majengo yote ambayo yatajengwa ikiwa ni Shirika au watu binafsi. Lakini ninachotaka kuwaambia, uzoefu wa Tanzania ulivyo, kama sekta binafsi itajenga nyumba, watakuwa na uwezo wa kukimbia kiwango cha *VAT* ambacho kinatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna nyumba hapa za Medeli zinauzwa Shilingi milioni 100. Kama zingekuwa za mtu binafsi, angeweza kumwambia kubali kwenye risiti iandikwe Shilingi milioni 70, ukifanya hivyo basi, mnunuaji anapata ahueni au tahfifu ya Shilingi milioni 5.4. Yaani badala ya nyumba kuuzwa Shilingi milioni 118 itakuwa Shilingi milioni 112.4 kwa risiti tu. Kwa hiyo, unapoweka Shirika lilipe, ina maana watakapoingia sekta binafsi katika nyumba, hawa watatolewa nje ya mchezo huu wa ujenzi wa nyumba. Kwa hiyo, lazima *VAT* ya asilimia 18 kwa nyumba za Shirika lazima iondoshwe, vinginevyo Shirika hili linaweza likafa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuepuka ubaguzi. Kuna wakala wa majengo iko chini ya Wizara ya Ujenzi wanauza nyumba zao bila *VAT.* Iweje Shirika la Nyumba liingiziwe *VAT?* Au kwa sababu wanunuzi wa nyumba hizi ni wakubwa? Wanyonge hawana haki hii? Kwa hiyo, hili tunaomba Serikali kwa kupitia Wizara

ya Fedha waliangalie na kwa sababu *Finance Bill* bado, Kamati yangu ilisema mwakani, lakini mimi nasema mwaka huu 2012/2013 kwa sababu *Finance Bill* bado. Halafu hili suala la *VAT* katika majengo, nahisi ni suala la nadharia. Ukweli wa mambo, mimi nafikiri Serikali haipati kitu. Watapata kwa Shirika la Nyumba, Shirika lao, kwa hiyo, wataliua wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali linadaiwa na Shirila la Nyumba. Serikali inadaiwa Shilingi bilioni 2.4, lakini wao mwaka huu wamepewa Shilingi bilioni 14.6 na Shirika hilo hilo. Ni jambo la ajabu. Mtoto wako kakupa Shilingi bilioni 14.6, wewe hutaki kumpa Shilingi bilioni 2.4 aendeleze ambapo mwakani huyu atakupa Shilingi bilioni 24. Kwa hiyo, naishauri Serikali ilipe deni hili. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Naomba nikiri wazi kwamba ninampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa - Mwalimu Nyerere, pamoja na *concept* ya uchumi, inasema: “Ili tuendelee, tunahitaji mambo manne; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najikita katika ardhi kwa sababu siku ya leo tunajadili kuhusu ardhi. Nchi yetu ni tajiri sana katika ardhi na tuna haki ya kujivunia

kwa sababu tuna ardhi kubwa, nzuri, yenye rutuba na yenye eneo kubwa. Lakini tatizo ni kwamba, hii sifa ya ardhi ambayo nchi yetu inajivunia, ndiyo imekuwa yenye migogoro na utata mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Serikali kwa maana ya kwamba imeweza ku-*introduce* hatimiliki ya kimila. Watanzania wengi zaidi ya asilimia 70 wanaishi vijijini na huko vijijini ndiko tunakozungumzia hati milki za kimila. Lakini Watanzania hawa wamekatishwa tamaa kwa sababu wapotaka kupimiwa ardhi yao na Maafisa Ardhi ambao ni wachache, na hii tunasema inaweza ikawa inatengeneza *chain,* wanakatishwa tamaa. Hawapati hizi hatimiliki za kimila. Kama unavyoelewa, huwezi kwenda benki kuomba mkopo kama huna hatimiliki za kimila. Sasa Watanzania hawa wataendeleaje? Mimi ningeishauri tu Serikali kwamba, hili suala la kutoa hatimilki za kimila lifanywe na Wizara yenyewe moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie masuala ya makazi holela. Mimi ni Mbunge wa kutoka Mbeya, tunapozungumzia makazi holela, ninamaanisha *squatters*. Unapoingia kwenye lango la Mbeya unakumbana na sehemu inaitwa Uyole. Lakini sisi Wanambeya, kwetu ardhi ni muhimu asubuhi, mchana na jioni. Kwa sababu ukizungumzia kilimo, ni ardhi; viwanda, ni ardhi; elimu, ni ardhi; biashara, ni ardhi; na kila kitu kiko juu ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoingia kwenye lango la Mbeya unakumbana na eneo la Uyole, ni

squatters; ukija Ilomba, Ilemi, Soweto, Somve, Iyunga, Ilemi, Isanga, Mwakibete kote ni *squatters*. Sasa ningependa kujua Serikali ina utaratibu gani kuhakikisha kuwa Jiji la Mbeya linaondokana na hii athari ya kuwa *squatter*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna majiji matano katika Tanzania na Mbeya likiwemo. Lakini ninaamini kwa zaidi ya asilimia 95, Mbeya yangu ndiyo inayoongoza kwa kuwa na makazi holela. Naomba sana Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hoja yake anipatie majibu, ana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba Jiji la Mbeya linaondokana na hii adha ya kuwa na makazi holela bila ya kuwabughudhi wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba wanawake ndiyo wachapakazi hodari katika kilimo, ufugaji, hata kwenye masuala ya familia, na katika biashara. Hao wanawake linapokuja suala la hatimilki ya kimila inakuwa ni matatizo. Hii ni hatari sana. Naomba hili liangaliwe, na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi anapojumuisha hoja yake aweze kunipatia majibu ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo na kuna desturi ya watu fulani kuvamia maeneo ya wazi. Hii ni hatari kubwa sana. Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, wameanza kazi vizuri, wanaifanya kazi vizuri na wakaze buti, haya mambo yanayotokea, hawa watu wanaovunja Sheria, hakika mkaze buti. Hakuna kuogopa! Sisi tuko nyuma yenu, tutawa-*support* na tuone utekelezaji wake kwa matendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye suala la Shirika la Nyumba. Nawapongeza sana Shirika la Nyumba, na sisi sote humu ni mashahidi na nimesikia Wabunge wengi wakilipongeza Shirika la Nyumba. Kwa kweli hili Shirika limekuwa *reformed,* maana wote tunajionea kwa vitendo. Nyumba nyingi za matabaka mbalimbali zinajengwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kule Mbeya bado tunawasubiri.Lakini tukumbuke kwamba, hili Shirika vilevile lilikuwa linadaiwa huko nyuma. Lilikuwa kama limekufa na sasa hivi lina *surplus*. Kwa kweli ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeambiwa kwamba hili Shirika linaidai Serikali Shilingi bilioni mbili. Tukumbuke kwamba hili Shirika la Nyuma lina vijana ambao ni *very energetic, creative management team.* Hilo lazima tuseme. Mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumezungumzia masuala ya nyumba zinazojengwa na Shirika hili la Nyumba kwamba kodi yake ni kubwa sana na Watanzania walio wengi ni wa kipato cha chini, hawawezi kumudu. Sasa tufanye nini? Bila utata ni kwamba, tatizo moja kubwa hapa kama siyo mawili, tunapozungumzia ongezeko la thamani *(VAT),* ni kubwa! Kwanini hili Shirika liendelee kutozwa *VAT* wakati hizi nyumba ni kwa ajili ya Watanzania wote, hususan wale wa kipato cha chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kwamba *VAT* iondolewe kwenye hili Shirika la

Nyumba ili liweze kujiendesha vizuri na Watanzania waweze kumudu kununua hizo nyumba ambazo tunalalamika kwamba bei yake ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunapozungumza kwamba hizi nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa bei, ni kubwa. Tuangalie miundombinu, wanapokwenda kujenga katika hayo maeneo, kila kitu inabidi wafanye wao wenyewe. Kama ni masuala la maji, kama ni masuala ya umeme, kama ni masuala ya barabara, wanafanya wao wenyewe. Naiomba Serikali isadie kutengeneza miundombinu kama ya barabara, maji na vinginevyo ili hili Shirika liweze kuendelea kufanya kazi zake vizuri kuliko kuwaachia kila kitu na *burden* ikawa kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho hakiingii akilini kabisa, ninashangaa ni kwamba Shirika la Nyumba ambalo ni mali ya Serikali, leo hii tukizungumzia kwamba zile *assets* zake ziende *TBA,* sielewi kabisa! Ni kwanini ziende *TBA?* Kwa sababu zote ni za Watanzania, na mapato yote yanayopatikana ni kwa ajili ya Serikali. Sasa nitashangaa sana! Kwanini hizi *assets* za Shirika la Nyumba zitoke ziende *TBA* wakati wote ni watoto wa baba mmoja na mama mmoja? Hii itatuletea kizungumkuti, hakuna haja ya kutoa *assets* kwenye Shirika la Nyumba kwenda *TBA* kwa sababu wote ni watoto wa baba mmoja na mama mmoja na mapato ni yaleyale. Hii itatufanya tujiulize, kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisizungumze sana, wala nisigongewe kengele la pili, yangu yalikuwa

ni hayo machache katika kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Ardhi. Nawapongeza tena Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kazi yenu ni nzuri, mkaze buti, wala msikatishwe tamaa, songeni mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijaalia jioni ya leo kuweza kusimama hapa katika Bunge lako hili. Muda wenyewe ni mdogo, naomba niende moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni mali, ardhi ni mtaji. Ardhi ndiyo mali pekee ambayo ingeweza kumwokoa Mtanzania wa kipato cha chini, lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi wameshindwa katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tanzania, ardhi ni mtaji mfu. Kwanini nasema hivyo? Ni kwa sababu Watanzania wengi wameshindwa kumilikishwa ardhi. Miaka 50 ya Uhuru mpaka leo, asilimia 90 ya ardhi ya nchi yetu haijapimwa. Kwa kweli hii ni hatari. Naomba nimnukuu Mheshimiwa Waziri, tarehe 1 Desemba, 2010 alipoteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, aliongea na Waandishi wa Habari. Naomba ninukuu machache ambayo aliyasema: “Ni asilimia 10 tu ya ardhi ya Tanzania ndiyo imepimwa na ardhi ni muhimu kuliko fedha. Hivyo, inapaswa kurasimishwa ili iwasaidie wananchi.”

Mheshimiwa Waziri, Watanzania bado wana imani na wewe, tunakuomba ulifanyie kazi na ukaze buti katika hili na mimi pia nina imani na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge kutoka Mkoa wa Tanga. Nitakuwa sijawatendea haki wananchi wa Tanga nisipoiongelea Tanga, na kwa sababu muda wenyewe ni mdogo, naomba niongelee Halmashauri ya Jiji la Tanga. Jiji la Tanga wakati ukiwa Mji wa Tanga hapo kabla, ni Mji ambao umepangika vizuri sana kwa sababu ya Idara ya Mipango Miji hapo kale. Sio sasa hivi. Idara ya Mipango Miji kwa sasa hivi ina changamoto nyingi sana ikiwemo watendaji ambao sio waadilifu, fedha pungufu, vitendea kazi hakuna, lakini kubwa kuliko yote ni changamoto ya mashamba ya Mkonge ambayo yametelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba haya yanafanya upungufu katika upimaji wa viwanja. Lakini tunashukuru kwa sasa hivi Sheria inaonyesha kuwa haitakiwi kuwa na *Estate* ndani ya Majiji. Kutokana na sheria hiyo, Halmashauri ya Jiji la Tanga lilikaa na likapendekeza Hati 10 za mashamba hayo ya mkonge zifutwe, wanyang'anywe umiliki kwa sababu Majiji sasa hivi hayatakiwi kuwa na *Estate* kama hayo mashamba ya mkonge. Wananchi wanakosa ardhi kwa sababu katika Jiji pia kuna na vijiji. Vile vijiji vinakosa mashamba ya kulima na wananchi wale wanateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo ni pamoja na *Malungwe Estate, Mkembe Estate, Amboni Estate*

ambayo imekwenda mpaka Mabokweni, kuna Uroa katika eneo la Pongwe na mengineyo ambayo tumeomba hati zake ziweze kufutwa. Nina imani kwa sababu Mkuu wetu wa Mkoa ni mwanamama mchapakazi, Halmashauri wameshapeleka kwake. Nina imani mama yule na yeye ameshaifanyia kazi na nina imani kuwa imeshafika sehemu husika. Namwomba Mheshimiwa Waziri akija hapa katika majumuisho, aniambie kama suala hili limefika kwenye dawati lake, lakini pia aniambie kama analifahamu na limefikia wapi. Ni muhimu sana kwa wakazi wa Jiji la Tanga, wanateseka, hakuna maeneo. Hao wawekezaji wenyewe ni matapeli, wameyatelekeza maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pande B ni kijiji ambacho kilikuwa na mgogoro wa ardhi, kati ya Wanakijiji wa Pande B na mwekezaji ambaye ni *Tanga Cement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi analifahamu hili, na mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Nampongeza, ameweza kutembelea Pande B na amesaidia kwa kiasi fulani, kwasababu kulikuwa na mgogoro mkubwa sana kuweza kuleta amani katika eneo lile. Kwa hiyo, kulipatikana utulivu, wananchi wale walipata imani na Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri imani hiyo uitumie vizuri kwasababu bado mgogoro upo, wananchi wale hawajapata haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa walizonazo wao kwa sasa hivi ni kwamba, tathmini itafanyika upya, kutapimwa upya na waweze kutambulika wale ambao

ni wamiliki halali wa yale maeneo, kwa sababu kuna watu wengi wametapeli na kuweza kupata haki yao. Nakuomba Mheshimiwa Naibu Waziri, ukija hapa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge katika hili, useme umefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie kwenye *EPZ.* Naishauri Serikali kwamba kama hamjakuwa tayari katika miradi, msiwataarifu wananchi. Mnawasumbua! Haiwezekani leo eneo la neema, zaidi ya miaka minne limeshafanyiwa tathmini, wananchi wale wanahaha. Wakati niko kwenye kampeni mwaka 2010 kabla sijawa Mbunge, walikuja wakaniomba, mpaka leo tuko mwaka 2012, bado hawajalipwa fidia. Hebu niambieni kwanza, mtawalipa fidia kwa thamani ya fedha ya mwaka huo, miaka minne nyuma au sasa hivi? Lakini pia mnawasumbua!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba, chonde chonde, kama hamjawa tayari kufanya mradi wowote, ni bora mkasubiri, kuliko kuwasumbua wananchi, ambao ni Watanzania. Kwa suala hili la neema, kwasababu wananchi wale wako njia panda na ninajua Wabunge wote linawagusa katika maeneo yao, naomba kujua, wale wananchi watalipwa? Ni lini watalipwa? Kwa sababu wamekaa muda mrefu, hiyo thamani ya pesa yenyewe imekwishakuwa ni ndogo sana kwa sasa hivi. Naomba kama itawezekana, basi walipwe kwa thamani ya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa haraka haraka niende kwenye suala la makazi holela. Tanzania jamani tuna Wizara nzima ya Ardhi, Nyumba

na Maendeleo ya Makazi, tuna Chuo Kikuu Kishiriki kinashughulika na ardhi tu, tuna Idara na Mipango Miji katika kila Halmashauri na Mabaraza ya Miji, lakini cha kushangaza, kuna makazi holela yanaongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 75 ya Watanzania wanaoishi Mijini, katika Majiji yetu ya Dar es Salaam, Mbeya, Arusha na Mwanza wanaishi katika makazi ambayo siyo rasmi, hayakupimwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri, na ninajua Mheshimiwa Waziri ni Mtaalam katika hili na ana uzoefu mkubwa alipokuwa *UN–HABITAT* na mimi siku moja nilishawahi kumsikia katika *TV* kabla hajawa Waziri, alinivutia sana wakati akielezea jinsi ambavyo ana uwezo mkubwa katika makazi na akaelezea Jiji la Dar es Salaam ambavyo bado halijajaa, alieleza kwa umakini mkubwa na ninamwamini, najua anayo nafasi kwasababu ni mwaka mmoja na nusu aweze kuhakikisha makazi holela anayafanyia kazi kama alivyoahidi katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia la mwisho kabla sijagongewa kengele, niungane na Wabunge wengine waliopita kuunga mkono hoja binafsi ya Mheshimiwa Makamba, aliyoileta Bungeni ya *Land Rent.* Hii ni muhimu sana kwa wananchi wetu ambao ni wengi wa kipato cha chini, wanateseka sana na hii kodi ya mpango. Naomba Mheshimiwa Waziri alete huo Muswada kama alivyosema Mheshimiwa Anne Kilango, ili tuweze kuwasaidia Watanzania na kujisaidia sisi wenyewe pia. Siyo aibu kuiga kwa wenzetu hapo jirani, Zambia. Wana *Land Rent* ambayo mpangaji

hatakiwi kulipa zaidi ya miezi mitatu. Lakini Tanzania ya leo siyo mwaka tu, mpaka miaka miwili. Kila mtu anacheza kivyake. Nakuomba Mheshimiwa Waziri hili ulifikirie. *(Makofi)*

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Ardhi. Naomba nianze kwa suala la uwekezaji katika ardhi tunatambua kwamba Sheria yetu inakataza uwekezaji au inakataza kwa mtu ambaye siye Mtanzania kumiliki ardhi kulingana na mujibu wa Sheria kifungu cha 20, Sheria Na. 4 ya Ardhi ya mwaka 1999. Lakini mwekezaji huyo pia amepewa fursa ya kuomba umiliki wa ardhi kupitia *TIC* kwa maana ya *Tanzania Investment Center,* na pale ambapo mwekezaji huyo anapitishwa, basi *TIC* huweza kumkabidhi mwekezaji kwa Benki ya Rasilimali, Benki ya Ardhi ili mwekezaji huyo aweze kupatiwa ardhi. Lakini tunajua kuwa benki hiyo haina ardhi ya kutosha ya kuweza kumpatia mwekezaji huyo. Basi mwekezaji naye hupata fursa ya kutembea nchi nzima kutafuta ardhi, hapo ndipo ambapo panaanza kuleta matatizo, ndipo ambapo panaleta migogoro kati ya mwekezaji na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wawekezaji hawa, wanawarubuni wananchi, wanatoa rushwa, wanawashinikiza katika Mikutano yao Mikuu ya Vijiji ili waweze kuwapatia ardhi au kwa kuwadanganya kwa vitu voidogo vidogo kama kuwachimbia visima, kujenga shule na madarasa ilihali haya yote hayawezi kutendeka. Pale ambapo wanapata tu wanachotaka, hakitendeki chochote tena, ilimradi huyu mwekezaji

ameshakidhi kile anachokihitaji. Naomba sana, na ninaishauri Serikali kwa wale viongozi wote ambao wanasimamia masuala ya ardhi na mamlaka husika, zisiingiliwe, zibaki huru na zifanye kazi yake, itekeleze majukumu yake ili haki iweze kutendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali iendelee na jukumu lake la kutoa elimu kwa wananchi. Wananchi hawa wapate elimu ya kutosha juu ya kuweza kuuliza maswali yote yanayohusu ardhi ili waweze kupata uelewa mkubwa na wasiweze kurubuniwa na aidha mwekezaji au watu wowote ambao watataka kurubuni ardhi ya wananchi hawa. Ikumbukwe kwamba, ardhi kwa mwananchi wa kawaida ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nigusie suala la migogoro ya ardhi. Katika Wilaya ya Karatu, kumekuwa na migogoro na uvamizi wa maeneo ya wazi. Maeneo haya yamevamiwa, yamejengwa bila utaratibu na bila vibali maalum. Tunaiomba Wizara ishughulikie matatizo ya ardhi Karatu. Kuna matatizo makubwa ambayo yanaweza yakapelekea uvunjifu wa amani. Sasa hivi hatuna ardhi, kuna tatizo liko pale linaendelea sasa hivi, kuna vijana ambao wanajishughulisha na masuala ya gereji wametakiwa kuondoka ili kupanga Mji. Kimsingi, sipingani na Halmashauri yangu kupanga Mji, lakini: Je, waliwashirikisha vizuri vijana hawa? Vijana hawa wanawaondoa, wanawapeleka wapi? Tunaomba Wizara iingilie kati, itatue matatizo ya migogoro ya ardhi katika Wilaya ya Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee suala la mgogoro wa ardhi Karatu, baina ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na vijiji vinavyopakana na Hifadhi hii. Kumekuwa na migogoro ambayo inaendelea kila siku, kumekuwa na uvunjifu wa amani, nah ii inapelekea watu kufungwa na kusingiziwa kesi mbalimbali. Tunaomba Mamlaka zinazohusika, kwa maana ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Halmashauri ya Karatu, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara hii ya Ardhi ikae na wananchi hawa ambao wananyanyasika, waweze kupatiwa ufumbuzi wa tatizo hili ambalo limedumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee suala la baadhi ya vijiji katika Wilaya ya Karatu ambavyo maeneo yake yameshikiliwa na baadhi ya Wazungu na Wahindi ambao wana Hati ya kumiliki ya kuanzia miaka ya 33 mpaka miaka 99, ambao wako pale kwa muda mrefu. Wawekezaji hawa wanawanyanyasa sana wananchi, wanapelekea kuwabambikizia baadhi ya wananchi kesi kwa uvamizi wa maeneo yao na baadhi ya wananchi wamefungwa na kesi nyingine zinaendelea. Tunaiomba Wizara ije Karatu, ikae na wananchi hawa ambao wananyanyasika, wamekaa pale kuanzia miaka ya 1970 mpaka leo, halafu wanaambiwa ni wavamizi. Tunaomba Waziri aje akae na wananchi hawa, wananchi hawa washirikishwe ili matatizo haya yaweze kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie suala la ubadilishwaji wa matumizi ya ardhi. Wazungu hawa ambao wanamiliki mashamba ya mikataba pale

Karatu na kwa Mkoa wa Arusha kwa ujumla, mwanzo walipewa mashamba haya kwa lengo ya kilimo, kwa maana ya kilimo cha Kahawa na mambo mengine. Lakini wameanza kufanya ujanja kwa kubadilisha matumizi ya ardhi kwa kujenga mahoteli ya kitalii. Tunafahamu kuwa Mji wa Karatu ni Mji wa kitalii kwa sababu unapakana na Hifadhi ya Ngorongoro. Kwa hiyo, hawa wanabadilisha matumizi na hatuna uhakika kama wamepata vibali vya ubadilishaji wa matumizi ya ardhi hii, lakini pia inakosesha Serikali mapato, kwasababu kama alikuwa anamiliki ardhi kwa ajili ya kilimo, alikuwa anatozwa kodi ya Sh. 200/= kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama leo ana hoteli za kitalii mle ndani, anaingiza wageni, wanalala pale: Je, Serikali inapoteza kodi kwa kiasi gani? Ni kiasi kikubwa. Tunaomba Waziri kwa hili, atupe majibu. Tunataka kujua, hao wawekezaji ambao wako hapo muda mrefu, waliobadilisha matumizi ya ardhi hii kama kweli wamefuata taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mashamba ya mikataba ambayo hayajaendelezwa, yameachwa au kutelekezwa. Tunaomba pia Waziri atupe majibu, kuna vijana wengi wa Karatu hawana ardhi, kuna vijana ambao wanaanza maisha, wanahitaji ardhi, kwa hiyo, tunaomba tujue mashamba haya yamefikia wapi? Kama hayaendelezwi tena, yapelekwe Halmashauri na Halmashauri iwagawie vijana hawa kwa haki bila upendeleo wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwenye suala la Mabaraza ya Kata. Tunafahamu kuwa tuna mfumo huu wa kujaribu kupunguza au kutatua migogoro ya ardhi, lakini hatujaona ufanisi wa Mabaraza haya. Mabaraza haya ya Kata yametelekezwa, Mabaraza haya hayawezeshwi kwa chochote, iliahidiwa kwamba Makatibu wa Mabaraza haya watalipwa, lakini hatujaona kinachofanyika. Athari ya hii ni kuongeza rushwa na kuendelea kuongeza migogoro, na haki haitaweza kutendeka kwa wakati. Tunaomba aidha, Serikali ibadilishe mfumo huo wa Mabaraza au iboreshe zaidi ili iweze kutoa haki na tuone kwamba haki inatendeka na kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuchangia hoja ambayo Wabunge wengi pia wamechangia kuhusiana na suala la Muswada wa Sheria ya kuwa na mahusiano kati ya Mpangaji na mwenye nyumba. Ikumbukwe kuwa suala hili pia lilisemwa na Kambi ya Upinzani katika bajeti yao ya mwaka 2010/2011. Hivyo hivyo katika mapendekezo ya bajeti yetu kwa mwaka huu. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ilete Muswada huu kuondoa manyanyaso ambayo wanayapata wapangaji kama ambavyo walisema na hasa vijana wanaoanza maisha. Nashukuru sana. *(Makofi)*

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika mjadala wa bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Ardhi na Makazi.

Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi pamoja na Naibu wake na Watumishi walio chini yake kwa kuja na hotuba moja ambayo ni nzuri, inayojali matakwa ya Tanzania ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuliona tatizo ambalo linaisumbua nchi hii. Ukienda katika ukurasa wa 40 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa maneno yenye msisitizo ameandika: “Ili kuharakisha upangaji na upimaji wa ardhi, Halmashauri zote nchini zinashauriwa kununua vifaa vya kisasa vya upimaji ardhi. Ni jambo la kusikitisha kwamba, katika Halmashauri kadhaa, wapimaji hawana hata darubini ya kawaida, achilia mbali vifaa vya kisasa kama *GPS.* Hii siyo kwasababu ya umasikini, bali kutoelewa kuwa fani hii haiwezi kuwa na manufaa bila kuwa na vifaa vya msingi.” Hapa ndipo ninapotaka nizungumzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inapata shida kwa sababu ya matatizo ya kujitakia na haya matatizo ya kujitakia yanakuwa na manufaa kwa baadhi ya watu. Kitendo cha kutokuwa na vifaa vya kupima katika maeneo mbalimbali ya nchi hii, kimekuwa ni chanzo cha migogoro mbalimbali inayoendelea nchini mwetu. Maana unakuta viwanja vinavyopimwa ni vichache, wananchi wanahamia Mjini kwa kasi na wanataka kujenga, viwanja havipo, wanavamia viwanja vichache na matokeo yake sasa mabwana ardhi na watumishi wa ardhi wanavitumia viwanja hivyo vichache kugombanisha watu na kuwa chanzo cha rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwamba Wizara ijipange sasa kupima nchi hii. Ardhi yetu ipimwe iwe katika mazingira mazuri ambayo yatawawezesha Watanzania wa nchi hii kuwa na umiliki halali unaokubalika, maana ustaarabu katika dunia hii umetokana na makazi. Nchi mbalimbali duniani, ukitembelea utaona wenzetu waliostaarabika siku za nyuma Miji yao imepangwa kwa utaratibu unaokubalika. Ajabu, kwetu hapa tunajua kuwa tatizo lipo, lakini tulikuwa hatujui chanzo chake ni nini. Ni kwasababu Wizara yenyewe ilikuwa bado haijatambua tatizo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wenzake kwa kutambua chanzo cha mgogoro wa makazi holela, napo hapa naomba ninukuu tena katika hotuba yake ukurasa wa 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukuonyesha wazi kwamba mimi hapa sina kingine cha kufanya isipokuwa kumpongeza Waziri wa Aridhi kwasababu ameshalielewa tatizo, na ninaamini kwamba sasa tutapata ufumbuzi wa kudumu, amesema: “Halmashauri zote nchini zinaagizwa zihakikishe kuwa zinapima viwanja na kuvigawa kwa wananchi ili kuepusha ujenzi holela. Wananchi wanaokaidi mipango Miji na kujenga kiholela, kuvamia maeneo ya wazi na kujenga katika maeneo yanayolindwa kisheria hususan fukwe na maeneo hatarishi, wasitegemee kupewa fidia wakati wa kuhamishwa. Tuko tayari kupokea maombi yenu, kupewa viwanja au nyumba kuliko kupoteza akiba yenu kujenga visivyo.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninamkushukuru Mheshimiwa Waziri, kwa mara nyingine naomba tu

kuwa wataalam wa upimaji wapelekwe katika maeneo mbalimbali na ikiwezekana kuanzia vijijini, maana vijiji ndivyo vinavyozaa Miji midogo, na ndiyo vinakuja kuzaa baadaye Halmashauri za Miji, baadaye Manispaa na baadaye Majiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kosa likianzia katika kijiji kwamba hakijapimwa, matokeo yake kitaendelea kukua kama *squatter*. Ili kutatua tatizo hili sasa, ninaishauri Wizara na Serikali kwa ujumla ianze utaratibu wa kuwa na wapimaji kuanzia ngazi za vijiji. Vifaa vya upimaji viweko huko ili kusudi tuanzie katika *nucleus* yenyewe ambayo ndiyo chanzo cha tatizo vijiji ndivyo vinavyoanzisha Miji sasa, visipopimwa vizuri vijiji hivi, matokeo yake tunakwenda kwenye *squatter.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa hatua za mwanzo. Kwa mfano ilipokuwa imedhamiria kuanzisha vijiji vya ujamaa na wananchi wakahamishiwa katika vijiji, lengo lilikuwa ni zuri. Lakini baadaye vijiji hivi vilikuja vikavunjwa, vingine utaratibu ukawa haueleweki, watu wengine wakarudi tena Mahameni. Vijiji hivi vimekuwepo na vingine vimekuwa katika utaratibu ambao siyo. Vijiji vilivyokuwepo pale mwanzo vilikuwa vimepimwa vizuri, unamkuta mtu ana eneo lake ekari moja ambayo inaweza ikamsaidia kujenga nyumba za kisasa na kuwa na eneo ambalo linamfanya mtu huyu aishi maisha ya kistaarabu. Atakuwa na nyumba, atakuwa na miundombinu, kama ni choo, lakini kwa sasa hivi unakuta maeneo mengine ni *squatter,* mtu hawezi kupata huduma, hawezi kujenga na kupanua makazi yake kwa sababu watu hawa wanabanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia mbaya ya Watanzania ni kwamba, sasa hivi mahali ambako wanapaona kwamba panakuwa ni *centre,* kijiji chote wanahamia pale. Wakishahamia pale, unakuta matatizo yanaanza. Ikitokea ajali kama ya moto kijiji kizima au soko zima linaungua kwa sababu halikupimwa. Watu wapo pale tu na hawaelewi tatizo ni nini. Lakini tatizo ni Watanzania wenyewe kutokuelewa. Tunakuwa sasa hatutofautiani na mnyama, maana mnyama akimwona mwenzake anafanana naye, anaambatana naye mpaka huko hata kama haelewi anakwenda wapi. Lakini sasa hawa ni Watanzania ambao ni watu wazima, watu ambao wanaelewa, lakini wamekuwa na tabia kwamba *centre* moja ikianza, wote wanaanza kwenda. Pale atajenga mmoja, mwingine anajenga nyuma yake, mwisho hawawezi tena sasa kujua wafanye nini. Tukija kutaka kuwahamisha au kuanza kuwapanga upya, mgogoro unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sasa Waziri kwa sababu ameshaliona tatizo hili, Serikali ichukue hatua za haraka na za makusudi kuwaajiri wapimaji kwa wakati mmoja wengi na kuwasambaza katika maeneo mbalimbali kuanzia vijijini, kwenye Kata, na Tarafa. Hawa watu wawepo, ndiyo watakuwa wanawaelekeza wananchi hawa. Watalaam hawa wamesomeshwa kwa pesa ya wali

pakodi ili waje wawasaidie Watanzania ambao hawaelewi. Watu wengine wanafikiri kwamba wanapokuwa wapo pamoja, wanaona kwamba ni

usalama. Sawa, lakini sasa usalama wakati mwingine tena inakuwa ni chanzo cha ghasia. Ndiyo maana unakuta kuna maeneo mengine kutokana na kuwa *squatter,* yanakuwa na majina mengine magumu. Unakuta kuna maeneo yanaitwa Chechnia, mengine yanaitwa Kosovo, kwa nini? Kwa sababu watu wamekaa zigzaga. Hawana choo, hawana kila kitu! Ni kwamba wanaishi kama wanyama, utafikiri wanaishi zizini! Maana mtu hana choo, hana njia ya kumtoa endapo itatokea dharura, hana njia ya kutokea endapo atatakiwa kwenda hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja hii. Naomba kwa maeneo ambayo sisi tuna maeneo mapya, Wilaya yangu ni Wilaya mpya na Mkoa wa Geita, sisi hatujawa na *squatter.* Sasa ndiyo tunakwenda kuanza katika hizi Wilaya ambazo kuna mpango wa kuzipimia viwanja elfu 40. Naomba katika Mkoa wetu wa Geita na Wilaya zake mpya Mheshimiwa Waziri uvigawe hivyo viwanja ili kusidi tuanze upya, tuanze na kasi yako hii ambayo wewe mwenyewe umeanza nayo, na uhimize kwamba Halmashauri zetu kweli zihakikishe kuwa na vipimo na watalaam wanaoeleweka, na zaidi sana naomba Wapimaji wawepo katika ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi hatimiliki za kimila naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha, atusaidie, kwa sababu kuna baadhi ya benki zinasema, hizi hati za kimila zimeanzishwa kisiasa na kwamba hazitambuliki kisheria, na kwa maana hiyo, watu wanashindwa kuzichukulia dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. ABAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nawashukuru wananchi wa Temeke, nipo hapa kwa niaba yao. Namshukuru sana Mkurugenzi wa Temeke, nimeona wakati bajeti ya Wizara ikisomwa, tumeambiwa Temeke hatuna deni. Kwa hiyo, nampongeza sana Mkurugenzi na *DC* wetu mpya, lakini na wananchi wote wa *TMK* na Dar es Salaam kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia mke wangu na watoto wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutounga mkono bajeti hii. Sababu ya msingi ni matatizo yale yale ya bajeti iliyopita, mwaka 2011/2012 hayajatekelezwa. Wananchi wangu wa Temeke, tena wale wa Chama changu pia wakiniona naunga mkono, watanishangaa sana. Nami pia ndani ya Bunge hili nilichaguliwa ni Mjumbe wa *NEC* halali kabisa, ambaye sina tatizo, lakini kubwa, ni kutetea wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaunga mkono na sababu za msingi zinafahamika. Moja, pale Temeke tuna Kijiji cha Wavuvi, leo wananchi wa pale wote wanakimbia. Kuna tajiri mmoja *TRH* ameuziwa maeneo na *TAZARA* na Serikali tukitazama, yule Bwana amejenga mpaka kwenye maeneo ya vyanzo vya maji. Matokeo yake wale wananchi wote wa kule chini wanapata matatizo makubwa sana. Suala hilo lipo

Wizarani siku nyingi, karibu miaka mitano iliyopita. Wale wananchi, wengi wao mpaka wanataka kukimbia Chama change. Ni vitu vya kusikitisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nirejee suala la Kurasini, mradi wa toka mwaka 2006; kikubwa cha kusikitisha tulikuwa na Mkutano wa hadhara pale Jangwani, Waziri akasimama pale akaniita vizuri, kwa raha, na akasema pale: “Wananchi wa Kurasini, pesa zenu tumetenga kwenye bajeti, msiwe na wasiwasi.” Akaniambia: “Mtemvu, umenisikia?” Nikamwambia, nakusikia, tuko pamoja. Safari hii tukienda Dodoma tutacheza kidedea tu. Lakini cha ajabu, sioni pesa za mradi wa Kurasini. *(Kicheko/Makofi)*

Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kidogo tufanye staha. Sisi asili yetu kwanza tukiongea, hata kushangiliwa hatupendi, tunapenda tuseme tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia hapa, lile eneo la maji machafu Kurasini ambako kuna nyumba 210, kiasi cha pesa tulichostahili kulipwa pale wakati ule ni Shilingi bilioni 6.7, lakini cha ajabu na kusikitisha, naona hapa imetajwa Shimo la Udongo Shilingi bilioni 60 na pesa hizo najua ni mradi wa Wachina wa kutuwekea kituo cha biashara. Nashindwa kuelewa tunakwenda wapi. Hao wanaotudai siku nyingi hawamo kwenye bajeti, tumeruka tunakwenda kuongelea habari ya Shimo la Udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili sitaki linipotezee muda, kwa sababu nilishasema nyuma na cha

kusikitisha Mheshimiwa Rais wangu Mpendwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 20 Oktoba, aliagiza wananchi wale walipwe. Lakini pia tarehe 14 Machi, 2009 tulikwenda na Waziri Mkuu pale siku ya Jumamosi saa 3.00, Waziri Mkuu akawasikiliza, naye akaagiza walipwe. Waziri wa Ardhi Mama Tibaijuka mwenyewe tarehe tarehe 31 Machi, alikutana na wananchi pale akawaahidi na akawaambia mpaka yale macheleweshо mtalipwa. Lakini hadi leo hayajalipwa. Sasa hili sitaki linipotezee wakati, kwa kuwa mimi ni Mbunge pale, nimechaguliwa kwa kura nyingi kipindi cha pili, ninawapa taarifa tu kwamba nikirejea baada ya Bunge, kama wananchi wale hawakulipwa, nitasimamia mimi. Kwa sababu wanahitaji pale kununua, nitasimamia, tutauza yale maeneo. Hatuwezi kuwatesa wananchi, wananchi wanazuiwa hata kujenga choo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima twende kwa utaratibu. Mradi wa miaka miwili, muda umepita, tunasubiri nini tena? Mradi ule toka mwaka 2006 mpaka leo tunatesa watu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale Kurasini Mungu amejalia, linajengwa Daraja, *NSSF* kushirikiana na Serikali na wengine. Nashukuru sana Uongozi wa Serikali katika hili, na ninaishukuru sana *NSSF,* Dkt. Ramadhan Dau na wenzake. Lakini cha kusikitisha, Wizara ya Ardhi, kwa sababu Temeke ninaijua ni yangu, Wizara ya Ardhi walitenga eneo kwa ajili ya daraja hilo, wakalipa fidia karibu Shilingi bilioni mbili na kitu. Lakini cha kusikitisha, Wizara ya Ujenzi wakaja wakalibadilisha lile eneo, wakaenda eneo lingine. Eneo la wananchi ambao

walinunua pale wakalipa fidia, sasa leo wananchi wanateseka.

Nakuomba sana Waziri ufanye utaratibu uwalipe wale wananchi. Mila zetu za Mjini ukidhulumu ukajenga kitu, kile kitu hakina Baraka. Daraja lile wananchi wamelingoja kwa siku nyingi, wana hamu nalo, wanalipenda. Sisi Wabunge tumehangaika kulitafuta lile daraja, miaka karibu mitano iliyopita. Wahusika wanajua. Kwa hiyo, tunaomba muwalipe wenyewe msiwadhulumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua, wenzangu wameongea, hatuoni kama Wizara mna dhamira kweli ya kuwasaidia Watanzania. Tulitarajia leo mje na mpango mzuri wa upimaji wa viwanja na yale makisio tuliyoambiwa na Mbunge mmoja ya Shilingi bilioni 20 zipatikane. Lakini pia Waziri utuambie, hivi leo mimi nikiomba hati kisheria, natakiwa nipate hati ile kwa muda gani? Nina uhakika hili eneo la hati na zile hati za kimila mngetumia vizuri mngeweza kukusanya mapato mengi sana ya kuisaidia Wizara. Lakini leo mimi Mbunge mzima najifikiria, mimi na wale wa chini, ni mwaka wa saba leo natafuta hati. Kwa hiyo, mjipange vizuri eneo hilo linaweza kuwasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamepongeza uongozi wa *National Housing* na mimi nisiwe mnafiki katika hili, naupongeza Uongozi wa *National Housing* unaoongozwa na rafiki yetu mpendwa. Wao nawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini nirejee maazimio tuliyosema hapa

Bungeni mwaka 2008, 2009 na mwaka 2010, kuhusu nyumba za *National Housing* za wale wanaoishi wa kipato cha chini. Tulikubaliana wauziwe na bajeti iliyopita, Naibu Waziri alizungumza hapa. Lakini leo nashangaa, naona Makamu Mwenyekiti wa Kamati anaongea maneno ya ajabu na walikuwa kwenye Kamati hii toka ile miaka mitano tulipopitisha haya. Lakini wanaongea maneno ya ajabu kabisa! Inasikitisha, kwa sababu walikuwepo, wanayajua! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mara nyingine watu wanaweza kuhisi kuna mambo yamefanyika. Sisi tunataka kauli ya Mheshimiwa Waziri atamke hapa kwamba zile nyumba zimesitishwa kuuzwa na Serikali, na mtupe sababu za kusitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wapo watu waliuziana wakati huo, hawa wanyonge kwa nini tunawanyima? Kwa hiyo, mtupe sababu, lakini siyo mtu wa Kamati ambaye alikuwepo kwenye Kamati hiyo na alishiriki, leo kwa mafuta, anasimama pale anaongea mambo ya ajabu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la kusikitisha kabisa, zile nyumba za siku nyingi, leo zimekwenda kujengwa nyumba mbele ya nyumba, hakuna mahali pa kuegesha magari, hata moto ukiwaka, gari ya zimamoto haipiti. Namwomba Mheshimiwa Waziri aende akatembelee haya maeneo, aende Temeke, aende Ilala na Ubungo. Ni mambo yanayosikitisha, tena ni mambo ambayo kwa kweli hayastahili katika

haki za binadamu na kwa kuwa Waziri alikuwa *UN-Habitat* akaangalie kama makazi yanajengwa vile, na tuwaombe mwende Mikoani mkajenge, Dar es Salaam pamejaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siuongi mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi na Makazi. Naomba nianze kwa kusema kwamba kwa kweli Serikali imefanya vizuri. Miaka kumi iliyopita au miaka kumi na mbili ilikuwa huwezi kupata hati, ilikuwa unapata kiwanja kina *offer* yenye *double allocation,* yaani ukikipata wewe, na mwenzio ana *offer* kama hiyo. Maeneo ya wazi yalikuwa yamevamiwa sana. Sasa hivi Serikali imejitahidi na mimi nadhani kuna haja ya kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri wa Ardhi - Mheshimiwa Prof. Tibaijuka, naomba aendelee na uzi huo huo, na kama walivyosema wenzangu, naomba akaze buti, anafanyakazi nzuri na Naibu wake. Tafadhali naomba waendelee kuchapa kazi. Watu wanahitaji utawala wa sheria katika ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mambo ambayo nataka Serikali ifafanue kwa wananchi na kwa Waheshimiwa Wabunge. Lipo tatizo la leseni za makazi. Tunaelewa kwamba watu wengi wanaishi Mijini. Mji kama Dar es Salaam inahitaji leseni za makazi,

kule vijijini watahitaji leseni za hati za kimila. Lakini kwa Miji kama Dar es Salaam na Miji mingine mikubwa kule ambako haiwezekani kupimwa hati kabisa, inabidi wapewe leseni za makazi. Rafiki yangu mmoja anakaa Kimara, akaniomba nimsaidie, nikamwambia kwani huna leseni ya makazi? Akaniambia sina, na ninahitaji kuchukua mkopo Benki. Nikamwambia huwezi kupata mkopo mpaka uwe na hati au leseni ya makazi. Nikamsaidia, nikaenda nikamwuliza Kamishana wa Ardhi na Kamishna akasema, hapa Kimara siyo leseni za makazi, ni hati. Kwa hiyo, uende Kinondoni uchukue Mpimaji, akakupimie, utachangia kidogo, na Serikali itachangia, lakini utapimiwa utapata hati. Nilipofika Kinondoni, nikawatafuta wapimaji, nao wakaniambia jambo lingine tofauti, kwamba hapana. Kimara ni wakazi wa nyumba kumi mpaka 30 wanajikusanya, halafu wanakusanya na pesa yao wanapeleka kwa Mtendaji wa Serikali za Mitaa na Mtendaji anapeleka Manispaa wanapimiwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikaona hili ni tatizo kwa kweli. Naiomba Serikali ifafanue, ni lipi ambalo lipo sawa? La Kamishna au la Manispaa, Wapimaji? Naomba pia vyovyote itakavyokuwa, Serikali kwenye Halmashauri za Wilaya iweke dirisha la leseni za makazi ili kila mwananchi aweze kujua na kuwepo na uwazi kwamba nikitaka leseni ya makazi nifanyaje. Napeleka *documents* gani? Nakwenda kulipa kiasi gani? Sambamba na hilo hata kama basi ni hati, kupimiwa, kwenda kuchukua *surveyors* uweze kuchangia kidogo wakupimie, naomba pia Halmashauri za Wilaya ziweke jambo hili wazi. Halmashauri ziweke dirisha la kupata hati na la kwenda kupimiwa, na waambiwe kabisa

kwamba ukija hapa unataka kupimiwa, unalipa unalipa kiasi kadhaa, kuliko hivi wananchi wanavyosumbuliwa, mtu hujui kwamba unatakiwa kulipa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kupeleka upimaji wa ardhi na kusajili hati katika Kanda. Mkoa wa Kilimanjaro hati zinasajiliwa Moshi Mjini, watu wa Arusha wanasajili Moshi, na naamini kwamba maeneo mengine zimepelekwa, na hii naona kama ni hatua kubwa muhimu badala ya watu kuja Dar es Salaam kwa ajili ya kutafuta hati; zinaweza zikachukuliwa kwenye Kanda zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nataka kuongea kuhusu uchache wa wapimaji. Kuna matatizo kweli ya uchache wa wapimaji walio na *qualification* za kutosha. Kwa mfano, Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Rombo, Wilaya ya Moshi Vijijini, Wilaya ya Mwanga, hakuna wapimaji. Wilaya zote hizi ziko mbalimbali. Kwa hiyo, ukitaka kupima ardhi yako, labda uende Manispaa ukamuombe Mkurugenzi akupe mpimaji. Kwa mwananchi wa kawaida hii, itakuwa ghali sana.

Naomba Serikali iliangalie hili, ili wapimaji wenye sifa za kutosha waweze kupelekwa katika maeneo hayo. Lakini sambamba na hilo, ni lile alilosema Waziri mwenyewe kwamba kuna haja ya kupata vifaa vya kupima kama *Total Station* na *GPS* na bila hivyo ni vigumu sana kufanya upimaji, na mwisho wa siku wananchi wataendelea kunung'unika kwa sababu ya kutoweza kupimiwa maeneo yao mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili. Inawezekana kabisa zikawekwa kwenye bajeti za Halmashauri za Wilaya, lakini inahitaji ufuatiliaji makini wa Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni sheria zilizopitwa na wakati, kwa mfano, Sheria ya *Rural Farm Land Acquisition and Re-grant*, sheria namba 30 ya mwaka 1966. *I stand to be corrected* kwa sababu mimi siyo Mwanasheria. Lakini sheria hii inampa mwekezaji/Mtanzania ambaye ana shamba eneo kubwa kulipa kodi ya ardhi ya Sh. 200/= kwa eka. Watalaam wangu kutoka Kilimanjaro wananiambia yuko mwekezaji analima maua, ana eka 320, kwa mwaka analipa kodi ya pango la ardhi Sh. 64,000/=. Hebu fikiria huyu analima maua, akitoa *rose* moja asubuhi pale *KIA* jioni liko *frank -foot* ni Dola ngapi? Lakini maduhuli ya Serikali yanayokusanya kwa mwaka ni Sh. 64,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ilete Muswada wa Kurekebisha Sheria kama hizi angalau Serikali iweze kupata pato la kutosha, angalau shamba mtu adaiwe Sh. 5,000/= kwa eka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu kuwapongeza Shirika la Nyumba, ni kweli wanafanya vizuri. Kwa mara ya kwanza tumeona nyumba za Shirika la Nyumba zimepakwa rangi. Zilikuwa hazipakwi rangi! Lakini mkakati wao wa kujenga nyumba nyingi kwa ajili ya kumsaidia mwananchi wa kipato cha chini, kwa kweli nyumba hizi ni ghali ukitegemea kwamba

vipato vya Watanzania siyo vikubwa. Kwa hiyo, naungana na wenzangu kuomba Serikali, hebu waangalie ni namna gani wasaidie Shirika la Nyumba. Hawa watu kama walivyosema wenzangu, wamekuwa *very creative, very innovative* na wana *ideas* nzuri za kuweza kusaidia Serikali yenyewe ili tuweze kupata pato la kutosha, lakini na mwananchi wa kawaida. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie, labda kweli kuna haja ya kuondoa kodi ya *VAT* kwenye *National Housing* ili waweze kupunguza bei hizi za nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nataka niongelee, ni Masjala za Ardhi za Vijiji. Kama tunahitaji kupata hati za kimila, sheria inasema, inabidi vijijini kuwe na masjala ya Ardhi ya Vijiji. Lakini haya Masjala ya Ardhi, Mheshimiwa Waziri amesema wanategemea Halmashauri za Wilaya zihamasishe wananchi kujenga. Lakini wananchi hawa wana mzigo mkubwa, tayari wanajenga shule, wanajenga hospitali, wanachangia kila kitu. Kwa hiyo, naomba basi kama inawezekana, Serikali nayo iseme pia wajenge, lakini mwisho wa siku Serikali iwasaidie angalau kupaua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kuweza kunipatia nafasi hii niweze kuchangia kwa ufupi kwenye bajeti iliyoko mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kutoa pole kwa familia moja ya Mkoa wa Tabora Manispaa, iliyopoteza baba na mama jana, tarehe 10 Julai, 2012, kwa sababu ya mgogoro wa ardhi. Nichukue fursa hii kumpongeza Mkuu wa Wilaya ya Tabora Manispaa, Mheshimiwa amejitahidi sana kuweza kushughulikia hili suala kwa haraka, lakini ni ishara tosha kwamba wananchi wengi wanapoteza maisha kwa sababu ya migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni kila kitu kinachozungumzia suala la maendeleo. Ukigusa rasilimali yoyote unagusa ardhi, wanyamapori ni ardhi, madini ni ardhi, kilimo ni ardhi, mifugo ni ardhi, kila kitu ni ardhi. Tatizo la kutojua jinsi ya kuweza kutumia ardhi yetu vizuri ndiyo ambacho kinasababisha kwamba sisi wenyewe Tanzania tunarudi nyuma badala ya kupiga hatua kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi, nampongeza Mheshimiwa Waziri, anajitahidi sana na amekuja na mikakati mizuri na mipango mizuri. Hawezi kuitekeleza kwa sababu hakuna fedha ya kuweza kutengeneza mipango hiyo. Hapa tutagawana, lakini kama Serikali haijawa na umuhimu wa kutafuta *resources* za fedha popote kwa maendeleo ya ardhi Tanzania, tutaendelea kugombana hapa siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuendelea kutegemea hii inayosema kasungura kadogo, kaswala kadogo, hakagawanyiki, ndiyo maana hata wananchi wamefika mahali wamechoka, miradi haipigi hatua,

wananchi wamekata tama, kwa sababu Serikali bado haijaja na mbinu, jinsi ya kuweza kutumia rasilimali ya ardhi kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianzia na masuala ya vijijini, Halmashauri zetu hazipewi fedha kwenye Kitengo cha Ardhi kwa ajili ya kupima. Maeneo yanayopimwa kwa ajili ya kilimo hayatoshi, ni madogo, yanayopimwa kwa ajili ya mifugo ni madogo, hayatoshi, hifadhi zenyewe kule zilipo hazijaainishwa. Mwananchi hajui mikapa ya mifugo yake, kwa sababu siyo kwamba anapenda, pengine mipaka haijaainishwa na kweli hawajapima. Migogoro inazuka kila siku! Tunasema tuna *land bank*, *land bank* hazipimwi hazijulikani ni matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Halmashauri hakuna wapima, hakuna vitendea kazi, hakuna rasilimali, yote haya kama hatuyafanyii kazi kama Serikali, hatuwezi kupiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye masuala ya uwekezaji, kumekuwa na mgogoro mkubwa, wawekezaji na wananchi hapa kila siku na kila Mbunge anayesimama hapa kazungumzia suala la mgogoro kati ya wawekezaji, ni kwa sababu Serikali haijafanya utafiti kwenye Mikoa yote kuainisha ardhi na *components* zilizopo kwenye ardhi; ardhi gani inafaa kwa kilimo cha mpunga, kilimo cha mahindi, kilimo cha mtama. Mwekezaji akija apelekwe *straight* kwenye eneo siyo mwekezaji anakwenda kuchagua, nataka hapa, *then* Serikali inaanza kuhamisha watu. Huo siyo utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Wizara iwezeshwe, ipime maeneo kwenye Mikoa mbalimbali, mwekezaji akija apelekwe *straight* kwenye eneo ambalo limeshajulikana tayari kwamba anataka kulima mahindi, Mkoa wa Mbeya, ndiyo mwenyewe anataka akalime. Anataka kulima mpunga, aende Tabora. Kwa hiyo, Serikali iwe inajua, iwepo kwenye *records*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye mfuko wa kupima *(Plot Development Revolving Fund),* jambo la kusikitisha kwenye *speech* ya Mheshimiwa Waziri, kasema kati ya fedha Shilingi milioni 606 zilizokopeshwa, Shilingi milioni 466 hazijarudi mpaka sasa hivi. Mfuko huu tulifurahi ulivyokuwa *introduced*. Tulijua kwamba Halmashauri nyingi watanufaika na huu mfuko kwa sababu ni mfuko wa kuendeleza maeneo ya ardhi. Lakini pia kwa sababu Serikali haiwezi kutoa kiasi cha kutosha, unakuwa na mzunguko, Halmashauri moja ikirudisha wanapewa wengine. Kitendo cha Shilingi milioni 606 kutokurudi mpaka hivi leo, Halmashauri nyingine zinakwama kupata huu mfuko. Lakini pia nashangaa Halmashauri zinapewa hizi hela kupima, wanapima maeneo, wanatangaza viwanja, wanauza viwanja, hawalipi kwenye Wizara, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala linguine, kuna baadhi ya Halmashauri ambazo zinawaibia wananchi. Wanapima maeneo, wanapima kwa mfano wana viwanja labda 10,000 wanatoa fomu za viwanja 100,000, kila kiwanja wanachaji Sh. 20,000/= mpaka Sh. 30,000/= kuja kujaza fomu wakati wakijua kwenye akili

yao kwamba viwanja tulivyonavyo ni 10,000. Vile viwanja vingine 90,000 siyo wizi? Zile fedha zinazotolewa kwenye fomu ambapo wananchi hawakupata viwanja, kwa nini hawarudishiwi wakati hajapata kiwanja? Huu ni wizi, Serikali iangalie, wananchi wanaona, hawa siyo vipofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi inayozuka kwenye Wilaya mbalimbali ikiwemo Wilaya yetu ya Urambo, tatizo la maeneo yaliyopimwa ni machache, kwa mfano unakuta wafugaji wanaingia kwenye kijiji wanapokelewa na Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, analipishwa ushuru wowote anaotakiwa, kila kichwa cha ng'ombe analipa, kichwa cha mbuzi analipa. Lakini wakijua kabisa kwamba maeneo yaliyoko ndani ya kijiji ni machache kutokana na kwamba rasilimali ni kidogo, hawapimi ya kutosha. Baada ya muda mfupi wanaanza kuambiwa kwamba wafugaji wamevamia wakati wameingizwa kwa utaratibu, wamelipa stahiki zinazotakiwa, wamelipa ushuru unaotakiwa, wanakaa miezi miwili wanaambiwa mmevamia. Hili ni tatizo, Serikali ihakikishe kila Kijiji wanapima maeneo kuainisha maeneo ya kilimo ni yapi, ya mifugo ni yapi na maeneo mengine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ningependa Mheshimiwa Waziri atuambie kwenye Mikoa iliyoko mbali na Dar es Salaam, mbali na Dodoma, mbali na maeneo ambayo yako jirani na rasilimali kama Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Rukwa ambapo mfuko wa *cement* ni Sh. 25,000/= ambapo

bati moja Sh. 20,000/= ambapo nondo haishikiki. Kuna mpango gani kuhakikisha wananchi wale wanapata nyumba bora kama wananchi wenzao? Tusije tukaanza kuangalia *National Housing* peke yake, *National Housing* inakwenda *strategically*.

Kule kijijini ambako wananchi wa Tabora hawana uwezo wa kununua *cement* ya Sh. 25,000/= ajenge nyumba, lakini anapenda akae kwenye nyumba nzuri. Wizara hii ya Nyumba imeandaa utaratibu gani? Ni nini kinafanyika kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata nyumba bora? Kwa sababu ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata nyumba bora, siyo wale ambao wanakaa mjini. Leo hapa Dodoma mfuko wa *cement* ni Sh. 13,000/= au Sh. 14,000/= mwisho. Tabora ni Sh. 25,000/=, ikifika Kaliua mwananchi gani mwenye uwezo huo? Naomba wakati wa ku-*wind-up* Mheshimiwa Waziri aniambie wananchi wanaoishi Tabora wananufaikaje kupata nyumba bora kama wananchi wengine ambao wako jirani na maeneo ambayo *cement* inapatikana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la utunzaji wa fukwe zetu. *Beach management* zetu Tanzania bado hatujaweza kuzipa uzito wa kutosha. Nchi yetu imepata bahati ya kuwa na *beach* nyingi sana, tena nzuri sana. Tatizo letu, maeneo ya *beach* karibu yote tumewapa wenye uwezo, ndiyo maana tunasema nchi inajengwa na wenye moyo, inaliwa na wenye meno. Wenye meno ni wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata bahati ya kwenda Brazil, nashukuru Ofisi ya Mheshimiwa Spika, ilinipatia fursa hiyo. Nilichojifunza Brazil ambacho kimeni-*impress* mpaka leo nasimama hapa na kuweza kusema, *beach* zote Brazil ni *public areas,* kila mwananchi ana fursa ya kwenda *beach* kucheza mpira, *netball*, watoto wanacheza pale, wazee wanafanya *jogging*, wengine wanakula chakula chao pale, *beach* zinapendeza. Nchi yetu *beach* tumewapa watu kuanzia Bagamoyo kule mpaka mwisho. Mtu anapewa *beach* anaweka uzio, analipisha wananchi wenzake kwenda *beach*. Zile ni *recreation areas.* Nataka Mheshimiwa Waziri atuambie, leo hapa *beach* za kwetu Tanzania maeneo ambayo bado hayajavamiwa ameandaa utaratibu gani kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata fursa ya kuweza kutumia *beach* kama rasilimali ambayo ni *public*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni usafi wa *beach. Beach* zetu ukienda kule saa nyingine unaweza ukashindwa kula chakula. *Beach* za Brazil kuna trekta linazunguka masaa 24 kuanzia mwanzo mpaka mwisho, halafu kuna kila mahali baada ya kilomita moja, baada ya hatua 10, 15 kuna sehemu ya kuwekea takataka. Mtu anakula dafu lake, nimekuta mpaka madafu ya Tanzania yako Brazil, mtu anakula dafu anaweka kwenye *dustbin* anaendelea kucheza mpira. *Beach* zetu haziridhishi, ni chafu! Hata kwa maeneo ambayo ni machache, tunaomba uwepo utaratibu maalum kuhakikisha kwamba zile *recreation areas* ni nzuri, zinakuwa safi, zinakuwa salama, sehemu ambayo ni *attractive* wananchi waweze kuzitumia.

Lakini kikubwa kila mwananchi anufaike na rasilimali ya *beach* kwa sababu ni ya wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu uko karibu kwisha, nitoe pongezi kwa *National Housing.* Nashukuru sana kwamba kwa kweli wanafanya kazi nzuri, kutegemea na huko nyuma tulikokuwa wamekuja *strategically* wana mipango mizuri. Lakini nyumba za National Housing hakuna mwananchi wa kawaida anayeweza kuinunua. Hii inasababisha na Serikali kutokuona umuhimu. *National Housing* inanunua *cement* bei ile ile, ananunua, nondo bei ya kawaida, *VAT* iko kila mahali, nyumba ikishakamilika inatakiwa *VAT*. Hivi kweli Serikali ina mpango wa kusaidia Mtanzania wa kawaida? Serikali inaangalia watu wa kada gani? Hasa ni wananchi wa huku chini ambao ni asilimaia 80 na wananchi wa hapa juu ambao ni asilimia 10 au ni hawa asilimia tano wa pale juu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ituambie wakati wa ku-*wind-up,* Wizara hii hapa ina mpango gani, Nyumba za *National Housing* ziweze kununulika na wananchi wa kawaida? Hakuna mwenye uwezo wa kulipa Shilingi milioni 190, hakuna! Kwa kipato gani? Kwa mshahara wa Sh. 100,000/= kwa mwezi? Naiomba sana Serikali, kwa nia na dhati, nzuri, kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anaishi kwenye nyumba nzuri, ahakikishe kwamba *National Housing* wanapunguziwa gharama za ujenzi, ikiwa ni pamoja kuwekewa huduma na Serikali, nyumba zao ziweke bei nzuri ambapo kila mwananchi mwenye uwezo na mwenye

dhamira ya dhati anaweza kuinunua au anaweza kupanga akaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, upanuzi wa uwanja wa ndege Mkoa wa Tabora. Maeneo yanayopanuliwa Kiwanja cha Ndege Mkoa wa Tabora ilikuwa ni maeneo ya wananchi, wamelima mpunga miaka yote tangu enzi za babu zao mpaka leo. Maeneo yale yamechukuliwa na Serikali kwa ajili ya kupanua Kiwanja cha Ndege. Jambo la kusikitisha, baadhi ya wananchi wengine ambao walikuwa na yale maeneo wameweka pembeni kwenye daftari la watakaofidiwa hawapo. Namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie, yapo malalamiko mengi na nitakuja na majina maalum. Yapo majina ambayo hutumika ufisadi, Viongozi wa Kata ambao ndio walikuwa wana-*register* yale majina, wanachagua mtu wanayempenda. Najua rushwa imetumika pia pale, maana rushwa imekuwa ni tatizo Tanzania nzima. Wale wazee ambao hawana uwezo wa kujitetea, wamewekwa *bench* ambapo ndio wenye haki ya kwanza ya kulipwa maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali kwamba hata kiwanja kikijengwa kama wananchi hawajaridhika, wale ambao walistahili...

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Kwa vile muda umekwisha, huyo alikuwa msemaji wetu wa mwisho. Kabla ya kuahirisha namwomba *AG* atupatie kwa ufafanuzi wa kisheria juu ya mwongozo wa Mheshimiwa Kangi Lugola.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nitekeleze moja ya majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola - Mbunge wa Mwibara, ilikuwa ni maneno ambayo yapo kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 31, yale maneno yaliyokolezwa; na anaposema kwamba "bila kupenda kuingilia uhuru wa Mabaraza," nimelazimika kuunda Tume ya Kuchunguza Baadhi ya Malalamiko. Wale watakaobainika wana makosa, watachukuliwa hatua stahiki. Suala sasa ni kwamba kama maneno hayo kwa jinsi na kwa namna, yanakiuka masharti yaliyoko kwenye kanuni ya 64 (1) (c) yanayosomeka kama ifuatavyo:-

"Bila kuathiri ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, (c) Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama au jambo lolote ambalo lilijadiliwa na kutolewa maamuzi kwenye Mkutano uliopo au uliotangulia na ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahsusi na vile vile hatapinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge isipokuwa tu kwa

kutoa hoja mahsusi inayopendekeza kuwa uamuzi huo uangaliwe upya.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mabaraza ya Vijiji, Mabaraza ya Kata ya Ardhi yanatekeleza majukumu ya utoaji wa haki kuhusu migogoro ya ardhi katika ngazi za Vijiji na Kata. Sasa ukisoma maelezo ya Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, maelekezo yako ni ya jumla na hakuna jambo au kesi mahsusi inayorejewa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. Isipokuwa anatoa taarifa ya kuunda Tume ya Kuchunguza Baadhi ya Malalamiko Yanayoathiri Ufanisi na Ambayo Yanaleta Utovu wa Uadilifu kwa Baadhi ya Wenyeviti.

Kwanza, Mabaraza haya yako chini ya Waziri na hayako kwenye muhimili wa Mahakama. Ina maana kwamba, Waziri anayo mamlaka na madaraka kamili ya kutoa maelekezo, maana watu wengi wanapendekeza, kwa sababu ya matatizo yanayozungumzwa kwa Mabaraza hayo, yarudishwe kwenye mhimili wa Mahakama ili yasiwe nje ya mfumo wa kawaida wa utoaji wa haki.

Sasa tofauti na kesi, miongozo iliyotolewa na Mheshimiwa Mwenyekiti, na pengine Spika, pale kulikuwa na kesi mahsusi ambayo unaweza kuitaja, inawahusu watu gani. Lakini hapa ni maelekezo ya jumla, na ukisoma pale juu bila kuathiri anasema Halmashauri zote nchini ziandae mpango utakaowezesha kuyaimarisha Mabaraza ya Vijiji na Mabaraza ya Kata ili yaweze kushughulikia migogoro ya ardhi kwa ufanisi katika ngazi hizo. Kwa hiyo,

Mheshimiwa Waziri anahimiza ufanisi ambao ni jambo la jumla na anaeleza ni kitu gani atafanya, amefanya anategemea kufanya ili kutatua malalamiko ya wananchi kuhusu Mabaraza haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri na namshauri ndugu yangu Mheshimiwa Alphaxard Lugola kwamba jambo hili ni tofauti na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, halivunji kanuni ya 64 (1) (c). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa *AG* nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu katika suala hili sasa ni kama maelezo ambayo *AG* ameyatoa. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Naomba pia niwatangazie kwamba *addendum* ya *Volume Four* ya hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi imeshakuwa *circulated* kwenu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kabla sijasitisha shughuli za Bunge, naomba niwataje ambao kesho wataanza kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Esther Matiko, ataendelea Mheshimiwa Riziki Lulida na wengine watatajwa. Nawashukuru, nawatakia jioni njema. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.42 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 12 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)